# MAOMBOLEZO

# YA

# SHAHIDI WA KARBALA

**MWANDISHI:**
**SEYYID ALI IBNI JA'AFAR IBNI TWAAWUS (664 HIJRIYA).**

**MTARJUMI NA MHAKIKI:**
**SHEKH SALIM NG'ANG'A MWEGA**

**Jina la kitabu:** Maombolezo ya Shaidi wa Karbala.
**Maudhui**: Historia ya Imam Husein (a.s.).
**Mtunzi:** Seyyid Ali ibni Ja'afar ibni Twaawus.
**Mtarjumi na mhakiki**: Shekh Salim Ng'ang'a Mwega
**Mchapishaji:** Madrasatul Imam Baqiril-uluum (a.s)
**Chapa ya**: Kwanza
**Chapa ya**: Negaresh.
**Idadi ya copy:**1000.
**Tarehe ya Usambazaji**:Agosti 2010.
Haki ya Usambaji imehifadhiwa na Mtarjumi na mwenezaji.

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

**Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu**

# YALIYOMO.

**MLANGO WA KWANZA**……………………………13
**MAMBO YALIYOJIRI KABLA YA MAPAMBANO YA KARBALA**…………………………………………..13
MALAIKA JIBRIL (A.S.) ANAELEZEA YATAKAYOMPATA IMAM HUSEIN (A.S.) KISHA MTUME (S.A.W.A.) AWAJULISHA UMMA WAKE…14
KUZALIWA KWA IMAM HUSEIN (A.S)…...………… 14
MU'AWIYA KUAGA DUNIA NA YAZID ACHUKUA BAI'A KUTOKA KWA WATU…………………………..19
YAZID AMUAMURU WALIID KUCHUKUA BAI'A KUTOKA KWA IMAM HUSEIN (A.S.)…………………20
NASIHA YA MARWAN KWA IMAM HUSEIN (A.S.) NA JAWABU LAKE IMAM…………………………………..20
IMAM HUSEIN (A.S.) AONDOKA NA KUELEKEA MAKKA…………………………………………………...22
BAADHI WAMNASIHI IMAM KUFANYA SULHU...…22
WATU WA AL-KUFA WAMUANDIKIA IMAM (A.S.) BARUA WAKIMWOMBA KUJA KWAO………………23
IMAM HUSEIN (A.S.) AMTUMA MUSLIM IBNI A'QIL KWENDA AL-KUFA AKIWA AMEBEBA JAWABU ZA BARUA ZAO……………………………………………...26
MUSLIM IBNI A'QIL AINGIA MJI WA AL-KUFA……26
BAADHI WAMWANDIKIA YAZID BARUA KUMJULISHA KUMHUSU MUSLIM, WAKIMUOMBA [illegible]A AMUUZULISHA NU'UMAN………….............26
YAZID AMTEUWA UBEIDULLAH IBNI ZIYAD KUWA MTAWALA WA AL-KUFA…………………………...27
IMAM HUSEIN (A.S.) AWAANDIKIA VIONGOZI WA BASRA BARUA AKIWAITA ILI KUMNUSURU………27

YAZID IBNI MAS’UD AMWANDIKIA IMAM HUSEIN (A.S.) AKIMJULISHA KUWA MAKABILA YAMEUNGANA ILI KUMNUSURU……………………29
ALICHOFANYA MUNDHIR IBNI JAARUD KUHUSIANA NA BARUA YA IMAM (A.S.) PAMOJA NA MTUME WAKE HUSEIN (A.S.)…………………….30
UBEIDULLAH IBNI ZIYAD AONDOKA BASRA AKIELEKEA MJI WA AL-KUFA……………………..31
MUSLIM IBNI AQIL AONDOKA KWENYE NYUMBA YA ALMUKHTAR NA KUHAMIA KWA NYUMBA YA HANI……………………………………………....31
HANI AENDA KWA UBEIDULLAH IBNI ZIYAD PAMOJA NA YALIYOJIRI BAINA YAO……………….32
MADH-HAJ WAIZINGIRA IKULU WAKITAKA HANI AACHWE HURU………………………………………36
MUSLIM ATOKA KUPIGANA NA JESHI LA UBEIDULLAH IBNI ZIYAD…………………….....37
MUSLIM ASEMEZANA NA UBEIDULLAH IBNI ZIYAD BAADA YA KUSHIKWA MATEKWA………………….38
MUSLIM IBNI AQIL AFA SHAHIDI……………………40
HANI IBNI U’RWA AFA SHAHIDI……………………..40
IMAM HUSEIN (A.S.) AONDOKA MJI WA MAKKA…41
KHUTBA YA IMAM HUSEIN (A.S.) ALIPOAZIMIA KUELEKEA MJI WA IRAQ…………………………...43
MUHAMMAD IBNIL HANAFIYYAH APINGA KUTOKA KWA IMAM HUSEIN (A.S.) KWENDA IRAQ…………44
IMAM HUSEIN (A.S.) AFIKA DHATU A’RAQ NA KUKUTANA KWAKE NA BISHRU IBNI GHALIB…....46
IMAM HUSEIN (A.S.) AFIKA THA’ALABIYA NA ALIYOONA KWENYE NDOTO YAKE…………………46
ZUHEIR IBNIL QAIN AJIUNGA NA KUNDI LA IMAM HUSEIN (A.S.)...........................................................

ALQAIM ISLAMIC ASSEMBLY OF KENYA
(AL-IS-A-K)
مجلس القائم الاسلامي في كينيا

IMAM HUSEIN (A.S.) AFIKA ZUBALA, NA KUPASHWA HABARI ZA KUUWAWA KWA MUSLIM……………………………………………..47
IMAM HUSEIN (A.S.) AKUTANA NA FARAZDAQ…..49
IMAM HUSEIN (A.S.) AWAANDIKIA MASWAHABA WAKE BARUA WALIOKO MJI WA AL-KUFA NA YALIYOMFIKIA MTUME WAKE…………………....50
IMAM HUSEIN (A.S.) AKUTANA NA HURR NA YALIYOJIRI BAINA YAO...........................................51
KHUTBA YA IMAM HUSEIN (A.S.) HURR ALIPOWAFUNGIA NJIA……………………………...52
ALIYOYASEMA ZUHEIR IBNIL QAIN BAADA YA KHUTBA YA IMAM (A.S.)……………………………53
ALIYOYASEMA HILAL IBNI NAFI'I ALBAJALI, NA ALIYOYASEMA BUREIR…………………………….54
IMAM HUSEIN (A.S.) AFIKA KARBALA NA KUSOMA BETI ZA MASHAIRI ZINAZOASHIRIA KUHUSU KUFA KWAKE SHAHIDI……………………………………..54
ALICHOKIFANYA BIBI ZAINAB (A.S.) BAADA YA KUZISIKIA BETI……………………………………....55
SABABU AMBAZO HUENDA ZILIMFANYA IMAM HUSEIN (A.S.) KUWABEBA WATU WAKE WA NYUMBANI PAMOJA NAYE………………………...57
**MLANGO WA PILI**…………………………………...58
**YALIYOJIRI KATIKA UWANJA WA MAPIGANO NA KABLA YA MAPIGANO**............……………………58
IMAM HUSEIN (A.S.) AWAHUTUBIA MAADUI NA KUTIMIZA HOJA JUU YAO………………………….58
JIBU LA ABBAS (A.S.) NA NDUGU ZAKE SHIMRI ALIPOWAPA AMANI……………………………….....61
IMAM HUSEIN (A.S.) AWAOMBA MAADUI MUHULA USIKU HUO ILI KUJISHUGHULISHA NA IBADA…62
IMAM HUSEIN (A.S.) AOTA NDOTO………………….62

ALQAIM ISLAMIC ASSEMBLY OFKENYA
(AL-IS-A-K)
مجلس القائم الاسلامي في كينيا

IMAM (A.S.) AWAKHUTUBIA MASWAHABA WAKE NA KUWARUHUSU KUONDOKA……………………..63
WALIYOSEMA NDUGU ZAKE NA WATU WAKE WA KARIBU………………………………………………...63
ALIYOYASEMA SA'ID IBNI ABDILLAH ALHANAFI NA ZUHEIR IBNIL QAIN NA BAADHI YA MASWAHABA……………………………………….....64
ALIYOYASEMA MUHAMMAD IBNI BASHIR ALIPOJULISHWA KUWA MWANAWE AMESHIKWA MATEKA…………………………………………………65
BUREIR AMFANYIA UTANI ABDUR RAHMAN ASUBUHI YA SIKU YA ASHURA……………………...66
KHUTBA YA IMAM HUSEIN (A.S.) MBELE YA JESHI LA IBNU SA'AD AKIWANASIHI NA KUWAKUMBUSHA BARUA ZAO WALIZOMTUMIA……………………………………..67
U'MAR IBNI SA'AD ATANGULIA NA KUWATUPIA MSHALE WA KWANZA JESHI LA IMAM HUSEIN (A.S.)……………………………………………………70
WAKAPIGANA KWA MUDA NA KIKUNDI KATIKA JESHI LA IMAM HUSEIN (A.S.) KIKAUWAWA……...71
KUJIUNGA KWA HURR NA JESHI LA IMAM HUSEIN (A.S.) NA KUFA KWAKE SHAHIDI………………………………………………..72
KUPIGANA KWA BUREIR NA KUFA KWAKE SHAHIDI………………………………………………..73
KUPIGANA KWA WAHAB IBNI HABAAB NA KUFA KWAKE SHAHIDI……………………………………..74
KUPIGANA KWA MUSLIM IBNI A'USAJA NA KUFA KWAKE SHAHIDI……………………………………..75
KUPIGANA KWA UMAR IBNI QARDHA AL-ANSWARI NA KUFA KWAKE SHAHIDI…………………………
KUPIGANA KWA JON MTUMWA WA ABU DHAR NA KUFA KWAKE SHAHIDI………………………………..76

KUPIGANA KWA UMAR IBNI KHALID AS-SWAIDAWI NA KUFA KWAKE SHAHIDI…………………………...77
KUPIGANA KWA HANDHALA IBNI AS'AD ASH-SHAMI NA KUFA KWAKE SHAHIDI………………….77
SWALA YA IMAM HUSEIN (A.S.) NA MASWAHABA WAKE…………………………………………………..78
KUPIGANA KWA SUWEID IBNI AMRU IBNI ABIL MUTWAA'I NA KUFA KWAKE SHAHIDI…………….79
KUPIGANA KWA ALI IBNIL HUSEIN (A.S.) NA KUFA KWAKE SHAHIDI……………………………………..80
KUPIGANA KWA QASIM IBNIL HASAN (A.S.) NA KUFA KWAKE SHAHIDI………………………………82
IMAM HUSEIN (A.S.) ABAKI PEKEE, KISHA ANADI KWA SAUTI AKIOMBA NANI ATAKAYE MNUSURU………………………………………………..84
MWANA MCHANGA WA IMAM HUSEIN (A.S.) AFA SHAHIDI……………………………………………..84
IMAM HUSEIN (A.S.) AMPANDA FARASI WAKE, NA KUELEKEA ALFURAT WAKIWA ABBAS (A.S.)……..86
ABBAS (A.S.) AFA SHAHIDI……………………………86
IMAM HUSEIN (A.S.) APAMBANA NA MAADUI MAPAMBANO MAKALI……………………………...92
MAADUI WAMZUIA IMAM HUSEIN (A.S.) KUZIFIKIA HEMA……………………………………………………..93
KUTOKA KWA ABDULLAH IBNIL HUSEIN – KIJANA MCHANGA – NA KUFA KWAKE SHAHIDI…………95
SHIMRI AZIVAMIA HEMA ZA IMAM HUSEIN (A.S.)…………………………………………………96
IMAM HUSEIN (A.S.) AVAA NGUO ILIYORARUKA ILI ASIJE AKAPORWA AKAACHWA UCHI………………96
IMAM HUSEIN (A.S.) AFA SHAHIDI…………………..97
MALAIKA WAANGUA KILIO BAADA YA IMAM HUSEIN (A.S.) KUFA SHAHIDI……………………...99
MAADUI WANAMPORA IMAM HUSEIN (A.S.)…… 101

MAADUI WAZITIA MOTO HEMA ZA IMAM HUSEIN (A.S.)……………………………………………………103
BIBI ZAINAB (A.S.) AMUOMBOLEZA KWA SAUTI YENYE KUHUZUNISHA…………………………….104
BI SUKEINA (A.S.) AUKUMBATIA MWILI WA IMAM HUSEIN (A.S.)…….......................................................106
WALIUKANYAGAKANYAGA MGONGONI WA IMAM HUSEIN (A.S.) KWA FARASI……………………….106
MTU KATIKA JESHI LA IBNI SA’AD AMUONA MTUME (S.A.W.A.) KWENYE NDOTO NA MTUME KUMPAKA KWENYE MACHO YAKE WANJA WA DAMU KISHA KUAMKA AKIWA AMEPOFUKA….108
KATIKA SIKU YA QIYAMA BIBI FATIMA (A.S.) ATAWEKEWA HEMA YA NURU AMBAPO ATATAKA KISASI CHA IMAM HUSEIN (A.S.) KULIPIZIWA KUTOKA KWA WAUWAJI WAKE……………………109
**MLANGO WA TATU**………………………………111
**MAMBO YALIYOJIRI BAADA YA KUUWAWA KWA IMAM HUSEIN (A.S.)**……………………………….112
U’MAR IBNU SA’AD AMTUMIA IBNU ZIYAD KICHWA CHA IMAM HUSEIN (A.S.) PAMOJA NA VICHWA VYA MASHAHIDI WENGINEO……………112
IBNU SA’AD AWABEBA AYALI WA IMAM HUSEIN (A.S.) NA KUWAPELEKA KWA IBNU ZIYAD………112
MAKABILA YANAGAWANA VICHWA ILI KUMPELEKEA IBNU ZIYAD……………………….113
WATU KATIKA KABILA LA BANI ASAD WAIZIKA MIILI YA MASHAHIDI………………………………114
MIONGONI MWA MATEKA ALIKUWA IMAM SAJJAD (A.S.) NA HASAN ALMUTHANNA NA ZAID NA AMRU……………………………………………………11[illegible]
KHUTBA YA BIBI ZAINAB (A.S.) ALIPOINGIA MJI [illegible] AL-KUFA………………………………………………115
KHUTBA YA BIBI FATIMA AS-SWAGHIRA (A.S.)…11[illegible]

KHUTBA YA BIBI YA UMMU KULTHUM BINTU ALI (A.S.)……………………………………………………123
KHUTBA YA IMAM ZAINUL ABIDIN (A.S.)………125
IBNU ZIYAD AKETI KWENYE IKULU NA KUWAPA WATU WOTE IDHINI KUJA KUWAONA MATEKA..128
BIBI ZAINAB (A.S.) ASEMEZANA NA IBNU ZIYAD…………………………………………………129
IMAM SAJJAD (A.S.) ASEMEZANA NA IBNU ZIYAD NA AZIMIO LAKE KUTAKA KUMUUWA IMAM (A.S.)……………………………………………………..130
KICHWA CHA IMAM HUSEIN (A.S.) CHAZUNGUSHWA KWENYE MJI WA AL-KUFA…131
UPINZANI WA ABDULLAH IBNU AFIF KWA IBNU ALIPOMSHUTUMU IMAM HUSEIN (A.S.), ZIYAD KISHA KUFA KWAKE SHAHIDI……………………132
ZAINAB BINTU AQIL (A.S.) AMUOMBOLEZA IMAM HUSEIN (A.S.)…………………………………………136
MSAFARA WA MATEKA HADI MJI WA SHAM……137
MTU MIONGONI MWA WALIOKIBEBA KICHWA CHA IMAM HUSEIN (A.S.) ASIMULIA ALIVYOONA KUSHUKA KWA MITUME (A.S.) NA MALAIKA (A.S.) KANDO YA KICHWA CHAKE KITUKUFU…………137
IMAM SAJJAD (A.S.) ASEMEZANA NA MTU ALIYEONYESHA FURAHA KWA KUUWAWA IMAM HUSEIN (A.S)………………………………………………140
MATEKA WAINGIZWA NA KULETWA MBELE YA YAZID HUKU WAKIWA WAMEFUNGWA KWA MAKAMBA………………………………………………141
ALIYOYASEMA BIBI ZAINAB (A.S.) ALIPOKIONA KICHWA KITUKUFU CHA IMAM HUSEIN (A.S.)...142
MWANAMKE KATIKA BANI HASHIM AMUOMBOLEZA IMAM HUSEIN (A.S.) KATIKA NYUMBA YA YAZID (LA'ANAHULLAH)…………142

AL-QAIM ISLAMIC ASSEMBLY OF KENYA
(AL-IS-A-K)
مجلس القائم الاسلامي في كينيا

ABU BARZA AL-ASLAMI APINGA KITENDO CHA YAZID ALIPOMWONA AKIYACHOKORA MENO YA IMAM HUSEIN (A.S.) KWA KIJITI……………………143
YAZID ASOMA BETI ZA MASHAIRI YA IBNUZ ZAB’ARI………………………………………………143
KHUTBA YA BIBI ZAINAB (A.S.) AKIMKIMBUSHA YAZID KUFURU YAKE NA MAOVU YAKE……………………………………………………….144
YALIYOJIRI MTU MMOJA ALIPOMWAMBIA YAZID, NIPE HUYU MJAKAZI, AKIMKUSUDIA FATIMA……………………………………………..151
YAZID AMUAMURU KHATIBU KUKHUTUBU NA KUMUAMURU KUMTUKANA IMAM HUSEIN (A.S.) NA MAJIBU YA IMAM SAJJAD (A.S.) ALIYOTOA…152
ALIYOYAONA BI SAKINA (A.S.) KWENYE NDOTO…………………………………………………..153
RA-ASUL JAALUT ASHANGAZWA NA WAISLAMU KUMUUWA MWANA WA BINTI YA MTUME WAO (S.A.WA.)……………………………………………153
ALIYOSEMA MFALME WA ROMA KUMWAMBIA YAZID BAADA YA KUKIONA KICHWA CHA IMAM HUSEIN (A.S.). ………………………………………154
AL-MINHAL IBNI AMRU AKIWA PAMOJA NA IMAM SAJJAD (A.S.)……………………………………156
YAZID AMWITA IMAM SAJJAD (A.S.) NA KUMWAMBIA ATAJE HAJA TATU…………….........157
MATEKA WAONDOKA SHAM NA KUFIKA KATIKA MJI WA IRAQ KISHA KWENDA KARBALA………158
MAJINI WAMUOMBOLEZA IMAM SAJJAD (A.S.)…159
MATEKA WAIACHA KARBALA NA KUELEKEA MADINA, KISHA BISHRU AMWOMBOLEZA IMAM HUSEIN (A.S.)……………………………………………[illegible]
MJAKAZI AMUOMBOLEZA IMAM HUSEIN (A.S.)…………………………………………………16[illegible]

WATU WAMTOLEA RAMBIRAMBI IMAM SAJJAD (A.S.), KISHA IMAM AWAKHUTUBIA………………161
SWAUHAN IBNI SWA'ASWA'A AMUOMBA IMAM (A.S.) AMUWIYE RADHI………………………………163
ALIYOSEMA SEYYID IBNI TWAAWUS KATIKA KHATIMA YA KITABU CHAKE KUHUSU KUOMBOLEZA KWA NYUMBA NA MAJENGO KWA AJILI YA KUWAPOTEZA WENYE KUZIHAMI……164
IMAM SAJJAD (A.S.) AMUOMBOLEZA BABAKE ALIYEUWAWA SHAHIDI……………………………168
**MAMBO YA AJABU YALIYODHIHIRI BAADA YA IMAM HUSEIN (A.S.) KUUWAWASHAHIDI**………171

# MLANGO WA KWANZA.

# MAMBO YALIYOJIRI KABLA YA MAPAMBANO YA KARBALA.

## KUZALIWA KWA IMAM HUSEIN (A.S).

Imam Husein (a.s.) alizaliwa katika siku ya tano ya mwezi wa sha'abani, mwaka wa nne hijriya.
Wengine wamesema kuwa ilikuwa katika siku ya tatu ya mwezi huo.
Na wengine wamesema kuwa ilikuwa mwisho wa rabi'ul awwal (mfungo sita) mwaka wa tatu hijriya.
Na kumepokewa riwaya nyinginezo tofauti na hizi.
Ummul Fadhli mke wa A'bbas (ibni A'bdil Muttalib) (ridhwanullahi anhuma) amesema "Niliona kwenye ndoto kabla ya kuzaliwa kwake, kana kwamba kipande cha nyama ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kimekatwa na kuwekwa mapajani mwangu, nikamwomba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) tafsiri yake, akaniambi: Umeona kheri.Ikiwa ndoto yako ni ya kweli, basi Fatima atamzaa mwana wa kiume, nami nitakupa ili umnyonyeshe."
Ummul Fadhli anasema "Basi mambo yakawa kama alivyofasiri (s.a.w.w.).
Siku moja nilimleta, nikamweka mapajani mwake Mtume, alikojoa na likaruka tone la mkojo kwenye nguo ya Mtume (s.a.w.w.), nikambinya akalia, Mtume (s.a.w.w.) akasema "Taratibu, ewe Ummul Fadhli! Nguo yangu hii itaoshwa, lakini umesha muumiza mwanangu."

## MALAIKA JIBRIL (A.S.) ANAELEZEA YATAKAYOMPATA IMAM HUSEIN (A.S.) KISHA MTUME (S.A.W.A.) AWAJULISHA UMMA WAKE.

Ummul Fadhl anaendelea kusimulia "Basi nikamwacha mapajani mwake, nikasimama kwenda kumletea maji.Nilipokuja nilimpata (swalawatullahi aleihi wa aalihi) analia.

Nikamwambia: Ni nini kinachokuliza, ya Rasulallah?
Akajibu: Jibrail (a.s.) amenijia na kunijulisha kuwa umma wangu utamuuwa mwanangu huyu, Mwenyezi Mungu asiwajaalie kupata uombezi wangu siku ya Qiyama."
Wapokezi wa hadithi wanasema: Imam Husein (a.s.) alipotimiza mwaka mmoja tangu kuzaliwa, Malaika kumi na wawili walimshukia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.). Mmoja kati yao alikuja katika umbo la simba, wa pili katika umbo la ng'ombe dume, wa tatu katika umbo la chatu, wa nne katika umbo la mwanadamu, na wanane waliobaki walikuja katika maumbo tofauti tofauti, nyuso zao zikiwa nyekundu, macho yao yakiwa katika hali ya kulia, huku wamezifunguwa mbawa zao, wakisema "Ya Muhammad! Yatampata mwanao Husein ibni Fatima yaliyompata Habil kutokana na Qabil, naye atapewa malipo mfano wa malipo ya Habil, naye aliyemuuwa atabeba madhambi mfano wa madhambi ya Qabil.
Kisha hakubaki mbinguni Malaika ila tu alimshukia Mtume (s.a.w.w.), na kila mmoja kati yao alikuwa akimtolea salamu na kumpa mkono wa ta'zia kwa kuuwawa Husein (a.s.), na kumjulisha thawabu atakazopewa, na kumuonyesha turba yake, naye Mtume (s.a.w.w.) akisema "Ewe Allah! Mtupe mwenye kumtupa, na muuwe mwenye kumuuwa, na usimpe alichokitaka kwa kumuuwa."
Mpokezi wa habari hizi anasema: Imam Husein (a.s.) alipotimiza miaka miwili, Mtume (s.a.w.w.) alitoka kwenye mojawapo wa safari zake, huko njiani alisimama na kusema "Inna lillahi wa inna ileihi raji-u'n" na machozi yake kutokwa na machozi.
Akaulizwa sababu ya kufanya hivyo, akajibu "Jibrail yuko hapa ananijulisha kuhusu ardhi iliyoko kwenye ukingo wa mto Furati inayoitwa Karbala, ambapo mwanangu Husein ibni Fatima atauwawa."
Akaulizwa "Nani atakayemuuwa ya Rasulallah?"

Akajibu “Mtu aitwaye Yazid.Sasa hivi ninaona (machoni mwangu) kufa kwake na kuzikwa (Husein).”
Kisha akarudi kutoka safarini akiwa mwenye huzuni nyingi, akapanda membar, akuhutubia na kutoa wa’adhi, huku Hasan na Hueina wakiwa mbele yake.
Alipomaliza khutba yake, aliuweka mkono wake wa kulia juu ya kichwa chake Imam Hasan na mkono wake wa kushoto juu ya kichwa chake Imam Husein, kisha akakiinua kichwa chake kuelekea mbinguni na kusema:

اللهم إن محمداً عبدك و نبيك و هذان أطائب عترتي و خيار ذريتي و أرومتي و من أخلفهما في أمتي و قد أخبرني جبرئيل (عليه السلام) أن ولدي هذا مقتول مخذول اللهم فبارك له في قتله و اجعله من سادات الشهداء اللهم و لا تبارك في قاتله و خاذله

“Ewe Allah! Hakika Muhammad ni mja wako na Mtume wako, na hawa wawili ni wazuri wa itra yangu , na wabora wa dhuria wangu na kizazi changu, na ndio ambao nitakao waacha wakiwa makhalifa katika umma wangu.Jibrail (a.s.) amenipa habari kwamba mwanangu huyu atauwawa akiwa hana wa kumnusuru.Ewe Allah! Basi mbarikie katika kuuwawa kwake na umjaalie miongoni mwa mabwana wa mashahidi.Ewe Allah! Usimbarikie muuwaji wake na mwenye kupuuza kumnusuru.”
Mpokezi wa habari hizi anaendelea kusimulia kwa kusema: Watu wakaangua kilio msikitini na kuomboleza.
Mtume (s.a.w.w.) akawaambia “Je, mnalia na hali ya kuwa hamtamnusuru?”
Kisha akarudi (swalatullahi aleihi) akiwa rangi yake imebadilika, uso wake ukiwa mwekundu, na kukhutubia khutba nyingine fupi, huku macho yake yanatiririka macho, akasema:

أيها الناس إني قد خلفت فيكم الثقلين كتاب الله و عترتي أهل بيتي و أرومتي و مزاج مائي و ثمرتي وإنهما لن يفترقا حتى يردا علي الحوض، ألا و إني أنتظرهما و إني لا أسألكم في ذلك إلا ما أمرني ربي أمرني أن أسألكم المودة في القربى فانظروا ألا تلقوني غدا علي الحوض و قد أبغضتم عترتي و ظلمتموهم وقتلتموهم

ألا و إنه سترد على يوم القيامة ثلاث رايات من هذه الأمة:

الأولى راية سوداء مظلمة و قد فزعت لها الملائكة فتقف عليّ فأقول من أنتم فينسون ذكري و

يقولون: نحن أهل التوحيد من العرب.

فأقول لهم: أنا أحمد نبي العرب و العجم.

فيقولون: نحن من أمتك يا أحمد.

فأقول لهم: كيف خلفتموني من بعدي في أهلي و عترتي و كتاب ربي؟

فيقولون أما الكتاب فضيعناه و أما عترتك فحرصنا على أن نبيدهم عن جديد الأرض.

فأولّي عنهم وجهي فيصدرون ظماءً عطاشاً مسودّة وجوههم.

ثم ترد على راية أخرى أشد سواداً من الأولى، فأقول لهم: كيف خلفتموني في الثقلين الأكبر و الأصغر، كتاب ربي و عترتي؟

فيقولون أما الأكبر فخالفنا و أما الأصغر فخذلناهم و مزقناهم كل ممزق.

فأقول: إليكم عني.

فيصدرون ظماء عطاشا مسودا وجوههم.

ثم ترد عليّ راية أخرى تلمع وجوههم نوراً. فأقول لهم: من أنتم؟

فيقولون: نحن أهل كلمة التوحيد و التقوى نحن أمة محمد (صلّى الله عليه وآله وسلّم) و نحن بقية أهل الحق، حملنا كتاب ربنا فأحللنا حلاله و حرمنا حرامه و أحببنا ذريّة نبيّنا محمد (صلّى الله عليه وآله وسلّم) فنصرناهم من كل ما نصرنا منه أنفسنا و قاتلنا معهم من ناواهم.

فأقول لهم: ابشروا فأنا نبيّكم محمّد، و لقد كنتم في دار الدنيا كما وصفتم. ثم أسقيهم من حوضي فيصدرون مَرويّين مستبشرين، ثم يدخلون الجنة خالدين فيها أبد الآبدين.

“Enyi watu! Hakika mimi nimeacha kati yenu vizito viwili, Kitabu cha Mweyezi Mungu, na itra yangu, watu wa nyumba yangu na kizazi changu, na mizaji ya maji yangu na tunda langu, na hakika viwili hivi havitotengana kamwe mpaaka vitakaponijia huko Hodhini (mwa Kauthar).Basi tambueni kuwa, hakika mimi ninavingojea (huko), nami siwaulizeni kuvihusu  ila tu alichoniamuru Mola wangu kuwauliza.Ameniamuru kuwaulizeni kuhusu kuwapenda watu wangu wa karibu, basi angalieni msikutane nami huko kesho kwenye Hodhi mkiwa mumewakasirisha kizazi changu na kuwadhulumu na kuwauwa.

Na tambueni kuwa zitanijia (kwenye Hodhi) siku ya Qiyama bendera tatu za watu wa umma huu: Ya kwanza itakuwa bendera (ya watu wenye nyuso) nyeusi zenye giza, zitakayowafanya Malaika kuwakimbilia.Watasimama mbele yangu, nami nitawaambia: Ni kina nani nyinyi?

Watasahao kunikumbuka, na watasema: Sisi ni wafuasi wa Tauhid katika waarabu.

Nami nitawaambia: Mimi ni Ahmad Mtume wa waarabu na wasiokuwa waarabu.

Kisha watasema: Sisi ni katika umma wako, ewe Ahmad.

Nami nitawaambia: Mliwatendeaje baada yangu watu wangu wa nyumbani na kizazi changu na Kitabu cha Mola wangu?

Nao watajibu: Ama Kitabu, basi tulikipuuza, na ama kizazi chako, tulitafuta kuwaondosha kabisa kwenye uso wa ardhi.

Nami nitawageuzia uso wangu (nisiwaangalie), nao wataondoka wakiwa (wenye midomo) kavu na wenye kiu, hali ya kuwa nyuso zao ni nyeusi.

Kisha itanijia bendera nyigine (ya watu wenye nyuso) nyeusi zaidi kuliko zile za kwanza, nami nitawaambie:
Mlivitendeaje baada yangu vizito viwili, kile kikubwa na kile kidogo, (yaani) Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Kizazi changu?
Basi hao watasema: Ama kile kikubwa, tulikipinga, na ama kile kidogo tulipuuza kukinusuru na tukakirarurarua.
Basi nitawaambia: Ondokeni mbele yangu.
Hapo wataondoka wakiwa (wenye midomo) kavu na wenye kiu, hali ya kuwa nyuso zao ni nyeusi.
Kisha itanijia bendera nyigine (ya watu wenye nyuso) zenye kung'ara kwa nuru.
Nami nitawaambia: Ni kina nani nyinyi?"
Watasema: "Sisi ndiyo watu wa neno la Tauhidi na UchaMungu, sisi ni umma wa Muhammad (s.a.w.w.) nasi ndiyo waliobaki katika watu wa haki, tulikibeba (vema) Kitabu cha Mola wetu, tukaihalalisha halali yake na tukaiharamisha haramu yake, na tuliwapenda kizazi cha Mtume wetu (s.a.w.w.), tukawanusuru katika kila tulichozinusuru nafsi zetu kutokana nacho, na tukapigana na kila aliyewafanyia uadui.
Nami nitawaambia: Furahini, kwani mimi ndiye Mtume wenu Muhammad, kwa hakika mliishi duniani kama mlivyosifia.
Kisha nitawanywesha maji kutoka ndani ya Hodhi langu (la Kauthar) nao wataondoka huku wamekata kiu chao wakiwa wenye furaha, kisha waingie peponi waishi humo milele na milele."

## MUAWIYA KUAGA DUNIA NA YAZID ACHUKUA BAI'A KUTOKA KWA WATU.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Watu walikuwa wamezoea kukumbushana mauaji ya Imam Husein (a.s.), na kuliona

kuwa jambo kubwa, na kungoja kwa makini kuja kwa siku hiyo. Basi Muawiya bin Abi sufyan alipoaga dunia katika mwezi wa rajabu mwaka wa sitini hijria, aliondoka duniani huku amemuachia mwanawe, Yazid kuwa khalifa.

## YAZID AMUAMURU WALIID KUCHUKUA BAI'A KUTOKA KWA IMAM HUSEIN (A.S.).

Yazid ibni Muawiya alimwandikia Waliid ibni Utba aliyekuwa amiri wa Madina akimuamuru kumchukulia baiah kutoka kwa wakazi wa Madina, na khususan kutoka kwa Husein bin Ali (a.s), na akamwambia kuwa "Akikataa kutoa baiah yake, basi kikate kichwa chake na kunitumia."
Waliid alimuita Marwan ibnil Hakam na kumuomba ushauri kuhusiana na Imam Husein (a.s).
Akamjibu "Hatokubali. Lao kama ningekuwa sehemu yako ningelikata kichwa chake." Waliid akasema "Laiti sikuja duniani kamwe."
Kisha akamtuma mtu kumlete Imam Husein (a.s.).Akamjia huku akiwa pamoja na watu thelathini miongoni mwa watu wake na wafuasi wake. Waliid akamjulisha kuhusu kifo cha Muawiya, na kumuomba kumbai Yazid.
Imam Husein akamwambia "Ewe amiri, baiah haitolewi kwa siri, lakini ukiwaita watu kesho basi tuite pamoja nao."

## NASIHA YA MARWAN KWA IMAM HUSEIN (A.S.) NA JAWABU LAKE IMAM.

Marwan akamwambia "Ewe amiri usikubali udhuru wake .Akikataa kutoa baiah basi kikate kichwa chake." Imam Husein (a.s.) akakasirika na kusema "Ole wako, yabnaz Zarqaa! Unaamuru kwamba kichwa changu kikatwe? Wallahi umedanganya na umekuwa duni kweli." Kisha akamwelekea Waliid na kumwambia "Ewe amiri sisi ni Watu

wa nyumba ya Utume na mahala pa ujumbe wa Mwenyezi Mungu, na watembelewa na Malaika..Mwenyezi Mungu ameanza kwa sisi na atamalizia kwa sisi .Yazid ni mtu fasiki ,mnyawaji wa pombe ,muuaji wa nafsi zisizo kuwa na hatia, anayefanya ufasiki waziwazi .Hastahiki hiki cheo ,na mfano wangu hawezi kumbai mfano wake.Lakini tungojee kukuche nanyi ngojeni kukuche ,tuangalie, nanyi muangalie ni nani kati yetu na nyinyi anayestahiki ukhalifa na baiah." Kisha akaondoka Imam (a.s.).

Marwan akamwambia Waliid "Umeniasi." Akamjibu "Ole wako ewe Marwan, hakika wewe umenielekeza kwenye kitu kitakachoniondolea dini na dunia yangu.Wallahi mimi singependi kwamba mali yote ya dunia iwe ni yangu na hali huku nimemuuwa Husein, Wallahi sidhani kuwa kuna mtu yeyote atakaye kutana na Mwenyezi Mungu akiwa na damu ya Husein ila tu mizani yake itakuwa ni khafifu, na wala Mwenyezi Mungu hatomwangalia siku ya Qiama na wala hatomtakasia matendo yake na atapata adhabu kali."

Mpokezi wa habari hizi anasema: Kukakucha, Imam Husein (a.s.) akatoka nyumbani kwake ili kusikiliza habari .Marwan akakutana naye, akamwambia "Ya Aba Abdillah , hakika mimi ni mwenye kukunasihi ,basi nitii ili uweze kuongoka." Imam Husein (a.s.) akasema, "Ni nini hicho? Sema nisikie (usemacho)."

Marwan akasema, "Ninakuamuru kumbai Yazid, Amirul muuminin, kwani ni bora kwako katika dini yako na dunia yako."

Imam Husein (a.s.) akasema:

(انا لله و انا اليه راجعون و على الاسلام السلام اذ قد بليت الامة براع مثل يزيد و لقد سمعت جدي رسول الله- صلى الله عليه و اله و سلم- يقول الخلافة محرمة علي آل ابي سفيان

“Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na hakika kwake tutaregea.Basi amani kwa uislamu, kwani uma umepatwa na balaa ya kuongozwa na kiongozi mfano wa Yazid. Nilimsikia Babu yangu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akisema kuwa: Ukhalifa ni haramu kwa aali Abi Sufyan.”
Mazungumzo yaliendelea kwa muda mrefu baina yake na Marwan hadi alipoondoka Marwan akiwa amekasirika.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AONDOKA NA KUELEKEA MAKKA.

Kulipo kucha Imam Husein (a.s.) aliondoka akielekea Makka, ikiwa ni siku ya tatu katika mwezi wa sha’aban, mwaka wa sitini.Akakaa huko kwa siku zilizobaki za mwezi wa sha’aban na ramadhan na shawwal na dhul qaadah.

## BAADHI WAMNASIHI IMAM (A.S.) KUFANYA SULHU.

Wakamjia Abdullah ibni Abbas (radhiyallahu anhu) na Abdullah ibni Zubeir wakimuashiria kuwa aache (kusafiri). Akawaambia “Mtume wa Mwenyezi Mungu aliniamuru jambo fulani, nami ni lazima kulitekeleza.”
Ibnu Abbas akatoka huku akisema “Waa Huseina!”
Kisha akamjia Abdullah ibni Umar akamuashiria kufanya sulhu na watu hawa wapotofu na kumtahadharisha kutokana na kupigana vita nao.
Akamjibu “Ewe Abu Abdur Rahman! Je hujui kwamba katika udhalili wa duniani hii ni kuwa kichwa cha Yahya bin Zakariya kinatolewa zawadi kupawa kahaba katika makahaba wa bani Israil.Je, hujui kwamba bani Israil walikuwa wakiwauwa Manabi sabini baina ya alfajiri na kuchomoza kwa jua kisha wakiketi masokoni mwao wakiuza na kununua kana kwamba hawakufanya chochote.Naye

Mwenyezi Mungu hakuwaharakishia (adhabu) bali aliwapa muhula, kisha akawachukua baada yake uchukuaji wa Mwenye nguvu na Mwenye uwezo.Mche Mwenyezi Mungu, ewe Abu Abdur Rahman, na wala usiache kamwe kuninusuru."

## WATU WA AL-KUFA WAMUANDIKIA IMAM (A.S.) BARUA WAKIMWOMBA KUJA KWAO.

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Watu wa al-Kufa walisikia kuhusu kufika kwa Husein huko Makka na kukataa kwake kumbai Yazid.Basi wakakusanyika nyumbani kwake Suleiman ibni Sward al-Khuza'i.Walipotimia wote alisimama kuwakhutubia, akasema mwisho wa khutba yake "Enyi kikundi cha mashia! Mmeshajua ya kwamba Muawiya ameshahiliki na kurudi kwa Mola wake na kwenda kukutana na matendo yake, na ameketi mahala pake mwanawe, Yazid .Na huyu ni Husein bin Ali (a.s.) amemkhalifu na amekwenda Makka akiwakimbia mataghuti wa aali Abi sufyan,nanyi ni mashia wake na mashia wa baba yake, kabla yake, na anahitajia nusra yenu leo .Ikiwa mnajua kwamba mtamnusuru na mtapigana jihadi na maadui wake, basi muandikieni barua.Na ikiwa mtaogopa udhaifu na kushindwa, basi msimhadae mtu huyu juu ya nafsi yake." Basi wakamwandikia (hivi):

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu.
(Barua) kwa Husein bin Ali Amirul muuminin (a.s) kutoka kwa Suleiman ibni Sward al-Khuza'i na Musayyab ibni Najbah na Rufa'ah ibni Shaddad na Habib ibni Madhahir na Abdullah ibni Wa-il na mashia wake wengineo katika waumini.

Salaamullahi aleika.Ama ba'adu, Himidi yote ni ya Mwenyezi Mungu aliyemuangamiza adui wako na adui wa baba yako kabla yako, aliyekuwa jabari, mwenye inadi, mwingi wa kudhulumu, aliyeunyang'nya umma huu uhuru wake, na kuwaibia mali yao, na kuwatawala kimabavu bila ya wao kumridhia, kisha akawauwa wema wake na kuwabakisha waovu wake, na kuifanya mali ya Mwenyezi Mungu kuwa inarudia baina ya majabari na wenye kiburi.Aangamizwe (na Mwenyezi Mungu) kama walivyoangamizwa (watu wa) Thamud.

Sisi hatuna Imamu ila wewe, basi njoo, huenda Mwenyezi Mungu akatukusanya pamoja nawe katika haki.

Nu'uman ibni Bashir yuko kwenye ikulu ya utawala, hatukusanyiki naye kamwe kwenye swala ya ijuma wala ya jamaa, na wala hatutoki naye kwenye sherehe za idi. Ikiwa tutapata habari ya kuwa unakuja, tutamuondosha na kumfanya aende Sham.

Was Salamu aleika yabna Rasulillah pamoja na baba yako kabla yako, wa la haula wa la quwwata illa billahil A'liyyil A'dhim.

Kisha wakaituma barua .Wakabaki siku mbili nyinginezo halafu wakakituma kikundi cha watu wakiwa na barua nyinginezo taqriban mia na hamsini zilizokuwa zimeandikwa na mtu mmoja au wawili au watatu au wane, wakimuomba aje kwao.Lakini yeye pamoja na hayo yote alikuwa anajicheleweshа bila kuwajibu.

Zikawa zimemjia kwa siku moja tu barua mia sita, bali zikaendelea kumjia kwenye nyakati tofauti tofauti hadi

kufikia barua elfu kumi na mbili.

Kisha wakamtembelea Hani ibni Hani as-Subai'i na Sai'd ibni Abdullah al-Hanafi wakimletea barua hii, ambayo ilikuwa barua ya mwisho kutoka kwa watu wa (mji) wa al-Kufa, ikiwa imeandikwa hivi:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu.
(Barua) kwake Husein bin Ali Amirul muuminin (a.s) kutoka kwa mashia wake na mashia wa baba yake Amirul muuminin (a.s).
Ama baadu, hakika watu wanakusubiri, na hawana rai nyingine ila wewe, basi haraka haraka yabna Rasulillah, kwani mashamba yamekuwa kijani, na matunda yameiva, na ardhi imemea nyasi ,na miti imeatoa matawi yake.Basi njoo kwetu utakapo, kwani utakuta jeshi lilitayarishwa kikweli.
Was Salaamu aleika wa Rahmatullahi wa Barakaatuh kwako wewe na baba yako kabla yako.

Imam Husein akamwambia Hani ibni Hani as-Subai'i na Sai'd ibni Abdullah al-Hanafi "Niambieni, ni nani waliokusanyika katika kuandika barua hii mliyonijia nayo?" Wakasema," Yabna Rasulillah! (Wameiandika) Shibthi ibni Rib'i na Hajjar ibni Abjar na Yazid ibni Harith na Yazid ibni Rawim na U'rwa ibni Qais na A'mru ibni Hajjaj na Muhammad ibni U'meir ibni A'twarid.
Hapo Imam Husein (a.s.) akasimama na kuswali rakaa mbili baina ya rukni na maqam, na kumuomba Mwenyezi Mungu kheri katika jambo hili.

## **IMAM HUSEIN (A.S.) AMTUMA MUSLIM IBNI A'QIL KWENDA AL-KUFA AKIWA AMEBEBA JAWABU ZA BARUA ZAO.**

Kisha akamwita Muslim ibni A'qil na kumjulisha hali ya mambo, na kumuandikia barua ya kuwajibu barua zao huku akiwaahidi kuwajia, na kuwaambia maneno yenye madhumuni haya, "Ninawatumieni binami yangu Muslim ibni A'qil ili aniarifu ni rai ipi mliyonayo."

## **MUSLIM IBNI A'QIL AINGIA MJI WA AL-KUFA.**

Muslim akaondoka pamoja na barua hadi kuingia katika mji wa al-Kufa.Walipoona barua yake walifurahishwa sana na kuja kwake, wakamkaribisha kwenye nyumba ya Mukhtar ibni Abi Ubeida ath-Thaqafi. Mashia wakawa ni wenye kumtembelea huko.

Walipokusanyika na kuwa kikundi, aliwasomea barua ya Husein (a.s.) huku wakilia.Wakambai miongoni mwao watu elfu kumi na nane.

## **BAADHI WAMWANDIKIA YAZID BARUA KUMJULISHA KUMHUSU MUSLIM, WAKIMUOMBA KUWA AMUUZULISHA NU'UMAN.**

Abdullah ibni Muslim al-Bahili na I'mara ibni Walid na U'mar ibni Sa'id walimwandikia Yazid wakimjulisha kumhusu Muslim ibni A'qil, na kumshauri kumuondoa Nu'uman ibni Bashir na kumteuwa mwengineo.

## YAZID AMTEUWA UBEIDULLAH IBNI ZIYAD KUWA MTAWALA WA AL-KUFA.

Naye Yazid akamuandikia U'beidullah binZiyad, aliyekuwa mtawala wa Basra, akimjulisha kuwa amemteuwa kuwa mtawala wa mji wa al-Kufa, na kumjulisha pia kumhusu Muslim ibni A'qil na Husein (a.s.), na kumsisitizia kumkamata Muslim na kumuuwa.
Basi U'beidullah akajitayarisha na kusafiri kuelekea mji wa al-Kufa.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AWAANDIKIA VIONGOZI WA BASRA BARUA AKIWAITA ILI KUMNUSURU.

Naye Imam Husein (a.s.) alikuwa ameshawaandikia barua kikundi cha viongozi wa Basra, akaituma pamoja na mtumwa wake aitwae Suleiman, na mwenye kun-yat ya abu Razin. Aliwaaita kwenye barua hiyo katika kumnusuru na kumfanyia utiifu .Wakiwemo kati yao Yazid ibni Masu'd an-Nah-shili na Mundhir ibni Jaarud al-A'bdi.
Basi huyu Yazid ibni Masu'd aliwakusanya bani Tamim na bani Handhala na bani Sa'ad. Walipofika aliwaambia "Enyi bani Tamim, je mnaonaje mahala pangu na cheo changu kati yenu?"
Wakasema "Pongezi! Pongezi! Wallahi wewe ni ute wa mgongo na kichwa cha fakhari, umechukua mahala pa kati pa sharafa, bali umetangulia katika sharafa kwa maradufu.
(Kisha) akasema "Hakika mimi nimewakusanyeni kwa jambo ambalo ninalotaka tushaurine nanyi kuhusiana nalo, na kuwaomba msaada juu ya jambo hilo."
Wakamwambia "Wallahi! Bila shaka tutakupa nasiha na kujitahidi kukutolea maoni yetu, basi semu tukusikie."
Akasema "Hakika Muawiya ameshakufa, na wallahi! Mwenyezi Mungu amesahilisha mambo kwa kumuangamiza

na kuumuondosha.Tambueni basi kuwa mlango wa ujeuri na maovu umevunjika, na nguzo za dhulma zimedhoofika.Alianzisha baiah ili kulifunga jambo fulani akidhani kuwa amelipa nguvu jambo hilo, lakini yuko mbali sana na alichokitaka. Alijitahidi lakini wallahi ameshindwa.Alitoa ushauri akapuuzwa.Naye mwanawe Yazid, mnywaji wa pombe, kichwa cha maovu, amesimama akidai ukhalifa juu ya waislamu na kujitawalisha juu yao, bila ya wao kuridhia.Yeye ni mtu asiyekuwa na upole, mchache wa elimu, asiyejua haki inapofaa kusimamishwa. Ninawaapieni kwa Jina la Mwenyezi Mungu, kiapo cha kweli, ya kwamba, hakika kupigana jihadi naye kwa ajili ya dini ni bora kuliko kupigana jihadi na washirikina.

Na huyu ni Husein ibni Ali mwana wa binti Rasulillah (s.a.w.w.), mwenye sharafa asili na mwenye rai thabiti, ana fadhila isiyayoweza kusifika, na elimu isiyokuwa na kifani, ndiye anayestashiki zaidi jambo hili, kutokana na kuwatangulia wote na umri wake na ukuruba wake kwa Mtume. Ni mwenye huruma kwa mdogo na mkubwa.

Basi ni utukufu ulioje ikiwa yeye atakuwa kiongozi wa raia, na Imam wa kaumu. Kupitia kwake Hoja ya Mwenyezi Mungu imetimia, na mawaidha yake yamefika.

Basi msipofuke mkakosa kuiona nuru ya haki, wala msikakamie katika baatil, kwani Swakhru bin Qais alikosa kunusuriwa nanyi siku ya (vita vya) Jamal. Basi yaosheni (makosa yenu) kwa kutoka ili kumnusuru ibnu Rasulillah (s.a.w.w).Wallahi, hatopuuza yeyote kumnusuru ila tu Mwenyezi Mungu atamrithisha udhalili katika kizazi chake na uchache katika jaamaa wa uko wake.

Mimi hapa nimeshavaa vazi la vita na deraya (yangu).Ambaye hakuuwawa (hatimae) atakufa, na mwenye kukimbia hakosi kupatikana. Basi rudisheni jawabu zuri rahimakumullah.”

Banu Handhala wakazungumza, na kusema “Ya Aba Khalid sisi ni mishale ya podo yako na wapanda farasi wa ukoo wako.Ukitutumia kama mishale yako yakutupia utawahi shabaha, na ukitutumia katika kupigana vita utashinda .Wallahi! hautoingia kwenye vita vyovyote, il tu tutaingi pamoja nawe, na wala hautokumbana wallahi na shida yoyote  ila tu sisi tutukumbana nayo.Tutakunusuru kwa mapanga yetu, na tutakukinga kwa miili yetu. Basi jitayarishe kwa kile ulichotaka.”

Kisha wakazungumza banu Sa’ad ibni Zaid, na kusema, “Ya Aba Khalid, hakika kinachotuchukiza zaidi sisi ni kukukhalifu na kupinga rai yako. Swakhru ibni Qais alituamuru kuacha vita, tukahimidi. Alituamuru tukabaki na utukufu wetu.Basi tupe muhula ili turudi kushauriana kisha tutakuletea maoni yetu.”

Banu A’mir ibni Tamim nao pia wakazungumza na kusema “Ya Aba Khalid, sisi ni wana wa baba yako tulioapizana kiapo cha undugu. Haturidhii unapokuwa umeghadhibika, wala hatukai majumbani unapokuwa umeondoka .Uamuzi ni wako, ukituita tutakujibu, na ukituamuru tutakutii, na uamuzi ni wako utakapotaka.”

Akasema, “Ya bani Sa’ad, mkifanya hivyo Mwenyezi Mungu hatowaondolea upanga kamwe, na utabaki upanga daima kati yenu (mkipigana).”

## YAZID IBNI MAS’UD AMWANDIKIA IMAM HUSEIN (A.S.) AKIMJULISHA KUWA MAKABILA YAMEUNGANA ILI KUMNUSURU.

Kisha akamwandikia Husein (a.s.):

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu.

Ama baadu, barua yako imenifikia, na nimefahamu ulichonisisitizia na ulichoniitia, yaani kuchukua hadhi yangu ya utiifu kwako na sehemu yangu katika kukunusuru. Hakika Mwenyezi Mungu hakuiacha ardhi bila mfanya kheri ndani yake, na bila mwongozaji kwenye njia ya wokovu.Nyinyi ndio Hoja wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake na Amana yake katika ardhi, mumetokana na mzeituni wa Ahmad, akiwa yeye ndiye mzizi wa mzeituni huo nanyi ndio matawi yake. Basi njoo, kwa sa'ada bora kabisa, kwani nimekudhalilishia shingo za bani Tamim, na nimewaacha wakiwa tayari kukufuata zaidi kuliko ngamia mwenye kiu anapokuwa na homa ya miundi anapoingia kunywa maji.Vilivile, nimekudhalilishia shingo za bani Sa'ad, na nimekuoshea uchafu wa vifua vyao kwa maji ya wingu la mvua hata umeme wake ulipopiga na kuviangazia vikameremeta.

Imam Husein (a.s.) alipoisoma barua hii alisema "Mwenyezi Mungu akupe amani siku ya khofu na akutukuze na kukuondolea kiu katika siku ya kiu kikali." Alipojitayarisha huyu ili kwenda kumnusuru Husein (a.s.) alileletewa habari kabla ya kuanza safari yake ya kwamba ameshauwawa. Akahuzunishwa sana kwa kutoweza kumfikia.

## ALICHOFANYA MUNDHIR IBNI JAARUD KUHUSIANA NA BARUA YA IMAM (A.S.) PAMOJA NA MTUME WAKE HUSEIN (A.S.).

Na ama Mundhir ibni Jaarud, basi yeye alimchukua mjumbe na kumleta pamoja na barua aliyoileta kwa U'baidullah bin

Ziyad, kwa kuwa Mundhir alikhofia kuwa huenda ikaw barua ile ilikuwa ni njama kutoka kwake U'baidullah ibni Ziyad, na hali ya kuwa Bahriyyah bintu Mundhir alikuwa mkewe U'baidullah.
U'baidullah alimchukua yule mjumbe na kumsulubisha.Kisha akapanda juu ya member na kuhutubia na kuwaonya watu wa Basra kutojaribu kukhalifu na kuzusha fitna.

## UBEIDULLAH IBNI ZIYAD AONDOKA BASRA AKIELEKEA MJI WA AL-KUFA.

Alilala usiku ule, na kulipo kucha alimuacha ndugu yake U'thman bin Ziyad kama naibu wake juu ya watu wa Basra, naye akaondoka haraka akielekea (mji wa) al-Kufa. Alipoukaribia mji alitulia hadi jioni, kisha akaingia usiku. Watu wakimdhania kuwa ni Imam Husein (a.s.) walibashiriana kuja kwake na wakaja karibu naye.Walipotambua kuwa ni ibnu Ziyad walitawanyika haraka.
Aliingia kwenye ikulu ya utawala na kulala huko usiku huo.Kisha alitoka asubuhi na kupanda juu ya membar na kuwakhutubia na kuwaonya kutomuasi sultani, na kuwaahidi kuwalipa mema ikiwa watatii.

## MUSLIM IBNI A'QIL AONDOKA KWENYE NYUMBA YA ALMUKHTAR NA KUHAMIA KWA NYUMBA YA HANI.

Muslim ibni A'qil aliposikia habari hizo alihofia juu ya nafsi yake asije akajulikana.Akatoka nyumbani kwake Mukhtar na kuelekea nyumbani kwake Hani ibni U'rwa, akampa makazi, mashia wakawa wakimtembelea huko.

U'baidullah ibni Ziyad alikuwa amewaweka majasusi (ili kufuata harakati zake).Alipojua kwamba yuko nyumbani kwake Hani, alimwita Muhammad ibni Ash-a'th na Asmaa ibni Kharija na A'mru ibni Hajjaj na kuwaambia, "Ni nini kinachomzuia Hani ibni U'rwa kututembelea?"
Wakasema "Hatujui, inasemekana kuwa anashtakia (ugonjwa)."
Akasema "Hilo limeshanifikia, na imenifiki pia kuwa ameshapona, na ya kwamba yeye huketi mlangoni mwa nyumba yake.Lao kama ningejua kuwa anashtakia ugonjwa ningelimtembelea.Basi kutaneni naye na mumuamuru kuwa asiache kutekeleza kilicho wajibu kwake katika haki yetu, kwani mimi sipendi mtu kama yeye kuharibika, kwani yeye ni katika watukufu wa waarabu."

## **HANI AENDA KWA UBEIDULLAH IBNI ZIYAD PAMOJA NA YALIYOJIRI BAINA YAO.**

Wakamjia jioni na kumpata akiwa mlangoni mwake.Wakamwambia, "Ni ni kinachokuzuia kumtembelea amiri.Amekutaja na kusema: Lao kama ningejua kuwa anashtakia ugonjwa ningelimtembelea"
Akasema, "Ugonjwa unanizuia." Wakamwambia "Ameshapata habari kuwa unaketi mlangoni mwako kila jioni, na anaona kuwa unajivuta kumtembelea, na kujivuta na kumpuuza kwa mtu mfano wako hakustahamili sultani, kwani wewe ni seyyidi wa kaumu yako.Tunakusihi sana kuwa upande farasi pamoja nasi twende kwake.
Akaitisha nguo zake akazivaa, akapanda farasi wake wakaondoka. Walipokaribia ikulu akawa ni ni kana kwamba nafsi yake imehisi baadhi ya yaliokuwepo.Akamwambia Hassaan ibni Asmaa ibni Kharija "Yabna akhi, hakika mimi ninaogopa wallahi kutokana na mtu huyu, wewe waonaje?"

Akasema “Wallahi ya a’mmu, sikuogopei chochote, kwa hivyo usiipe nafasi khofu juu ya nafsi yako.” Naye Hassaan alikuwa hajui U’baidullah ibni Ziyad alikuwa amewatuma.kwa lengo gani.
Basi Hani akaja pamoja nao wakaingia wote kwa U’baidullah.
U’baidullah alipomuona Hani akasema, “Imekuletea mukhaini miguu yake mwenyewe.” Kisha akamuelekea Shureih al-Qadhi, ambaye alikuwa ameketi karibu naye na kumuashiria Hani na kuusoma ubeti wa shairi la A’mru ibni Mu’udi Karbu az-Zubeidi:

اريد حياته و يريد قتلي * عذيرك من خليلك من مراد

Ninataka aishi naye anataka kuniuwa
Mletee rafiki yako mtu atoe udhuru wa nia yako.

Hani akamwambia “Na ni nini hicho ewe amiri?”
Akamwambia “Funga mdoma wako, ewe Hani! Ni vitu gani hivi mnavyoficha nyumbani kwako ili kumvizia Amirul muumini pamoja na waislamu? Umemleta Muslim ibni A’qil na kumuingiza nyumbani kwako, na kumkusanyia silaha pamoja na jeshi la watu kwenye nyumba zilizo kando ya nyumba yako ukidhani kuwa mambo haya hatweza kunifikia.”
Hani akamjibu “Sikufanya hivyo.”
Ibnu Ziyad akamwambia “Bali umefanya.”
Akasema “Sikufanya hivyo.Mwenyezi Mungu amfanye amiri kuwa mwema.”
Ibnu Ziyad akasema “Niitieni Ma’aqil mtumwa wangu.”
Ma’aqil alikuwa jasusi wake aliyekuwa akimletea khabari zao, na alikuwa anazijua siri zao nyingi.
Ma’aqil alikuja na kusimama mbele yake U’baidullah.

Hani alipomwona akatambua kuwa alikuwa jasusi juu yake.Akasema “Mwenyezi Mungu amfanye amiri kuwa mwema! Wallahi! Sikumtuma yeyote kwa Muslim wala sikumwita, lakini alinijia akiwa mkimbizi, nikaona haya kumrudisha.Nikaona nimpe ulinzi basi nikampa makazi.Lakini kwa kuwa umeshajua, basi niache nirudi kwake ili nimwamuru kutoka nyumbani kwangu aelekee kokote atakako katika ardhi, ili atoke kwa njia hiyo kwenye ulinzi wake.”

Ibnu Ziyad akamwambia “Wallahi! Sitokuacha kamwe mpaka utakaponijia naye”

Akasema “Wallahi! Sitokujia naye kamwe.Yaani, nikuletee mgeni wangu ili umuuwe?”

Ibnu Ziyad akasema “Wallahi utanijia naye.”

Naye akajibu “Wallahi! Sitokujia naye.”

Maneno yalipozidi kati yao, Muslim ibni A’mru al-Bahili alisimama na kusema “Mwenyezi Mungu amfanye amiri kuwa mwema. Niache nizungumze naye kwa siri”

Akasimama wakaenda naye kando, kwa umbali ambao Ibnu Ziyad alikuwa anaweza kuwaona na kuwasikia.

Mara sauti zao zikapanda.Muslim akamwambia “Ewe Hani, ninakusihi kwa Jina la Mwenyezi Mungu, usiiangamiza nafsi yako na kuwaletea balaa watu wa uko wako.Wallahi, hakika mimi nakuthamini wala singependa uuwawe.Huyu mtu ni binami ya watu hawa, hawawezi kumuuwa wala kumdhuru.Basi mletee huyu mtu, kwani wewe huna aibu au kasoro yoyote kwa kuwa unamleta kwa sultani.”

Hani akasema, “Wallahi! Kwa kufanya hivyo ndio nitakuwa nimepata lawama na aibu.Mimi nimtoe mkimbizi wangu na mgeni wangu na mjumbe wa Ibnu Rasulillah kisha nimkabidhi kwa adui yake, huku nikiwa nina mikono iliyosalama pamoja na watetezi wengi! Wallahi! Lao singekuwa ila mimi peke yangu, bila wa kuninusuru singemkabidhi hata ikiwa nitakufa kwa ajili yake.”

Akawa ni mwenye kumnasihi naye akimjibu “Wallahi simkabidhi”
Ibnu Ziyad akamsikia, akasema, “Mlete karibu nami”Akaletwa karibu naye.Kisha akasema “Wallahi! Utanijia naye, la sivyo nitakikata kichwa chako”
Hani akasema “Basi, wallahi mapanga yatajaa kando ya ikuli yako hii.”
Ibnu Ziyad akasema “Woi huzuni kwako! Unanititisha kwa mapanga?”Huku Hani akidhania kuwa watu wa ukoo wake wanamsikia.
Kisha akasema “Mlete karibu nami.”
Akaupiga uso wake kwa kijiti.Alimpiga pua lake na kipaji chake na shavu lake mpaka akaivunja pua yake na damu kutiririka kwenye nguo yake, na vipandevipande vya nyama ya shavu lake na kipaji chake vikaangukia ndevu zake, hata kile kijiti kikavunjika.
Hani akaupiga mpini wa upanga wa askari kwa mkono wake, lakini yule mtu akauvuta haraka.
Ibnu Ziyad akapaza sauti na kusema “Mchukueni.”Wakamvuta na kumtupa katika chumba mojawapo wa viumba vya ikulu, na kumfungia mlango wake.
Akawaambia “Muwekeeni mlinzi juu yake.” Wakamuwekea mlinzi.
Akasimama Asmaa ibni Kharija - au Hassaan ibni Asmaa kama ilivyotajwa kwingineko- na kumuelekea U’baidullah ibni Ziyad na kusema, “Kwani mchana kutwa tulikuwa ni wajumbe wa khiana? Ewe amiri ulituamuru kukuletea mtu huyu kisha tulipokuletea ukaupondaponda uso wake na kumwaga damu yake hata ikafika kwenye ndevu zake, sasa wadai kuwa utamuuwa?”
Ibnu Ziyad alikasirishwa na maneno yake na kusema “Wewe pia utabaki papa hapa.”

Akaamrishwa akamatwe, kisha akapigwa na mwishowe kuachwa.Kisha akafungwa minyororo na kufungiwa chumba cha pembeni ndani ya ikulu.
Akasema “Inna lillahi wa inna ileihi rajiu’n, ninaitangazia nafsi yangu kifo chako ewe Hani.”

**MADH-HAJ WAIZINGIRA IKULU WAKITAKA HANI AACHWE HURU.**

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: A’mru ibni Hajjaj akapata habari kuwa Hani ameshauwawa.Ruweiha bintu A’mru alikuwa mke wake Hani bin U’rwa.
A’mru akatoka pamoja na watu wote wa kabila la Madh-haj na kuizingira ikulu, na kunadi “Mimi ni A’mru ibni Hajjaj na hawa ni wapanda farasi wa Madh-haj na viongozi wake, hawajaacha utiifu wao wala hawajatoka kwenye jama’ah.Tumepata habari kuwa sahibu wetu Hani amekwisha uwawa.”
U’beidullah akapata habari za kukusanyika kwao na maneno waliyoyasema, akamuamuru Shureih al-Qadhi kuingia alipokuwa Hani amefungiwa ili ashuhudie kuwepo kwake, kisha awajulishe watu hawa kuwa yuko salama hajauwawa.Akafanya hivyo na kuwajulisha, wakaridhishwa na kauli yake, wakaondoka.
Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Habari zikamfikia Muslim ibni A’qil, akatoka pamoja na waliombai ili kupigana vita na U’baidullah ibni Ziyad, akajihami kutokana naye kwa kujifungia ndani ya ikulu ya utawala, wafuasi wake wakapigana na wafuasi wa Muslim.
Wafuasi wa U’baidullah waliokuwa naye ndani ya ikulu wakawa wanajitukuza kuwa naye na kuwatahadharisha wafuasi wa Muslim na kuwatishia kuwa jeshi la Sham linakuja ili kuwasaidia.Waliendelea katika hali hii hadi usiku ukaingia.

Wafuasi wa Muslim wakaanza kutoka mmoja baada mwingine.Baadhi wakawa wanawaambia wenzao, “Tuna haja gani ya kuiharakisha fitna.Yatupasa kukaa majumbani kwetu na kuwaita hawa watu ili Mwenyezi Mungu alete sulhu baina yao.” Wakabaki naye watu kumi tu.
Muslim alipoingia msikitini ili kuswali magharibi wale kumi waliokuwa naye pia wakamuacha peke yake.
Alipoona kuwa ameachwa, aliondoka pweke kwenye vichochoro vya al-Kufa, hadi kufikia kwenye mlango wa mwanamke mmoja aliyeitwa Twao’a, akamuomba maji ya kunywa akamnywesha.Kisha akamuomba ampe makimbilio nyumbani kwake, yule mwanamke akampa makimbili (na kuficha nyumbani kwake).
Mwanawe Twao’a akatambua kuwepo kwake Muslim, akampelekea habari U’baidullah ibni Ziyad.Akamwita Muhammad ibni Ash-a’th na kumtuma pamoja na kikundi ili kumleta Muslim.

## MUSLIM ATOKA KUPIGANA NA JESHI LA UBEIDULLAH IBNI ZIYAD.

Walipofika kwenye nyumba ya yule mwanamke, Muslim aliposikia vishindo vya kwato za farasi, aliivaa deraya yake akampanda farasi wake,na kupigana (kishujaa) na majeshi wa U’baidullah.
Muslim alipowauwa kikundi kikubwa kati yao, Muhammad ibni Ash-a’th alimuita kwa sauti, “Ya Muslim una amani.” Muslim akamwambia “Amani gani? Amani ya kuhadaa na ya ufisadi?”
Kisha akaendelea kupigana nao, huku akisoma beti za sharai la Hamran ibni Malik al-Khath-a’mi aliyoisoma katika siku ya Qarni, kwa kusema;

أقسمت لا اقتل الا حراً *** و إن رأيت الموت شيئاً نكراً
أكره أن أُخدع أو أُغرا *** أو أخلط البارد سخناً مُراُ
كل امرءٍ يوماً يلاقي شراً *** أضربكم و لا أخاف ضُراً

Ninaapa kutouwawa ila nikiwa huru
Hata nikiona mauti kuwa ni chukizo
Nachukia kuhadaiwa au kughuriwa
Au ya baridi kuichanganya kwa ya moto na chungu
Kila mtu siku moja atakutana na shari
Nitawapiga wala siogopi madhara

Wakamwambia “Hauhadaiwi wala haughuriwi.”Lakini yeye hakuwasikiliza.
Lakini wakamghilibu kwa wingi baada ya kuwa amedhoofika kwa majeraha.Mtu mmoja kutoka nyuma yake akamchoma kwa mkuki, akaporomoka kwenye ardhi na kuchukuliwa mateka.

**MUSLIM ASEMEZANA NA UBEIDULLAH IBNI ZIYAD BAADA YA KUSHIKWA MATEKWA.**

Alipoingizwa kwa U’baidullah ibni Ziyad hakumtolea salamu.Mlinzi akamwambia “Mtolee amiri salamu.”
Akamjibu “Nyamaza, kefule! Wallahi yeye si amiri wangu.”
Ibnu Ziyad akasema “Huna ulazima, utoe salamu au usitoe, utauwawa tu.”
Muslim akamwambia “Hata ukiniuwa, ameshauwa aliye shari zaidi yako aliyebora zaidi yangu, na bado hutaacha mauaji mabaya na uovu wa kuiumbua miili ya uliowauwa na kuwa na nia chafu na kutaka ushindi kikhasisi.Hakuna anayestaki hayo ila wewe.”

Ibnu Ziyad akamwambia “Ewe Muasi! Ewe mchochezi! Umemuasi Imamu wako na kuwachochea waislamu, na kuleta fitna kati yao.”
Muslim akamwambia “Umedanganya, ewe Ibnu Ziyad.Aliyewachochea waislamu ni Mu’awiya na mwanawe Yazid.Ama fitna, aliyeileta ni wewe na baba yako, Ziyad ibni U’beid, mtumwa wa bani i’laaj wa mji wa Thaqif.Nami ninatamani kuwa Mwenyezi Mungu ataniruzuku shahada mikononi mwa mshari zaidi ya watu wote.”
Ibnu Ziyad akasema “Umetamani kitu, Mwenyezi Mungu akunyime na asikuone kuwa mwenye kukistahiki, bali akijaalie wenye kukistahiki.”
Muslim akasema “Na ni nani wenye kukistahiki, yabna Marjana?”
Akasema “Wenye kukistahiki ni Yazid na Mu’awiya.”
Muslim akasema “Alhamdu lillah! Tumemridhia Mwenyezi Mungu awe ni mwenye kuhukumu baina yetu na nyinyi.”
Ibnu Ziyad akasema “Unadhani kuwa utapata chochote”
Muslim akasema “Wallahi! Sio dhana, bali ni yakini.”
Ibnu Ziyad akasema “Niambie ewe Muslim, ni kwa nini umekuja katika mji huu, watu wake wakiwa na umoja, ukawagawanya na kuleta mfarakano kati yao.”
Muslim akasema “Sikuja kwa ajili ya hilo, lakini nyinyi mumeyadhirisha maovu na kuyazika mema na mkawatawala watu bila ya wao kuridhia, na kuwafanya watende ambayo Mwenyezi Mungu hajawaamuru nyinyi, na mkawafanyia matendo ya Kisra na Qaisar, basi sisi tukaja ili tuamrishe kati yao mema na tukataze maovu, na kuwaita kwenye hukmu ya Qurani na Sunna.Nasi ndio tunaostahiki jambo hilo kama alivyoamuru Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).”
Ibnu Ziyad (la’anahulla) akaanza kumtukana Muslim na kumtukana Ali na Hasan na Husein (aleihimus salaam).

Muslim akamwambia “Wewe na babako ndio mnaostahiki kutukanwa huko.Basi hukumu unachohukumu, ewe adui wa Mwenyezi Mungu.”

## MUSLIM IBNI A’QIL AFA SHAHIDI.

Ibnu Ziyad akamwamuru Bukeir ibni Hamran kupanda naye juu ya ikulu na kumuuwa.Akapanda naye, huku Muslim anamsabihi Mwenyezi Mungu na kumuomba maghfira na kumswalia Mtume wake (s.a.w.w), akakikata kichwa chake na kushuka huku akiwa ametishika.
Ibnu Ziyad akamwambia “Umepatwa na nini?”
Akasema “Ewe amiri, nimeona wakati wa kumuuwa, mtu mweusi mwenye uso wa kuchukiza, kando yangu akiwa amekiuma kidole chake”Au akasema “ameviuma vidomo vyake.” “Nikapatwa na woga aambao sijawahi kupatwa nao kabla yake.”
Ibnu Ziyad akasema,”Huenda umetishika.”

## HANI IBNI U’RWA AFA SHAHIDI.

Kisha akaamrisha kuwa Hani bin U’rwa aletwe.Akatolewa ili kuuwawa, akawa anasema “Waa madh-hajaah! Nitawatoa wapi (watu wakabila langu la) madh-haj! Waa a’shirataah! Nitawatoa wapi watu wa ukoo wangu!”
Wakamwambia “Ewe Hani, inyoshe shingo yako.”
Akasema “Wallahi! Mimi simkarimu wa kuwatolea kichwa changu, na wala siwasaidii juu ya nafsi yangu.”
Ghulamu wake U’baidullah ibni Ziyad aliyekuwa akiitwa Rashiid, akampiga na kumuuwa.
Kuhusiana na mauaji ya Muslim na Hani, A’bdullah ibni Zubeir al-Asadi anasema, nakwenye upokezi mwingine yasemekana kuwa ni (shairi) la Farazdaq:

**فإن كنتِ لا تدرين ما الموت فانظري* إلى هاني في السوق و ابن عقيل**

إلى بطل قد هشم السيف وجهَه * و آخر يهوى من طمار قتيل

أصابهما جور البغي فأصبحا * أحاديث من يسعي بكل سبيل

ترى جسداً قد غيّر الموت لونه * و نضح دم قد سال كل مسيل

فتىً كان أحيا من فتاة حيّيةً * و أقطع من ذي شفرتين صقيل

أ يركب أسماء الهماليج آمناً * و قد طلبته مذحج بذحولِ

تطوف حفافيه مراد و كلّهم * على رقبة مِن سائل و مسولِ

فإن أنتم لم تثأروا بأخيكم * فكونوا بغايا أَرضيت بقليل

Ikiwa hujui mauti yana nini basi muangalie
Hani huko sokoni na ibnu A’qili
shujaa aliyepasuliwa uso wake na upanga
na mwengine anaanguka toka juu huku kauwawa
wamekumbwa na ujeuri wa dhulma wakawa
mazungumzo ya kila mpita njia
unauona mwili uliobadilishwa rangi yake na mauti
na mtiririko wa damu umepita mpito wa mafuriko
Kijana aliyekuwa na haya zaidi ya binti mwenye haya
na mkali zaidi kuliko upanga ulionolewa ukang’aa
je apande farasi wenye nguvu akitaka usalama
na huku midh-haju wanamtafuta kumlipizia kisasi
wanazunguka kando yake wakimkusudia na wote
wakiwa tayari miongoni mwao kuna muulizaji na muulizwa
Ikiwa nyinyi hamtamlipizia kisasi ndugu yenu
Basi kuweni madhalimu walioridhishwa kwa kitu kidogo

## IMAM HUSEIN (A.S.) AONDOKA MJI WA MAKKA.

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: U’baidullah ibni Ziyad alimuandikia Yazid ibni Mu’awiya akimjulisha habari za Muslim na Hani.Akamrudishia jawabu akimshukuru ndani yake kwa ajili ya kitendo chake na uwezo wake wa kutawala

mambo, na akimjulisha ya kwamba amepata habari ya kwamba Imam Husein (a.s.) ameshaondoka kuelekea upande wake, na akimuamuru kuadhibu na kulipiza kisasi na kumkamata na kumfungia jela yeyote anayedhaniwa wa lao kwa dhana ndogo.

Imam Husein (a.s.) alikuwa ameshatoka Makka akielekea mji wa al-Kufa, siku ya juma nne tarehe tatu ya mwezi wa dhuj hijjah, na katika kauli nyingine yasemekana kuwa ili kuwa tarehe nane ya mwezi wa dhul hijjah mwaka wa sitini hijriya, kabla ya kupata habari kuhusu kuuwawa kwa Muslim, kwani alitoka Makka katika siku ambayo aliuwawa Muslim (ridhwanullahi aleih).

Abu Ja'afar Muhammad ibni Jureir at-Twabari al-Imami amepokea kwenye kitabu chake 'Dala-il Imamah' kwa kusema "Abu Muhammad Sufyan ibni Waki'i ametuhadithia kutoka kwa babake kutoka kwa al-A'amash ya kwamba alisema: Abu Muhammad al-Waqidi na Zurarah ibni Khalaj waliniambia: Tulikutana na Husein ibni Ali (a.s.) kabla ya kutoka kuelekea Iraq kwa siku tatu, tukamjulisha kuhusu udhaifu wa watu huko al-Kufa, na ya kwamba nyoyo zao ziko pamoja naye na panga zao ziko juu yake.

Akanyanyua mikono yake kuilekeza mbinguni, milango ya mbingu ikafunguka, Malaika wakashuka kwa idadi ambayo hakuna awezaye kujua hesabu yake ila Mwenyezi Mungu Azza wa Jalla.

Imam (a.s.) akasema "Lao kama si kukaribiana kwa vitu na kuwadia kwa ajali, ningepigana nao tukiwa na hawa (Malaika), lakini ninajua kwa yakini kuwa hapo ndipo yatakaponifika mauti yangu na mauti ya maswahaba wangu, na hakuna atakayeokoka ila mwanangu Ali."

## KHUTBA YA IMAM HUSEIN (A.S.) ALIPOAZIMIA KUELEKEA MJI WA IRAQ.

Imepokewa pia kuwa Imam (a.s.) alipokuwa ameazimia kuondoka kuelekea Iraq alisimama ili kukhutubia, akasema:

الحمد الله ما شاء الله و لا قوة إلا بالله و صلى الله على رسوله خط المو ت على ولد آدم مخط القلادة على جيد الفتاة و ما أولهني إلى اشتياق أسلافي اشتياق يعقوب إلى يوسف و خير لي مصرع أنا لاقيه، كأني بأوصالي تتقطعها ذئاب الفلوات بين النواويس و كربلاء فيملأن مني أكراشا جوفا و أجربة سغبا لا محيص عن يوم خط بالقلم رضى الله رضانا أهل البيت نصبر على بلائه و يوفينا أجور الصابرين، لن تشذ عن رسول الله (صلّى الله عليه وآله وسلّم) لحمته و هي مجموعة له في حضيرة القدس تقر بهم عينه و ينجز بهم وعده. من كان باذلا فينا مهجته و موطّنا على لقاء الله نفسه فليرحل معنا فإنني راحل مصبحا إن شاء الله تعالى

"Himidi yote ni ya Mwenyezi Mungu, akitakacho Mwenyezi Mungu (ndicho huwa), hakuna nguvu ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu amswalie Mjumbe wake.
Mwanadamu ameandikiwa (na kufungwa kwa) mauti mfano wa mkufu uliofungwa kwenye shingo la mwanamwali.Kilichonitia mapenzi makali ya kukutana na (wazazi wangu na ndugu) waliotangulia ni shauku aliyokuwa nayo Yaaqub kwa (mwanawe) Yusuf (alipopotea).Ni bora kwangu kifo kile kitakachonipata.
Ninaviona sasa hivi machoni mwangu viungo vya mwili wangu vikikatwakatwa na mbwa mwitu wa jangwa lililo baina ya Nawawiisu na Karbala, kisha wananijaza kwenye matumbo na mifuko yenye njaa kali.Hakuna njia ya kuikwepa siku iliyokwisha andikwa kwa kalamu (ya uamuzi

wa Mwenyezi Mungu).Radhi ya Mwenyezi Mungu ndio radhi yetu Ahlul bait, tunaisubiria balaa yake, naye anatulipa malipo ya wasubiriao. Kizazi cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) hakitatenganishwa naye kamwe, bali kitakusanywa kiwe pamoja naye huko Hadhiratul qudsi (peponi), awe ni mwenye kujituliza nao macho yake, na awe ni mwenye kutimiza nao ahadi yake. Yeyote atakayejitolea roho yake kwa ajili yetu, na akawa ameiandaa nafsi yake kukutana na Mwenyezi Mungu, basi na asafiri pamoja nasi, kwani mimi nitaondoka asubuhi Insha-allah."

## MUHAMMAD IBNIL HANAFIYYAH APINGA KUTOKA KWA IMAM HUSEIN (A.S.) KWENDA IRAQ.

Imepokewa kwa isnadi kutoka kwa Muhammad bin Dawuud al-Qummi kwa isnadi kutoka kwa Abu A'bdillah (a.s.) ya kwamba alisema "Muhammad ibnil Hanafiyya alimjia Husein (a.s.) katika usiku aliotaka Husein kutoka Makka asubuhi yake, akamwambia "Ewe ndugu yangu!Hakika watu wa mji wa al-Kufa, unajua vyema khiyana waliyomfanyia baba yako na ndugu yako (I mam Hasan (a.s.)), nami nachelea kwamba yakufike yaliyowafika waliokutangulia, basi ikiwa utaamua kubaki (ni vyema), kwani wewe ndiye uliye azizi zaidi ya walioko katika Haram hii (ya Makkah) na mwenye himaya zaidi."

Imam (a.s.) akasema, "Ewe ndugu yangu! Hakika mimi ninachelea Yazid ibni Mu'awiya asije akaniuwa ndani ya Haram, halafu mimi nikawa ndiyo sababu ya kuvunjwa kwa heshima ya nyumba hii (tukufu)."

Muhammad ibnil Hanafiyya akasema, "Basi ikiwa unachelea hilo, nenda Yemen au sehemu nyingine za nchi, kwani una himaya zaidi ya watu wote huko, na wala hakuna akuwezaye (huko)".

Imam Husein akasema, “Nitaangalia katika uliyoyasema.” Kulipokucha alfajiri mapema, Imam Husein (a.s.) alifungasha akaondoka.Ibnul Hanafiyya akapata habari, akamjia, na kuzishika hatamu za ngamia wake, hali ya kuwa amekwisha mpanda.Akamwambia “Ewe ndugu yangu, je hukuniahidi kwamba utaangalia katika niliyokuomba?”
Imam akasema, “Ndivyo (nilikuahidi).”
Muhammad ibnil Hanafiyyah akasema, “Basi jambo gani limekufanya utoke haraka namna hii?”
Imam akajibu, “Nilipokuacha, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alinijia (kwenye ndoto) akaniambia, “Ewe Husein toka (wende Iraq), kwani Mwenyezi Mungu amekwisha taka kukuona wewe umeuawa.”
Muhammad ibnil Hanafiyya akasema “Inna lillahi wa Inna ileihi raji-‘un (Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na hakika kwake tutarejea), basi nini maana yako kuwachukuwa wanawake hawa pamoja nawe ikiwa wewe unaondoka kukumbana na hali kama hii?”
Akamjibu, “Ameniambia (pia) kwamba: Mwenyezi Mungu amekwisha taka kuwaona wakiwa ni mateka.”
Ibnil Hanafiyya akasalimu amri na kuondoka.
Imam Husein (a.s.) akasafiri hadi kufika (sehemu iliyoitwa) Tan-‘im, akakutana na msafara uliokuwa umebeba zawadi ambayo Buheir ibni Riisaan al-Himyari, mtumishi wa Yazid ibni Mu’awiya huko Yemen aliyokuwa amewatuma nayo kwa Yazid.
Imam (a.s.) akaichukua ile zawadi kwani ndiye mwenye utawala juu ya mambo ya waislamu.
Kisha akawaambia wenye ngamia (kwenye msafara) “Anayependa kuondoka pamoja nasi kwenda Iraq tutamlipa ujira wake na kusuhubiana naye kwa wema, na anayependa kutuacha, tutampa ujira wake kwa kadiri ya masafa aliyokata katikia safari.”
Baadhi wakasafiri naye na wengine wakakataa.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AFIKA DHATU A’RAQ NA KUKUTANA KWAKE NA BISHRU IBNI GHALIB.

Kisha akaendelea Imam (a.s.) na safari yake hadi kufikia mahala paitwapo Dhatu A’raq, akakutana na Bishru ibni Ghalib akiwa anaingia kutoka I’raq, akamuuliza kuhusu hali ya watu wa I’raq.
Akasema, “Nimeziacha nyoyo (zao) zikiwa pamoja nawe na mapanga (yao) yakiwa pamoja na banu Umayya.”
Imam (a.s.) akasema “Amesema kweli ndugu wa bani Asad.Hakika Mwenyezi Mungu hufanya ayatakayo na huamua ayatakayo.”

## IMAM HUSEIN (A.S.) AFIKA THA’ALABIYA NA ALIYOONA KWENYE NDOTO YAKE.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Kisha Imam (a.s.) akaendelea na safari yake hadi kufikia mahala paitwapo Tha’alabiya, wakati wa adhuhuri. Akapumzisha kichwa chake, akalala kisha akaamka na kusema, “Nimemuona mpaza sauti akisema: Nyinyi mnasfiri na mauti yanawasafirisha hadi peponi.”
Ali Akbar (a.s.), mwanawe Imam (a.s.) akamwambia “Ewe baba! Je, kwani hatuko kwenye haki?”
Imam akamjibu “Bila shaka, ewe mwanangu, ninaapa kwa yule ambaye waja wote watarudi kwake.”
Ali Akbar akamwambia “Ewe baba, kwa hivyo basi, hatujali kupatwa na mauti.”
Imam Husein (a.s.) akamwambia “Mwenyezi Mungu akujazi ewe mwanangu, bora zaidi  ya aliyomjazi mwana kwa niaba ya baba yake.”

Imam Husein (.s.) alibaki sehemu hiyo katika usiku huo.Kulipokucha, mara akakutana na mtu katika watu wa al-Kufa aliyekuwa akiitwa Abu Hirra al-Azdi.
Alipofika karibu naye alimsalimu, kisha akamwambia "Yabna Rasulillah, ni kipi kilichokutoa kwenye Haram ya Mwenyezi Mungu na Haram ya Babu yako Rasulullah (s.a.w.w.)?"
Imam Husein (a.s.) akasema "Kefule, ewe Abu Hirra!Bani Umayya walichukua mali yangu, nikasubiri,wakanivunjia heshima yangu, nikasubiri, wakatafuta kumwaga damu yangu nikakimbia.Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba kitaniuwa kikundi cha madhalimu, naye Mwenyezi Mungu atawavisha udhalilifu utakaowaenea wote, na kuwaadhibu kwa upanga mkali, na atatawalisha juu yao atakaye wadhalilisha, hadi wawe dhalili zaidi ya watu wa mji wa Saba' walipotawaliwa na mwanamke akawa ndiye mwenye uamuzi juu ya mali zao na damu zao hadi kuwadhalilisha."

## ZUHEIR IBNIL QAIN AJIUNGA NA KUNDI LA IMAM HUSEIN (A.S.).

Kisha akaendelea Imam Husein (a.s.) na safari yake. Wamehadithia baadhi ya watu kutoka banu Fizara na Bujeila kwa kusema "Tulikuwa naye Zuheir ibnil Qain tulipokuwa tukija kutoka Makka, na tulikuwa tukisafiri karibu naye Husein (a.s.), lakini hakuna kitu kilichokuwa kikituchukiza zaidi kama kusafiri karibu naye, kwa kuwa alikuwa na wanawake wake, na kila alipotaka kutua mahala popote tulilazimika kutengana naye, na kutua sehemu nyingine. Katika siku mojawapo alitua sehemu fulani, tukawa hatuna budi ila kutua pamoja naye sehemu ile.Basi tulipokuwa tukila chakula chetu cha mchana, ghafla mjumbe wake Husein (a.s.) akatujia na kututolea salamu.Kisha akasema

“Ewe Zuheir ibnil Qain, Abu ‘Abdillah (a.s.) amenituma kwako kukujulisha kwamba uje kwake.”
Kila mmoja kati yetu akatupa kilichokuwa mkononi mwake, tukawa kana kwamba kuna ndege juu ya vichwa vyetu.
Mke wake Zuheir, ambaye alikuwa akiitwa Dailam bintu A’mru, akamwambia, “Sub-hanallah! Mwana wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anakutumania, kisha unakosa kwenda, laiti ungekwenda na kusikiliza maneno yake.”
Basi Zuheir akaondoka na kumfwata Imam (a.s.) .Haukupita muda mrefu akarudi akiwa mwenye furaha na uso wake ukiwa umenawiri, akaamrisha hema yake kubomolewa na mizigo yake kuwekwa pamoja na mizigo ya Husein (a.s.).Kisha akamwambia mkewe “Anti twaliq (nimekutaliki) kwani mimi singependa yakupate ila mazuri.Nimesha amua kufwatana na Imam Husein (a.s.) ili nimfidie roho yangu na kumhami kwa nafsi yangu.” Kisha akampa mali yake na kumkabidhi mkewe kwa baadhi ya binami zake ili wamfikishe kwa jamaa zake.
Mkewe akasimama na kumuaga huku akilia na kusema “Khaarallahu laka (Mwenyezi Mungu akujaalie kheri. Nakuomba unikumbuke siku ya Qiyama mbele ya Babu yake Imam Husein (a.s.).”
Kisha akawaambia maswahaba wake “Anayependa kufwatana nami na aje, la sivyo, basi huu ndio wakati wa mwisho wa kuonana naye.”

## IMAM HUSEIN (A.S.) AFIKA ZUBALA, NA KUPASHWA HABARI ZA KUUWAWA KWA MUSLIM.

Kisha Imam Husein (a.s.) akaendelea na safari yake hadi kufika mahala paitwapo Zubala, ikamfikia huko khabari ya kuuwawa kwa Muslim ibni A’qil.Miongoni mwa waliofwatana naye wakajua khabari hizo, wenye tama na

wenye shaka wakamuacha, akabaki na jamaa zake na maswahaba wake walio waaminifu.
Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Sehemi ile ikalipukwa kwa kilio na maombolezi kwa kuuwawa kwa Muslim bin A’qil, na machozi yakatirika kwa wingi kwa majonzi ya kumpoteza.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AKUTANA NA FARAZDAQ.

Kisha Imam Husein (a.s.) aliendelea na safari yake akiyakusudia aliyoitiwa na Mwenyezi Mungu kuyatekeleza. Farazdaq akakutana naye na kumsalimu na kusema “Yabna Rasulillah utawezaje kuwategemea watu wa al-Kufa, na hali ya kuwa wao ndio waliomuuwa binami yako, Muslim bin A’qil na wafuasi wake?”
Mpokezi wa habari hizi anasema: Imam Husein (a.s.) alipatwa na huzuni na kulia, kisha akasema “Mwenyezi Mungu amrehemu Muslim, amekwishafika kwenye pepo ya Mwenyezi Mungu, kwenye raha na raihani na salamu na radhi ya Mwenyezi Mungu.Ama kwa kweli, yeye amekwisha tekekeleza jukumu lake na (sasa) limebaki jukumu letu.”Kisha akasema beti hizi:

فإن تكن الدنيا تعدّ نفيسة فإنّ ثواب الله أعلى و أنبلُ
و إن تكن الأبدان للموت أنشئت فقتل امرئ بالسيف في الله أفضلُ
و إن تكن الأرزاق قسما مقدّراً فقلّة حرص المرء في السعي أجملُ
و إن تكن الأموال للترك جمعُها فما بال متروك به المرء يبخلُ

Ikiwa dunia inachukuliwa kuwa ni ya thamani
basi thawabu ya Mwenyezi Mungu ni bora na ya sharafa zaidi
Na ikiwa miili iliumbwa kwa ajili ya mauti

basi mtu kuuwawa kwa upanga kwa njia ya Mwenyezi
Mungu ni bora zaidi
Na ikiwa riziki zina kipimo kilichokadiriwa
basi mtu kupunguza tamaa katika kutafuta kunapendeza zaidi
Na ikiwa mali zinakusanywa kwa ajili ya kuachwa
basi kwa nini chenye kuachwa, mtu akifanyie ubakhili.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AWAANDIKIA MASWAHABA WAKE BARUA WALIOKO MJI WA AL-KUFA NA YALIYOMFIKIA MTUME WAKE.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Imam Husein (a.s.) alimuandikia barua Suleiman ibni Sward na Musayyib ibni Najba na Rufa'a ibni Shaddad na baadhi ya mashia wa al-Kufa, na kumkabidhi Qais ibni Mus-har as-Swaidawi ili kuwapelekea.
Qais alipokaribia mji wa al-Kufa akakumbana na Haswin ibni Numeir, swahibu wake U'baidullah ibni Ziyad, akamzuia kuinga al-Kufa ili amfanyie upekuzi.
Qais akaitoa ile barua ya Imam Husein (a.s.) na kuichana.Haswin akamchukua na kumpeleka kwa Ibnu Ziyad.
Alipoletwa mbele yake akamwambia "Ni nani wewe?"
Akasema "Mimi ni mmoja katika mashia wa Amirul Muuminin (a.s.) Ali ibni abi Twalib na wa mwanawe (aleihimas salaam)."
Akamwambia "Basi ni kwa nini umeichana barua?"
Akajibu "Ili usijue kilichoandikwa ndani yake."
Akamwambia "Barua imetoka wapi na ni ya nani?"
Akajibu "Ameituma Husein ibni Ali (a.s.) kwa baadhi ya watu wa al-Kufa, siwajui majina yao."
Ibnu Ziyad akakasirika na kusema "Wallahi sikuachi hadi utakaponijulishe majina ya hawa watu, au upande kwenye

membar umlaani Husein na baba yake na ndugu yake, la sivyo nitakukatakata vipandevipande."
Akapanda kwenye menbar, akamhimidi Mwenyezi Mungu, akamtukuza na kumswalia Mtume (s.a.w.w.) na kumuombea rehma kwa wingi Imam Ali na kizazi chake (swalawatullahi aleihim), kisha akamlaani U'baidullah ibni Ziyad pamoja na baba yake na kumlaani madhalimu wa banu Umayya, toka mwanzo wao hadi wa mwisho.
Kisha akasema "Enyi watu, mimi ni mjumbe wa Husein ibni Ali (aleihimas salaam) kwenu, na nimemuacha sehemu fulani.Basi mjibuni."
U'baidullah ibni Ziyad akajulishwa aliyoyasema, akaamrisha kuwa aporomoshwe toka juu ya paa ya ikulu.Akatupwa kutoka huko akafariki (rahimahullah).
Imam Husein (a.s.) akafikiwa na habari za kufa kwake, akahuzunika sana na kulia, kisha akasema "Ewe Allah! Tujaalie sisi na mashia wetu mahala patukufu na utukutanishe pamoja nao katika makao ya rehma yako, hakika wewe ni mweza wa kila kitu."
Imepokewa kuwa Imam Husein (a.s.) aliandika hii barua akiwa katika mji wa Hajiz, na wengine wamesema kinyume chake.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AKUTANA NA HURR NA YALIJIRI BAINA YAO.

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Imam Husein (a.s.) aliendelea na safari hadi kufika umbali wa vituo viwili toka al-Kufa, mara akatokea Hurr ibni Yazid akiwa na wapanda farasi elfu.
Imam Husein (a.s.) akamwambia "Mmekuja kwa faida yetu au dhidi yetu?"
Akamjibu "Bali dhidi yenu, ya Aba A'bdillah!"

Imam akasema “La haula wa la quwwata illa billahil a’liyyil a’dhim (hakuna uwezo wala nguvu ila kwa kuwezeshwa na Mwenyezi Mungu aliyetukuka aliye adhimu.)”
Kisha wakajibizana maneno hadi Imam Husein (a.s.) kufikia kumwambia “Basi ikiwa mko kinyume cha yaliyonijia katika barua zenu na waliyokujia nayo wajumbe wenu, niacheni nirudi mahala nilipotoka.”
Lakini Hurr na maswahaba wake wakamzuia kurudi, bali akamwambia “La, yabna Rasulillah, bali ifwate njia ambayo haitakuingiza mji wa al-Kufa wala kukufikisha mji wa Madina, ili niwe nina udhuru wa kumtolea Ibnu Ziyad, nimwambie kuwa tulipishana nawe katika njia ukawa umepita njia nyingine.”
Basi Imam Husein (a.s.) akachukua njia ya kushoto hadi kufika sehemu iitwayo A’dhiibul Hijanat.
Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Barua kutoka kwa U’baidullah ibni Ziyad ikamfikia Hurr huku akimlaumu kuhusiana na aliyomfanyia Imam Husein (a.s.) na akimuamuru kumbana.
Hurr na maswahaba wake wakamfwata na kumzuia kuendelea na safari yake.
Imam Husein (a.s.) akamwambia “Je, hukuniamuru kufwata njia nyingine?”
Hurr akasema “Ndiyo, nimekuamuru, lakini barua ya amiri U’baidullah ibni Ziyad imenijia akiniamuru ndani yake kuwa nikubane, na ameniwekea jasusi anayenilazimisha kukubana.”

## KHUTBA YA IMAM HUSEIN (A.S.) HURR ALIPOWAFUNGIA NJIA.

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Imam Husein (a.s.) akasimama na kuwakhutubia maswahaba wake.Akamhimidi

Mwenyezi Mungu na kumtukuza, kisha akamtaja Babu yake na kumswalia, kisha akasema:

إنه قد نزل بنا من الأمر ما قد ترون، و إن الدنيا قد تنكّرت و تغيّرت و أدبر معروفها و استمرت جذّاء، و لم تبق منها إلا صبابة كصبابة الإناء، و خسيس عيش كالمرعى الوبيل، أ لا ترون إلى الحق لا يُعمل به، و إلى الباطل لا يتناهى عنه، ليرغب المؤمن في لقاء ربّه محقاًّ، فإنّي لا أرى الموتَ إلاّ سعادةً و الحياةَ مع الظالمين إلاّ برماً

“Hakika yameshatufikia mambo mnayoyaona, nayo dunia imeshaonyesha chuki na kubadilika na mema yake kutuelekezea mgongo wake na kuendelea kuwa ni yenye kukatika,na hakukubakia katika mema yake ila masazo mfano wa masazo yanayosalia kwenye chombo, na maisha duni mfano wa malisho yasiyofaa, je hamuoni kwamba haki haitekelezwi na uovu haukemewi ili muumini awe na raghba ya kukutana na Mola wake akiwa ndiye mwenye haki.Hakika mimi sioni kifo (katika njia ya haki) si kitu ila sa’ada na kuishi pamoja na madhalimu si kitu ila unyonge."

## **ALIYOYASEMA ZUHEIR IBNIL QAIN BAADA YA KHUTBA YA IMAM (A.S.).**

Zuheir ibnil Qain akasimama na kusema “Tumesikia kauli yako, hadanallah bika (Mwenyezi Mungu atuongoze kupitia kwako) yabna Rasulillah.Lao kama dunia ingekuwa ni yenye kudumu kwa ajili yetu nasi tukawa wenye kuishi milele ndani yake, tungelipendekeza kujitoa muhanga pamoja nawe badala ya kuishi milele ndani yake.”

## ALIYOYASEMA HILAL IBNI NAFI'I ALBAJALI, NA ALIYOYASEMA BUREIR.

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Hilal ibni Nafi'i al-bijli alisimama haraka na kusema "Wallahi! Hatuchukii kukutana na Mola wetu.Hakika sisi tumesimama katika nia zetu na basira zetu, tunampenda anayekupenda na kumfanyia uadui anayekufanyia uadui."
Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Naye Bureir ibni Haswin alisimama na kusema "Wallahi yabna Rasulillah! Mwenyezi Mungu ametuneemesha kupitia kwako kwa kutujaalia kuwa tupigane mbele yako na viungo vyetu vikatakatwe kwa ajili yako, kisha Babu yako awe ndiye Muombezi wetu siku ya Qiyama."

## IMAM HUSEIN (A.S.) AFIKA KARBALA NA KUSOMA BETI ZA MASHAIRI ZINAZOASHIRIA KUHUSU KUFA KWAKE SHAHIDI.

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Kisha Husein (a.s.) alisimama na kupanda farasi na kuendelea na safari, lakini walikuwa wakimzuia wakati mwingine na wakati mwingine wakisafiri karibu naye hadi akafika Karbala katika siku ya pili ya mwezi wa muharram(Yaani mfungo nne).
Alipofika huko akauliza "Ardhi hii inaitwaje?"
Akaambiwa "Karbala."
Akasema "Shukeni.Hapa wallahi ndipo kituo cha msafara wetu, na ndipo mahali ambapo damu zetu zitamwagika, na hapa wallahi ndipo sehemu yatakayokuwa makaburi yetu, na hapa wallahi ndipo watafanywa mateka mahaarimu wetu.Babu yangu alinihadithia haya."
Wakashuka wote, naye Hurr akashuka na maswahaba wake pembeni.

Imam Husein (a.s.) akaketi akiutengeza upanga wake huku akisema:

يا دهر أُفٍّ لك من خليلِ * كم لك بالإشراق و الأصيلِ
من طالب و صاحب قتيل * و الدهر لا يقنع بالبديل
و إنما الأمر إلى الجليل * و كل حيٍّ فإلى سبيلِ
ما أقرب الوعد من الرحيل * إلى جنان و إلى مقيل

Kefule ewe zama kwa urafiki wako
ni wangapi asubuhi na jioni
wakutafutao na maswahibu wako waliouwawa
wala zama hazikinaishwi na badili
bali mambo uamuzi wake ni kwa Jalali
na kila aliyehai ni msafiri
Ni ukuruba ulioje wa ahadi ya kuondoka
kuelekea peponi na mapumzikoni

## ALICHOKIFANYA ZAINAB (A.S.) BAADA YA KUZISIKIA BETI.

Mpokezi wahabari hizi anasema: Bibi Zainab bintu Fatima (aleihimas salaam) akayasikia maneno hayo, akasema "Ewe ndugu yangu, haya ni maneno ya mtu ambaye ameshapata yakini ya kwamba atauwawa."
Akamjibu "Na'am ewe dadangu!"
Bibi Zainab akasema "Waa thaklaah! (Woi nimefelewa!) Husein ananiombolezea kifo chake mwenyewe!"
Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Wanawake wakalia na kupiga shavu zao na kupasua nguo zao.
Naye Ummu Kulthum akawa ni mwenye kunadi kwa kusema, "Woi Muhammad! Woi Ali wangu! Woi mama!

Woi Hasan! Woi Husein! Woi maangamio baada yako, ya Aba A'bdillah!"
Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Imam Husein (a.s.) alimtuliza na kumwambia "Ewe dadangu tulia ujifariji kwa faraja ya Mwenyezi Mungu, kwani wakazi wa mbinguni wana kufa na watu wa ardhini hawabaki milele, na viumbe wote wataangamia."
Kisha akasema "Ewe dadangu! Ewe ummu Kulthum! Nawe, ewe Zainab! Nawe ewe Ruqaiyya! Nawe ewe Fatima! Nawe ewe Rubab! Angalieni, mimi nitakapo uwawa msizipasue nguo, wala kuzikwaruza nyuso kwa kuniomboleza, wala msiseme maneno machafu kwa ajili yangu."
Imepokewa kwa upokezi mwingine ya kwamba Zainab aliposikia beti hizi, huku akiwa mbali kidogo na Imam (a.s.) pamoja na wanawake na mabanati, alitoka akiwa mwenye huzuni na huku akikokota nguo zake, hadi kusimama mbele yake na kusema, "Waa thaklaah! (Woi tumefelewa!) Laiti mauti yangeniondolea uhai! Leo hii amekufa Mama yangu Fatima az-Zahra, na Baba yangu A'li al-Murtadha, na Ndugu yangu Hasan az-Zaki, ewe uliyebaki baada ya waliotutangulia, na nguzo ya tuliobaki."
Imam Husein (a.s.) akamwangalia na kusema "Ewe dadangu usiondokwe kamwe na utulivu wako."
Akamwambia, "Baba yangu na mama yangu wawe fidia kwako! Je, kweli utauwawa? Nafsi yangu iwe fidia kwako."
Imam Husein (a.s.) akawa anajaribu kuzuia huzuni yake kubwa, lakini machozi yakawa yanamlengalenga, kisha akasema, "Haiwezekani, haiwezekani kamwe! Lao kama qatwa (ambaye ni kuku wa porini) ataachwa usiku atalala."
Bibi Zainab (a.s.) akasema "Ya wailata! (Ole wangu!) Je, (ni kweli) utatolewa nafsi yako kimabavu? Basi, hilo ndilo lenye kuumiza moyo wangu zaidi na lililo zito zaidi kwa nafsi yangu." Kisha akazishika nguo zake na kuzipasua na kuanguka akiwa amepotewa na fahamu.

Imam (a.s.) akasimama na kumwagilia maji usoni, akarudiwa na fahamu zake.Akawa anamtuliza na kumpa subira, na kumkumbusha msiba wa kifo cha Baba yake Imam Ali na Babu yake Mtukufu Mtume (swalawatullahi aleihim ajma'in).

## SABABU AMBAZO HUENDA ZILIMFANYA IMAM HUSEIN (A.S.) KUWABEBA WATU WAKE WA NYUMBANI PAMOJA NAYE.

Na miongoni mwa mambo ambayo huenda yakawa ndiyo sababu ya Imam Husein (a.s.) kuwabeba mahaarimu, wanawake na watoto ni kwa kuwa lao kama angewaacha huko Hijaz au sehemu nyingine, Yazid ibni Mu'awiya (la'anahullah) angewatumia mtu awachukue kwa nguvu na kuwaleta kwake na kuwafanyia mabaya ambayo yangelimzuia Imam Husein (a.s.) kupigana jihadi na kufa shahidi na kupata sa'ada.

# MLANGO WA PILI.

# YALIYOJIRI KATIKA UWANJA WA MAPIGANO NA KABLA YA MAPIGANO.

## YALIYOJIRI KATIKA UWANJA WA MAPIGANO NA KABLA YA MAPIGANO.

Mpokezi wa habari hizi anasema: U'baidullah bin Ziyad aliwatuma wafuasi wake waende kupigana vita na Imam Husein (a.s.) wakamfwata, akawa amewadhoofisha watu wake wakamtii.
Akanunua kutoka kwa U'mar bin Sa'ad akhera yake kwa dunia yake, kwa kumpa uongozi wa vita, naye akakubali. Akatoka kupigana na Imam Husein (a.s.) na wapanda farasi elfu nne, naye Ibnu Ziyad akawa anamtumia majeshi ya askari katika vipindi tofauti tofauti, hata wakatimia majeshi elfu ishirini katika usiku wa tano kabla ya mwezi wa Muharram (mfungo nne) kuingia.Wakamuwekea Imam Husein (a.s.) vikwazo kiasi cha kumfanya kupatwa na kiu yeye na wafuasi wake.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AWAHUTUBIA MAADUI NA KUTIMIZA HOJA JUU YAO.

Imam (a.s.) akasimama huku ameuegemea mpini wa upanga wake na kupaza sauti akisema, "Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je nyinyi mnanijua mimi?"
Wakajibu, "Bila shaka tunakujua, wewe ni Ibnu Rasulillah na Mjukuu wake."
Imam akasema, "Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je mnajua kwamba Babu yangu ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)?"
Wakajibu, "Bila shaka tunajua."
Akawaambia tena, "Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je mnjua kwamba Mama yangu ni Fatima bintu Muhammad?"
Wakajibu, "Bila shaka tunajua."

Akawaambia tena, “Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je mnjua kwamba Baba yangu ni Ali ibni Abi Twalib?”
Wakajibu, “Bila shaka tunajua.”
Imam akasema, “Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je munajua kwamba Nyanya yangu Khadija Bintu Khuwailid, ndiye mwanamke wa kwanza kusilimu katika umma huu?”
Wakajibu, “Bila shaka tunajua.”
Akawaambia tena, “Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je mnajua ya kwamba Hamza ambaye ni Seyyidush Shuhada ni Ami yangu?”
Wakajibu, “Hilo pia bila shaka tunalijua.”
Akawaambia tena, “Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je mnajua ya kwamba Jaafar at-Tayaar aliyeko Peponi ni Ami yangu?”
Wakajibu, “Hilo pia bila shaka tunalijua.”
Imam (a.s.) akawaambia, “Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je mnajua ya kwamba upanga huu nilioufunga kiunoni ni upanga wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?”
Wakajibu, “Hilo pia bila shaka tunalijua.”
Akasema tena, “Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je mnajua kuwa kilemba hiki nilichokivaa ni cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?”
Wakajibu, “Hilo pia bila shaka tunalijua.”
Imam (a.s.) akawaambia, “Nakuapieni Mwenyezi Mungu, je mnajua kwamba Ali ibni Abi Talib ndiye aliyekuwa muislamu wa kwanza na ndiye aliyekuwa mjuzi kuliko wengine (baada ya Mtume s.a.w.w.) naye ndiye aliyekuwa mpole kuliko wote, na ya kwamba yeye ndiye Walii wa kila muumini mwanamume na mwanamke?”
Wakasema, “Bila shaka tunajua.”
Kisha Imam Husein (a.s.) akawaambia, “Basi ni kwa nini mnahalalisha damu yangu wakati ambapo Baba yangu ndiye mlinzi wa Hodhi (ya Kauthar) hapo kesho, atawazuia baadhi ya watu kuyanywa (maji yake) kama anavyozuiwa ngamia

anayejaribu kuyanywa maji, na Bendera Tukufu ya Mtume itakuwa mikononi mwake siku ya Qiyama?”
Kisha wakamwambia Imam (a.s.) “Yote hayo uliyoyasema sisi tunayajua vyema, lakini hatutakuacha mpaka uyaonje mauti hali ya kuwa una kiu.”
Alipotoa khutba hii, mabanati zake na dada yake Zainab waliposikia maneno yake walianza kulia na kuomboleza kwa sauti za juu, huku wakijipiga nyuso zao.
Imam (a.s.) akawatuma kwao ndugu yake A’bbas na mwanawe Ali akiwaambia “Wanyamazisheni.Naapa kwa uhai wangu, kwamba watazidi kulia.”

## JIBU LA ABBAS (A.S.) NA NDUGU ZAKE SHIMRI ALIPOWAPA AMANI.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Barua kutoka kwake U’baidullah ikamfikia U’mar ibni Sa’ad akimisisitizia kuanza mapigano na kuyaharakisha mapambano na kumtahadharisha kutokana na kuchelewesha.Wakatoka wakimuelekea Imam Husein (a.s.).
Shimr ibni Dhil Jaushan (La’anahullah) akakaribia na kupaza sauti akisema “Wako wapi wana wa dadangu, A’bdullah na Ja’afar na A’bbas na U’thman?”
Imam Husein (a.s.) akasema “Mjibuni hata kama ni fasiki, kwani ni katika wajomba wenu.”
Wakamjibu “Unataka nini?”
Akasema “Enyi wana wa dada yangu, ninawapeni amani, kwa hivyo msiziuwe nafsi zenu pamoja na ndugu yenu Husein, bali fanyeni utiifu kwa amirul muuminin Yazid ibni Mu’awiya “
A’bbas ibni Ali akapaza sauti na kumjibu “Mikono yako iangamie na amani yako uliyotuletea ilaaniwe, ewe adui wa Mwenyezi Mungu.Unatuamuru tumuache ndugu yetu na

Bwana wetu Husein ibni Fatima na kuingia kwenye utiifu wa maluuni na wana wa maluuni?”
Shimri akarudi kwenye jeshi lake akiwa amekasirika.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AWAOMBA MAADUI MUHULA USIKU HUO ILI KUJISHUGHULISHA NA IBADA.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Imam Husein (a.s.) alipoona pupa yao ya kuharakisha kuanza mapigano na uchache wa kunufaika kwao na waadhi na nasiha, akamwambia ndugu yake A’bbas, “Ikiwa utaweza kuwazui kupigana nasi kwa leo basi wazuie, ili huenda tukaswali kumuabudu Mola wetu usiku wa leo, kwani Yeye yuajua kwamba mimi ninapenda swala na kusoma Kitabu chake (Kitukufu).”
Mpokezi wa habari hizi anasema: A’bbas akawaomba wawape muhula huo lakini U’mar ibni Sa’ad akasita, U’mar ibni Hajjaj az-Zubeidi akamwambia, “Wallahi! Lao kama walikuwa watu watokao Uturuki au Dailam wakatuomba muhula tungewapa, basi kwa nini tusiwajibu hawa na hali ya kuwa wao ni Aali zake Mtume Muhammad.”
Basi wakawapa muhula huo wa kufanya ibada.

## IMAM HUSEIN AOTA NDOTO.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Imam Husein (a.s.) aliketi akapatwa na kusinzia kidogo, kisha akaamka na kusema “Ewe dada yangu! Nimemuona sasa hivi Babu yangu, Muammad (s.a.w.w.) na Baba yangu, Ali na mama yangu Fatima na Ndugu yangu Hasan huku wakiniambia: Ewe Husein! Hakika wewe utakuja kwetu hivi karibuni.”
Katika mapokezi mengine impokewa kuwa alisema, “hakika wewe utakuja kwetu kesho.”

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Bibi Zainab (a.s.) akapiga uso wake na kupaza sauti kwa kulia.
Imam Husein (a.s.) akamwambia “Tulia, usije ukawafanya maadui kufurahia msiba wetu.”

## IMAM (A.S.) AWAKHUTUBIA MASWAHABA WAKE NA KUWARUHUSU KUONDOKA.

Usiku ulipoingia Imam Husein (a.s.) aliwakusanya maswahaba wake, akamhimidi Mwenyezi Mungu na kumtukuza kisha akawakaribia na kusema:

أما بعد، فإني لا أعلم أصحاباً خيراً منكم و لا أهل بيت أفضل و أبرّ من أهل بيتي فجزاكم الله عنّي جميعاً خيراً، و هذا الليل قد غشيكم فاتخذوه جملاً، و ليأخذ كل رجلٍ منكم بيد رجلٍ من أهل بيتي، و تفرّقوا في سواد هذا الليل و ذروني و هؤلاء القوم فإنهم لا يريدون غيري

“Ama ba’adu, hakika mimi siwajui maswahaba bora zaidi yenu, wala ahlu baiti
walio bora na wema zaidi kuliko Ahlu baiti wangu, Mwenyezi Mungu awajazi kheri nyote kwa niaba yangu.Huu ni usiku na giza lake limewaficha, basi ondokeni kwenye giza hili, na kila mtu kati yenu na aushike mkono wa mmoja katika Ahlu baiti wangu kisha mtawanyike katika giza la usiku huu, mniache peke yangu pamoja na hawa watu kwani hawamtaki yeyote ila mimi.”

## WALIYOSEMA NDUGU ZAKE NA WATU WAKE WA KARIBU.

Ndugu zake na wanawe na wana wa A’bdullah ibni Ja’afar wakamwambia “Kwa nini tufanye hivyo? Ili tuishi baada

yako?! Laa! Mwenyezi Mungu asituonyeshe siku hiyo kamwe."
Aliyeanza maneno haya alikuwa A'bbas ibni A'li, kisha wengine wakamfwata.
Mpokezi wa habari hizi anasema: Kisha akawaangalia wana wa A'qil na kuwaambia "Inatosha kutoka kwenu kuuliwa kwa ndugu yenu Muslim.Nendeni nimewapa ruhusa."
Imepokewa kwa mapokezi mengine ya kwamba, wakati huo walizungumza ndugu zake na ahlu baiti zake wote na kusema "Yabna Rasulillah! Basi watu watatuambia nini, nasi tutawaambia nini, tukiwa tumemwacha Mzee wetu na Mkubwa wetu na Bwana wetu na Imamu wetu na Mwana wa Binti ya Mtume wetu, bila ya kutupa pamoja naye hata mshale wala mkuki wala kupiga pamoja naye upanga? Laa wallahi yabna Rasulillah! Hatukuachi kamwe, bali tutakuhami kwa nafsi zetu hadi kuuwawa mbele yako na kuingia utakapoingia, Mwenyezi Mungu ayachukize maisha baada yako."
Kisha Muslim ibni A'usaja akasimama na kusema "Sisi tukuache hivi tuondoke na huku umezingirwa na huyu adui? Laa wallahi! Mwenyezi asinione kamwe nikifanya kitu kama hicho hadi niwe nimeuvunja mkuki wangu kwenye vifua vyao na kuwapiga kwa upanga wangu muda wote mpini wake utakaobaki mkononi mwangu, na lao kama sitakuwa na silaha ya kupigana nao nitawapiga kwa mawe, wala sitokuacha kamwe hadi kufa kwa ajili yako."

## ALIYOYASEMA SA'ID IBNI ABDILLAH ALHANAFI NA ZUHEIR IBNIL QAIN NA BAADHI YA MASWAHABA.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Naye Sa'id ibni A'bdullah al-Hanafi akasimama na kusema "Yabna Rasulillah! Hatukuachi kamwe mpaka Mwenyezi Mungu ajue kwamba

kwa kukuhami tumeuhifadhi wasia wa Mjumbe wake, Muhammad (s.a.w.w.).Lao kama nitajua kwamba nitauwawa kwa ajili yako kisha nifufuliwe kisha nichomwe kwa moto, kisha majivu yangu yapeperushwe, nifanyiwe hivi mara sabini, sitokuacha kamwe hadi nikutane na kifo changu katika kukuhami.Vipi basi, na hali ya kuwa ni kuuwawa mara moja, kisha nipate karama ambayo haina mwisho kamwe?"

Kisha Zuheir ibnil Qain akasimama na kusema "Wallahi yabna Rasulillah! Ningependa kuwa niuwawe na kufufuliwa mara elfu, na kwa kuuwawa huku Mwenyezi Mungu akuepushie kifo wewe na hawa vijana katika ndugu zako na wanao na Ahlu baiti zako."

Mpokezi wa habari hizi anasema: Kisha wakazungumza wengineo katika maswahaba wake mfano wa maneno hayo kwa kusema "Nafsi zetu ni fidia kwako, tutakulinda kwa mikono yetu na nyuso zetu, sisi tukifa mbele yako tutakuwa tumetekeleza ahadi tuliomtolea Mola wetu, na kutimiza yaliyo wajibu juu yetu."

## ALIYOYASEMA MUHAMMAD IBNI BASHIR ALIJULISHWA KUWA MWANAWE AMESHIKWA MATEKA.

Muhammad ibni Bashir al-Hadhrami akiwa katika hali hii aliambiwa "Mwanao amechukuliwa mateka katika maingilia ya mji wa Rei."

Akasema "Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu nimemtoa pamoja na nafsi yangu, hata hivyo sikupenda kuwa achukuliwe mateka nami nibaki hai baada yake."

Imam Husein (a.s.) akasikia kauli yake, akamwambia "Rahimakallah (Mwenyezi Mungu akurehemu). Wewe unaruhusa ya kutonibai, nenda ukashughulikie kumfanya huru mwanao."

Muhammad ibni Bashir al-Hadhrami akamwambia, “Ikiwa nitakuacha, basi na niliwe na wanyama wakali nikiwa hai.” Imam (a.s.) akamwambia “Basi mpe mwanao mavazi haya, ayatumia kumfanya huru ndugu yake.”Akampa nguo tano zenye thamani ya dinari elfu moja.
Mpokezi wa habari hizi anasema: Imam Husein (a.s) alikesha usiku huo pamoja na maswahaba wake, na sauti zao zilichanganyika na kusikika kama mvumo wa nyuki wengi, baadhi wakiwa katika hali ya rukuu, na wengine katika hali ya kusujudu, na wengine katika hali ya qiyam, na wengine wakiwa katika hali ya kuketi.Wakahama katika usiku huo askari jeshi thalathini na wawili kutoka kwenye jeshi la ibni Sa’ad na kujiunga na jeshi la Imam Husein (a.s.).

## BUREIR AMFANYIA UTANI ABDUR RAHMAN ASUBUHI YA SIKU YA ASHURA.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Kulipokucha Imam Husein (a.s.) aliamuru hema yake kusimamishwa, ikasimamishwa .Kisha akaitisha bakuli ambayo ilikuwa na miski nyingi ndani yake na kuichanganya na dawa ya kuondolea nyele, akaingia ndani ya hema ili kujipaka (kwenye viungo ili kuziondoa nyele za ziada).
Bureir ibni Haswin al-Hamdani na A’bdur Rahman ibni A’bdi Rabbihi al-Answari walisimama kwenye mlango wa hema ili kujipaka dawa ya kuondolea nyele baada ya Imam (a.s.). Bureir akawa anamchekesha A’bdur Rahman (kwa kumtania).
A’bdur Rahman akamwambia “Ewe Bureir, unacheka! Huu sio wakati wa kucheka na kufanya mambo ya ubatilifu.” Bureir akamwambia “Watu wangu wanajua kwamba mimi sijawahi kupenda mambo ya ubatilifu katika uzeeni wala katika ujana, bali ninafanya hivi kwa kufurahia kile tutakachokifikia.Wallahi hakuna jambo tunalofanya ila tu ni

kukutana na hawa watu kwa mapanga yetu, tukakabiliana nao kwa mapanga kwa muda mfupi, kisha baada yake, kwa kufariki tukakumbatiana na Hurul a'in."
Mpokezi wa habari hizi anasema: Wafuasi wa U'mar ibni Sa'ad walipanda farasi wao (ili kuanza mapigano), Imam Husein (a.s.) akamtuma Bureir ibni Haswin, akawatolea waadhi lakini hawakumsikiza, akawanasihi lakini hawakunufaika.

## KHUTBA YA IMAM HUSEIN (A.S.) MBELE YA JESHI LA IBNU SA'AD AKIWANASIHI NA KUWAKUMBUSHA BARUA ZAO WALIZOMTUMIA.

Basi Imam Husein (a.s.) akampanda ngamia wake- au farasi wake kwenye mapokezi mengine- akawanyamazisha wakanyamaza, kisha akamhimidi Mwenyezi Mungu na kumtukuza na kumtaja kwa sifa zake anazozistaki, na kumswalia Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na Malaika na Mitume na Wajumbe wa Mwenyezi Mungu, na kujitahidi kuwazungumzia (ili huenda waathirike).
Kisha akasema "Muangamizwe na mkumbwe na huzuni enyi kikundi kiovu! Mlipotuomba usaidizi mkiwa kwenye mashaka tuliwasaidia kwa haraka, mkayatoa mapanga dhidi yetu sisi yaliyokuwa katika mikono yenu ya kuume, na mkatuelekezea moto tuliokuwa tumeuwasha kwa ajili ya adui wetu na adui wenu, mwishowe mkawa marafiki na maadui wa marafiki zenu, bila ya kuwepo uadilifu waliokuwa wamewafanyia nyinyi wala nyinyi kupata matarajio kutoka kwao.
Ole wenu! Basi kwa nini msituache mapanga yetu yakiwa yamefungwa na mahangaiko ya nafsi yakiwa yamefichika, na uamuzi ukiwa haujakatwa, lakini nyinyi mmekimbilia fitna

mfano wa nzige na kuiangukia mfano wa vipepeo (wanavyoanguka motoni).
Mwenyezi Mungu awaangamize! enyi watumwa wa umma huu, na waovu wa vikundi, na waliokiacha Kitabu (cha cha Mwenyezi Mungu),na wenye kuyabadili maneno yake, na vikundi vya madhambi, na mate ya shetani, na wavunjaji wa sunna.
Je imekuaje, mnawasaidia hao na kutupuuza sisi?
Ndio, wallahi, ni khiana ya tangu iliyokolea kwenye asili zenu na kuyavika matawi yenu, hata mkawa tunda mbovu kabisa kwa mtunzaji wa matunda haya, na chakula kizuri kwa wanyang'a nyaji.

ألا و إن الدعي ابن الدعي قد ركّز بين اثنتين بين السلّة و الذلّة و هيهات منّا الذلّة يأبى الله ذلك لنا و رسوله و المؤمنون و حجور طابت وحجور طهرت و أنوف حميّة و نفوس أبيّة من أن نؤثر طاعة اللئام على مصارع الكرام ألا و إني زاحف بهذه الأسرة مع قلّة العدد و خذلان الناصر

Mwana haramu ambaye baba yake ni mwana haramu amenilazimisha kuchagua baina ya mambo mawili, baina ya kuchukua upanga na kukubali kuwa dhalili, na haiwezekani kwetu kamwe kukubali kuwa dhalili, Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake na Waumini na watu wema na watu waliojitakasa na watu wenye hamasa na watu wenye nafsi sharifu wanatukatalia kupendekeza kuwatii watu duni badala ya kufa kifo cha heshima.
Basi jueni kuwa, mimi ninaondoka pamoja na jamaa zangu wa nyumbani hata ingawa idadi yetu ni ndogo, na watetezi wametupuuza."
Kisha Imam (a.s.) akaunganisha maneno yake kwa kuzisoma beti za shairi la Farwa ibni Masiik al-Muradi:

فإن نهزم فهزامون قدما          و إن نغلب فغير مغلبينا
و ما أن طبّنا جبن و لكن          منايانا و دولة آخرين
إذا ما الموت رفّع عن أناس          كلاكله أناخ بآخرينا
فأفنى ذلكم سرواة قومي          كما أفنى القرون الأوّلينا
فلو خلد الملوك إذاً خلدنا          و لو بقي الكرام إذاً بقينا
فقل للشامتين بنا أفيقوا          سيلقى الشامتون كما لقينا

Basi tukishinda ni kwa kuwa tuwashindi wa tangu
Natukishindwa sio wenye kushindwa daima
Hatuna ada ya kupatwa na woga bali
ni wakati wa kufa kwetu umefika na wengine kutawala
Ikiwa baadhi ya watu wataepushiwa mauti
Lakini hatimae yatawaangukia wengineo
Yamewaondolea furaha watu wangu
Kama yalivyo waangamiza watu wa kale
Lao kama wafalme waliishi milele nasi pia tungeishi milele
Na lao kama watukufu wangebaki sisi nasi tungebaki
Basi waambie wanaofurahia msiba wetu subirini
Watafikiwa wanao furahia msiba na yaliyo tufika.

Kisha akasema “Ama wallahi, hautawapita baada yake ila muda mfupi, kiasi cha muda wa kumpanda farasi, kisha mambo yawazungushe mzunguko wa jiwe la kusagia unga, na kuwahangaisha mahangaiko ya kipini.Haya ni mambo aliyoniahidi Baba yangu kutokea kama alivyoelezewa na Babu yangu. **(Basi kusanyeni mambo yenu na washirika wenu, kisha tena shauri lenu lisifichike kwenu, kisha mpitishe kwangu wala msinipe nafasi.**
**Hakika mimi nimemtegemea Mwenyezi Mungu Mola wangu na Mola wenu, hakuna mnyama yeyote isipokuwa**

**yeye anamwendesha atakavyo.Bila shaka Mola wangu yuko juu ya njia iliyonyooka).**
Ewe Allah wazuie matone ya mvua, na uwape miaka (ya kiangazi) kama miaka ya Nabii Yusuf, na tawalisha juu yao kijana atokae Thaqif awape kikombe kilichojaa kwa adhabu, kwani wametukadhibisha na kutukimbia, nawe ndiwe Mola wetu, tumekutegemea wewe na kwako tumeregea na maishilio ya mambo yote ni kwako."
Kisha akashuka (a.s.) na kutaka aletewe farasi wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliyekuwa akiitwa al-murtajaz, akampanda na kuwatayarisha maswahaba wake kwa mapigano.
Imepokewa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.) kwamba "Walikuwa wapanda farasi arobaini na tano na mia moja waliokuwa wakitembea." Na imepokewa pia kinyume chake.

## U'MAR IBNI SA'AD ATANGULIA NA KUWATUPIA MSHALE WA KWANZA JESHI LA IMAM HUSEIN (A.S.).

Mpokezi anasema: U'mar ibni Sa'ad akasonga mbele na kuwatupia mshale majeshi wa Imam Husein (a.s.), na kusema "Nishuhudieni mbele ya amiri kuwa mimi ndiye niliyekuwa wa kwanza kutupa mshale." Kisha ikafwatilizia mishale miingine kutoka kwao, ikawamwagikia mfano wa mvua. Imam (a.s.) akawaambia maswahaba wake "Simameni, Rahimakumullah, muyaelekee mauti, mauti ambayo hamna budi kuyaonja, kwani hii mishale ni wajumbe wa watu hawa kwenu."

## WAKAPIGANA KWA MUDA NA KIKUNDI KATIKA JESHI LA IMAM HUSEIN (A.S.) KIKAUWAWA.

Wakapigana kiasi cha muda wa mchana kwa kufanyiana ushambulizi, mwingine baada ya mwingine, hata kikauwawa kikundi katika maswahaba wa Imam Husein (a.s.).
Mpokezi anasema: Hapo basi Imam Husein (a.s.) alikipiga kidevu chake na kusema:

اشتد غضب الله على اليهود إذ جعلوا له ولداً، و اشتد غضبه على النصارى إذ جعلوه ثالث ثلاثة، و اشتد غضبه على المجوس إذ عبدوا الشمس و القمر دونه، و اشتد غضبه على قوم اتفقت كلمتهم على قتل ابن بنت نبيهم. أما و الله لا أجيبهم إلى شيء مما يريدون حتى ألقى الله و أنا مخضب بدمي

“Mwenyezi Mungu alipatwa na ghadhabu kali kwa mayahudi, walipomfanya kuwa ana mwana, na alipatwa na ghadhabu kali kwa manaswara, walipomfanya kuwa ni wa tatu
katika utatu, na alipatwa na ghadhabu kali kwa majusi, walipoabudu jua na mwezi badala yake, na alipatwa na ghadhabu kali kwa watu (katika umma huu) walipokubaliana kumuuwa mwana wa Binti ya Mtume wao.Ama wallahi, mimi sitowakubalia chochote katika wanachotaka hadi nikutane na Mwenyezi Mungu nikiwa nimezitia (ndevu zangu) rangi kwa damu yangu.”
Imepokewa kutoka kwa Imam as-Swadiq (a.s.) ya kwamba alisema “Nilimsikia baba yangu (a.s.) akisema: Husein (a.s.) walipokutana na U’mar ibni Sa’ad (la’anahullah) na vita vikapiganwa, Mwenyezi Mungu alimteremshia nusra yake hata kufikia karibu na kichwa chake Husein (a.s.), kisha akampa khiari, achague baina ya kuwashind maadui wake na

baina ya kukutana na Mola wake, akachagua kukutana na Mola wake."

## KUJIUNGA KWA HURR NA JESHI LA IMAM HUSEIN (A.S.) NA KUFA KWAKE SHAHIDI.

Mpokezi wa habari hizi anasema "Kisha Imam Husein (a.s) akapaza sauti na kusema:

أ ما من مغيث يغيثنا لوجه الله أ ما من ذاب يذب عن حرم رسول الله

"Je hakuna msaidizi atusaidie kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu!? Je, hakuna mtetezi awatetee mahaarimu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!?"
Mpokezi anasema: Mara Hurr ibni Yazid ar-Riyahi akamwelekea U'mar ibni Sa'ad na kumwambia "Je wewe utapigana na huyu mtu?"
Akamjibu "Ndio wallahi, nitapigana naye mapigano ambayo uchache wake ni vichwa vipeperuke na mikono ipotee."
Mpokezi anasema: Hurr akaondoka na kusimama kando na maswahaba wake akawa ni kama kuetetemeka kwa woga. Muhajir ibni Aus akamwambia "Hakika hali yako ni ya kutia shaka.Lao kama kungeulizwa: Ni nani mashujaa zaidi katika watu wa mji wa al-Kufa? Singekosa kukutaja katika idadi hiyo.Basi ni hali gani hii ninayo kuona nayo?"
Akasema "Wallahi! Ninaichagulia nafsi yangu baina ya pepo na moto, na wallahi sikichagui chochote kingine badala ya pepo, hata kama nitakatwakatwa na kuchomwa."
Kisha akampiga farasi wake na kumwelekea Imam Husein (a.s.) huku ameuweka mkono wake kichwani na kusema "Ewe Allah! Hakika mimi nimetubu kwako, basi nikubalie toba yangu, kwani nimezitisha nyoyo za wapenzi wako na Wana wa Binti ya Mtume wako."

Kisha akamwambia Imam Husein (a.s.) “Nijaaliwe kuwa fidia yako! Mimi ni mwenzako aliye kuzuia kurudi na kukubana.Wallahi sikudhani kuwa watu hawa watafikia kukufanyia haya ninayoyaona, nami kwa yote haya natubia kwa Mwenyezi Mungu, basi je unaona kuwa ninaweza kukubaliwa toba yangu?”

Imam Husein (a.s.) akamwambia, "Na’am, Mwenyezi Mungu atakusamehe, basi shuka.”

Hurr akasema “Mimi ni bora kwako nikiwa mpanda farasi kuliko nikiwa katika hali ya kutembea, na mwisho wangu hatimae utakuwa kushuka.”

Kisha akasema,“Kwa kuwa mimi nilikuwa ndiye mtu wa mwanzo kutoka dhidi yako, basi niruhusu niwe wa mwanzo kuuawa mbele yako ili niwe miongoni mwa watu watakaopeana mkono na Babu yako Muhammad (s.a.w.w.) kesho siku ya Qiyama.”

Msimulizi wa yaliyopita anasema: Hurr alikuwa akikusudia wa mwanzo kuuwawa baada ya sasa, kwani kikundi cha maswahaba wengine walikuwa wameshauwawa kabla yake kama ilivyopokelewa.

Basi Imam (a.s.) akamruhusu.Akapigana vizuri sana hata kuwauwa mashujaa na majasiri wengi, kisha akafa shahidi. Alibebwa na kupelekwa kwa Imam Husein (a.s.). Imam (a.s.) akawa anampangusa udongo uliokuwa usoni mwake huku akisema “Wewe ni Huru kama alivyokuita mama yako. Huru duniani na huru huko Akhera.”

## KUPIGANA KWA BUREIR NA KUFA KWAKE SHAHIDI.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Bureir ibni Khudheir akatoka kwa mapambano. Alikuwa mtu mtawa na mwingi wa ibada.

Akatoka Yazid ibni Ma'aqil ili kupambana naye, wakakubaliana kufanya mubahala (maapizano kwa Mwenyezi Mungu) kwamba aliye katika haki amuuwe aliye katika upotofu, wakakubiliana kupambana, Burair akamuua Yazid, na kuendelea kupigana na wengineo kisha hatimaye akauawawa 'Ridh-wanullahi a'leih'.

## **KUPIGANA KWA WAHAB IBNI HABAAB NA KUFA KWAKE SHAHIDI.**

Mpokezi anasema: Wahab ibn Hibab al-Kalbi naye akaingia kwenye uwanja wa mapambana akapigana vyema kwa upanga na kuonyesha ushupavu katika Jihadi.
Bwana huyu alikuwa amefwatana na mkewe pamoja na mama yake. Ikawa kipindi fulani alirudi (kwenye mahema) na kumuambia mama yake "Ewe mama, je uko radhi nami au la?"
Mama yake akasema "La, siwi radhi hadi utakapouwawa mbele ya Husein (a.s.)."
Naye mkewe akasema "Billahi a'leika, nakuomba usiniachie majonzi kwa kuuwawa."
Mama yake akamwambia, "Mwanangu yapuuze maneno ya mkeo na rejea ukapigane mbele ya Mwana wa Binti ya Mtume wako, ili upate maombezi ya Babu yake siku ya Qiyama."
Basi akarudi na kuendelea kupigana mpaka mikono yake yote miwili ikakatwa.
Mkewe huyu bwana akachukua mkongojo akawa anamfuata mumewe huku akimwambia, "Baba yangu na mama yangu wawe fidia kwako! Endelea kupigana kuwatetea watu wema, mahaarimu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)."
Wahab akamfuata ili amrejeshe mahali waliko wanawake, lakini mkewe akaishika sehemu ya nguo zake na kusema. "Sirudi kamwe mpaka nitakapokufa pamoja nawe."

Imam Husein (a.s.) (alipoiona hali hiyo) akasema “Hakika mumekwisha kulipwa mema kwa kujitoa kwenu muhanga kwa ajili ya watu wa Nyumba ya Mtume (s.a.w.w.), rudi kwa wanawake, Mwenyezi Mungu akurehemu.” Akarudi kwa wanawake.
Al-Kalbi aliendelea kupigana hata akauwawa ‘Ridh-wanullahi a’leih’.

## KUPIGANA KWA MUSLIM IBNI A’USAJA NA KUFA KWAKE SHAHIDI.

Kisha alitoka Muslim ibni A’usajah, akapigana na maadui kwa ushupavu, na kuyavumilia makali ya shida alizokabiliana nazo mpaka alipoanguka chini kwenye ardhi akawa karibu kukata roho, Imam Husein (a.s.) akiwa pamoja na Habib ibni Mudhahir akaenda hapo alipoanguka.
Imam Husein (a.s.) akamwambia, “Rahimakallah, ewe Muslim! Katika waumini kuna ambao wamekwisha kufa (wakitetea dini ya Mwenyezi Mungu), na wapo wengine wanakingujea kifo, na kamwe hawakubadilisha misimamo yao.”
Habib akamsogelea na kusema “Kifo chako, wallahi ni kizito sana kwangu, ewe Muslim! basi jibashirie kupata pepo.”
Muslim akajibu kwa sauti ya unyonge (kwani alikuwa karibu kukata roho) na kumwambia Habib “Mwenyezi Mungu nawe akubashirie kupata kheri.”
Kisha Habib akamwambia Muslim “Lao kama nisingejua ya kwamba mimi nitakufuatia, basi ningependa uniusie kila lililomuhimu kwako.”
Muslim akamwambia Habib, "Nakuusia juu ya huyu (akamuashiria Imam Husein a.s.) pigana katika kumtetea mpaka ufe.”

Habib akamwambia Muslim “Basi nitakufurahisha kwa kutimiza wasia wako.” Kisha akakata roho ‘Ridh-wanullahi a’leih’.

## KUPIGANA KWA UMAR IBNI QARDHA AL-ANSWARI NA KUFA KWAKE SHAHIDI.

Kisha akatoka A’mru ibni Qardha al-Answari, akamuomba Imam Husein (a.s.) ruhusu ya kupambana, akamrusu.Akapambana mapambano ya mwenye shauku ya kupata jazaa, na akajitolea katika njia hii ya Mwenyezi Mungu, na kuwauwa watu wengi katika kikundi cha Ibni Ziyad.
Bwana A’mru aliweza kukusanya mafanikio na jihadi, kwani kila mshale uliomlenga Imam Husein (a.s.) alikuwa akiuzuia kwa mkono wake, na kila upanga uliomwelekea alikuwa akiuzuia kwa kiwiliwili chake.Kwa kuihatarisha nafsi yake alimuhifadhi Imam Husein (a.s.), akawa hakupatwa na chochote kibaya. Kutokana na tendo hili A’mru alipatwa na majeraha mengi sana.
Kisha akamwelekea Imam Husein (a.s.) na kusema “Yabna Rasulillah!Je, nimetekeleza?”
Akamjibu, “Na’am, umetekeleza.Wewe unanitangulia kuingia peponi, basi mfikishie Mjumbe wa Mwenyezi Mungu salamu zangu, na mjulishe kuwa ninafuatia.”
Akaendelea kupigana hadi akauwawa, ‘Ridh-wanullahi a’leih’.

## KUPIGANA KWA JON MTUMWA WA ABU DHAR NA KUFA KWAKE SHAHIDI.

Kisha akatoka kwa mapambano, Jon mtumwa wa Abu Dhar.Alikuwa mtumwa mweusi.

Imam Husein (a.s.) akamwambia "Wewe unaruhusa kutoka kwangu, kwani ulitufwata kwa kutaka afia, basi usipatwe na balaa kwa kufwata njia yetu."
Akamjibu "Yabna Rasulillah! Itawezekanaje katika siku za raha nala chakula chenu, na katika siku za shida nawakimbia! Wallahi, hakika harufu yangu ni yenye kuchukiza, na nasabu yangu ni duni, na rangi yangu ni nyeusi, basi nifariji kwa kunipa pepo, harufu yangu ipate kuwa nzuri, na nasabu yangu iwe tukufu, na uso wangu upate kunawiri.Laa, wallahi!Siwaachi mpaka damu hii nyeusi ichanganyikane na damu zenu."Kisha akapigana mpaka kuuwawa 'Ridh-wanullahi a'leih'.

## KUPIGANA KWA UMAR IBNI KHALID AS-SWAIDAWI NA KUFA KWAKE SHAHIDI.

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Kisha akatoka kwa mapambano, A'mru ibni Khalid as-Swaidawi, akamwambia Imam Husein (a.s.) "Ya Aba A'bdillah! Nijaaliwe kuwa fidia kwako! Nimepatwa na hamu ya kuwafwata wenzangu, na nimechukia kubaki nyuma nikakuona ukiwa umeachwa pweke, ukiwa umeuwawa mbele ya jamaa zako."
Imam Husein (a.s.) akamwambia "Tangulia, sisi tutakufwata baada ya muda kidogo."
Akatoka na kupambana mapambano makali hata mwishowe kuuwawa, 'Ridh-wanullahi a'leih'.

## KUPIGANA KWA HANDHALA IBNI AS'AD ASH-SHAMI NA KUFA KWAKE SHAHIDI.

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Kisha akaja Handhala ibni Sa'ad ash-Shaami na kusimama mbele ya Imam Husein (a.s.) akawa anamkinga kwa uso wake na shingo yake kutokana na mishale na mapanga na mikuki ya maadui, huku akinadi kwa

sauti ya juu “Enyi watu wangu, hakika mimi ninawakhofieni mfano wa siku ya makundi, mfano wa hali ya watu wa Nuhu na A’di na Thamudi na wale waliokuwa nyuma yao, na Mwenyezi Mungu hataki dhulma kwa waja (wake). Enyi watu wangu, kwa hakika nawakhofieni siku ya kuitana, siku mtakapogeuka kurudi nyuma, hamtakuwa na mlinzi kwa Mwenyezi Mungu,na mwenye kupotezwa na Mwenyezi Mungu, basi huyo hana wa kumuongoza.Enyi watu wangu, msimuuwe Husein mkasababisha Mwenyezi Mungu kuwaangamiza kwa adhabu.Hakika amekwisha shindwa anayezua uongo.”

Kisha akamwangalia Imam Husein (a.s.) na kumwambia “Je, si umewadia wakati wa kwenda kwa Mola wetu, tuwafwate wenzetu?”

Imam (a.s.) akamjibu “Bali nenda kwa kilicho bora zaidi kwako kuliko dunia hii na vyote vilivyoko ndani yake, nenda kwa ufalme usioisha.”

Akatoka na kupambana kwa ujasiri mwingi, na kusubiri a na kuvumilia makali ya vita hata akauwawa ‘Ridh-wanullahi a’leih’.

## SWALA YA IMAM HUSEIN (A.S.) NA MASWAHABA WAKE.

Mpokezi anasema “Ulipofika wakati wa swala ya adhuhuri, Imam Husein (a.s.) aliwaamuru Zuheir ibnil Qain na Sa’id ibni A’bdillah al-Hanafi wasimame mbele yake pamoja na nusu ya waliobaki naye katika maswahaba, kisha akawaswalisha swala ya khofu.

Maadui walimtupia mshale Imam Husein (a.s.), lakini Sa’ad ibni Abdillah al-Hanafi akasonga mbele, akawa anamkinga Imam (a.s.) kwa nafsi yake.Akaendelea hivi hata mwishowe akaporomoka kwenye ardhi huku akisema “Ewe Allah! Walaani laana ya A’di na Thamud.Ewe Allah! Mfikishie

Mtume wako salamu zangu, na mjulishe maumivu ya majeraha niliyoyapata, kwani nilitaka thawabu kutoka kwako katika kukinusuru kizazi cha Mtume wako.”Kisha akakata roho ‘Ridh-wanullahi a’leih’.
Baada ya kufariki alipatikana kuwa na mishale kumi na tatu na majeraha mengi kutokana na kukatwa na mapanga na kuchomwa na mikuki.

## KUPIGANA KWA SUWEID IBNI AMRU IBNI ABIL MUTWAA’I NA KUFA KWAKE SHAHIDI.

Mpokezi wa yaliyojiri anasema: Kisha akatoka Suwaid ibni A’mru Abil Mutwaa’i, alikuwa ni mtu sharifu na mwingi wa kuswali, akapambana mfano wa simba mkali mwenye ushujaa, na kuvumilia balaa zilizokuwa zimeshuka mpaka mwishowe akaanguka baina ya waliokuwa wameshauwawa huku amedhoofishwa na wingi wa majeraha.Akabaki katika hali hii, hatikisiki, hata alipowasikia wakisema “Husein ameuwawa!” akajivuta na kutoa kisu kwenye viatu vyake, na kupigana nacho hata mwishowe akauwawa ‘Ridh-wanullahi a’leih’.
Mpokezi anasema: Wakawa maswahaba wake Imam Husein (a.s.) wanapambana mbele yake Imam, na walikuwa kama ilivyosemwa katika:

قوم إذا نودوا لدفع ملمّة * و الخيل بين مدعّس و مكردس
لبسوا القلوب على الدروع أقبلوا * يتهافتون إلى ذهاب الأن

Wao ni watu wanapoitwa kuiondoa balaa
Huku farasi wamebeba mikuki na vikosi vya majeshi
Wanazivaa nyoyo zao juu ya deraya zao na kusonga mbele
Huku wakifwatana mmoja baada ya mwingine katika kuzitoa nafsi.

**KUPIGANA KWA ALI IBNIL HUSEIN (A.S.) NA KUFA KWAKE SHAHIDI.**

Walipouwawa wote akawa hakuna aliyebaki na Imam Husein (a.s.) ila watu wake wa nyumbani, Ali ibni Husein (a.s.) alitoka, ambaye alikuwa mwenye uso wenye kupendeza sana na mwenye tabia njema, akamuomba Baba yake ruhusa ya kwenda kupambana, akamrusu.
Kisha akamtazama kwa mtazamo wa aliyekata tamaa ya kuonana naye tena, akainamisha macho yake na kulia.Kisha akasema:

اللهم اشهد فقد برز إليهم غلام أشبه الناس خَلقا و خُلقا و منطقاً برسولك (صلّى الله عليه وآله وسلّم) و كناّ إذا اشتقنا إلى نبيّك نظرنا إليه

“Ewe Allah! Shuhudia, hakika amewatokea kupambana nao kijana ambaye kwa umbo na tabia anafanana sana na Mjumbe wako (s.a.w.w) nasi tulipokuwa na hamu na Mtume wako tulikuwa tukujituliza kwa kumtizama yeye.”
Imam Husein akapaza sauti na kusema:

يا ابن سعد قطع الله رحمك كما قطعت رحمي

“Yabna Sa’ad! Mwenyezi Mungu aikate nasaba yako kama ulivyoikata nasaba yangu.”
Basi Ali akawaelekea maadui na kupigana nao mapigano makali na kuwauwa watu wengi sana kati yao.Kisha akarudi kwa Baba yake na kumwambia “Ewe Baba, kiu kinaniuwa na uzito wa chuma umenichosha, je ninaweza kupata kinywaji cha maji?”
Imam Husein (a.s.) akalia na kusema “Ni nani wakunisaidia, ewe mwanangu! Nitakutolea wapi maji? Pigana kidogo, si

muda mrefu utakutana na Babu yako Muhammad (s.a.w.w.) akunyweshe kikombe cha maji ambacho kitakutosheleza kiu chako na hutahisi tena kiu."
Basi akarudi kwenye uwanja wa mapambano na kupigana kwa nguvu sana lakini Munqidh ibni Murra al-A'bdi akamtupia mshale ambao ulimpata na kumfanya adondoke chini.Akanadi kwa sauti kwa kusema "Ewe Baba pokea salamu kutoka kwangu! Ndio huyu Babu yangu (naye) anakutolea salamu na kukwambia, fanya haraka uje huku tuliko." kisha alivuta pumzi ndefu na kukata roho.
Imam Husein (a.s.) alikuja mpaka mahali alipofia mwanawe, akaweka shavu lake juu ya shavu la mwanawe na kusema:

قتل الله قوما قتلوك ما أجرأهم على الله و على انتهاك حرمة الرسول. على الدنيا بعدك العفاء

"Mwenyezi Mungu awaangamize watu waliokuuwa ewe mwanangu, ni majasiri kiasi gani kwa Mwenyezi Mungu na kwa kumvunjia heshima Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).Dunia iangamie baada yako."[1]

---

[1] Karbala iliwafanya nini wana wa Ahmad
Vingapi walivyoporwa wana wa Ahmad
Miguu na mikono ilikatwa kwa mapanga
Damu zisizokuwa na hatia zilimwagwa
Miili mingapi ya wema iliyokatakatwa
Huko moyo wa Husein ulilia kwa huzuni
Kwa kijana bora aliyependwa na waumini
Kakusanya sifa njema umbo bora na tabia
Kamshabihi Mtume kwa sauti umbo na tabia
Aliwakumbusha Mtume wakimtazama yeye
Kapambana kisimba kwa ushujaa wa babuye
Kiu kilimkata koo kwa ukali wa pambano

Mpokezi wa habari hizi anasema: Baada ya hapo, Bibi Zainab bintu Ali alitoka huku akinadi kwa sauti: "Ewe kipenzi changu! Ewe mwana wa Ndugu yangu!"Akaja na kujiangusha juu yake (na kumkumbatia).
Imam Husein (a.s.) akaja na kumuondoa na kumrudisha walikokuwa wanawake.
Baada ya kuuawa kwa Ali ibni Husein (a.s.) ikawa sasa anatoka mtu baada ya mwingine katika watu wa Nyumba ya Imam Husein (a.s.), wakawa wamewauawa watu wengi katika maadui.
Hali hiyo ilimfanya Imam Husein (a.s.) aseme kwa sauti ya juu "Fanyeni subira enyi wana wa Ami zangu! Fanyeni subira enyi watu wa Nyumba yangu! Wallahi hamtaona unyonge kamwe tena baada siku ya leo."

## **KUPIGANA KWA QASIM IBNIL HASAN (A.S.) NA KUFA KWAKE SHAHIDI.**

Mpokezi wa habari hizi anasema: Kisha alitoka kijana mwingine katika watu wa Nyumba ya Imam (a.s.) (aliyekuwa akiitwa Qasim) ili kupigana na maadui.

---

Kamuomba Babae maji baada ya pambano
Zawadi ya mzazi kwa ushujaa aliyoonyesha
Husein alisikitika kwa kukosa kumzawidisha
Kwani ulimi wake likuwa mkavu kama ukuni
Alirudi kupambana na kuuwawa kiushujaa
Huyu kamchoma kwa mkuki huyu kwa khanjari
Akaita Baba niokoe maadui wamenizingira
Husein akamjia kama simba mwenye hasira
Kifo chake kilimliza Imamu na wote khalaiki.

Kijana huyu alikuwa na uso wenye kung'ara kama kipande cha mwezi, na alipoingia katika mapigano alipigwa upanga kichwani na mtu mmoja aliyekuwa akiitwa Ibn Fudhail al-Azdi, upanga ule ukampasua, akadondoka chini kifudifudi na kuita "Ewe Ami yangu!”

Imam Husein aliposikia sauti ya kijana huyu alitazama kama anavyotazama kipanga anapotaka kuvamia mawindo, kisha akashambulia kushambulia kwa simba mkali mwenye hasira nyingi, akampiga lbn Fudhail kwa dhoruba kali ya upanga.Akajaribu kuizuia kwa mkono wake lakini Imam akamkata katika fundo la mkono. Akapiga ukelele kwa nguvu wakamsikia askari wa Yazid, wakavamia ili kumuokoa, lakini kuja kwao kwa wingi na kwa khofu kulisababisha wakamkanyagakanyaga kwa miguu ya farasi mpaka akafariki.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Vumbi lililokuwa limejaa kote kutokana na kukimbia kwa farasi, lilipo pungua nilimuona Imam Husein (a.s.) akiwa amesimama karibu na kichwa cha yule kijana wake ambaye alikuwa akirusha mateke kwa mgu wake katika hali ya kukata roho, na huku Imam Husein anasema “Walaaniwe watu waliokuuwa.Mhasimu wao siku ya Qiyama atakuwa Babu yako.”

Kisha akasema, “Wallahi limekuwa ni jambo zito kwa ami yako, wewe kumwita asikuitike au akuitike lakini asikusaidie kitu. Wallahi! Hii ni siku ambayo dhulma yake imezidi na wenye kutunusuru wamekuwa wachache mno.”

Kisha Imam Husein (a.s.) alimbeba kijana huyo (baada ya kufariki) na kumuweka pamoja na maiti wengine katika watu wa nyumba yake.

## IMAM HUSEIN (A.S.) ABAKI PEKEE, KISHA ANADI KWA SAUTI AKIOMBA NANI ATAKAYE MNUSURU.

Mpokezi anasema: Imam Husein (a.s.) alipoona mauaji ya vijana wake na wapenzi wake aliazimia kupambana na maadui zake yeye mwenyewe binafsi.
Akaanza kwa kutoa mwito:

هل من ذاب يذب عن حرم رسول الله ؟ هل من موحد يخاف الله فينا؟ هل من مغيث يرجو الله بإغاثتنا؟ هل من معين يرجو ما عند الله في إعانتنا؟

"Je kuna mtetezi atakayewatetea mahaarimu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Je kuna mwenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu atakayemuogopa Mwenyezi Mungu kwa ajili yetu sisi? Je kuna mwenye kutoa msaada hali ya kuwa anatarajia mema kwa Mwenyezi Mungu katika kutusaidia sisi? Je kuna mwenye kuauni anayetarajia radhi ya Mwenyezi Mungu kwa kutuauni sisi?"
Mwito huu wa Imam Husein (a.s.) uliwafanya wanawake waliokuwepo hapo walie kwa sauti.

## MWANA MCHANGA WA IMAM HUSEIN (A.S.) AFA SHAHIDI.

Imam Husein (a.s.) akaenda kwenye mlango wa hema na kumwambia Bibi Zainab
"Hebu nipe huyo mwanangu mdogo nipate kumuaga."
Akamchukua mtoto huyo akawa anataka kumbusu, lakini Harmalah ibni Kahil akamtupia mshale mtoto yule, ukampata shingoni na kumrararua vibaya sana hata kumuuwa.

Imam Husein (a.s.) akamwambia Bibi Zainab "Mchukue mtoto." kisha akaviweka viganja vyake ili kuizuia damu ya mwanawe kumwagika chini.Ikawa inatiririka katika viganja vyake hadi vikajaa damu.Akairusha damu ile juu mbinguni kisha akasema "Yamekuwa mepesi kwangu yaliyonifika (kwa kuwa yote) yanatendeka mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu."

Imam al-Baqir (a.s.) amesema, "Hakuna hata tone moja la damu hiyo lililodondoka chini."

Imepokewa kwa pokezi nyinginezo, ambazo zinakubaliana na akili zaidi, kwani hali iliyokuwepo haingeweza kumpa wakati wa kumuaga mwanawe, kwa kuwa alikuwa ameshughulishwa na vita na mapambano, bali kilichotokea ni kuwa Bibi Zainab (a.s.) alimletea Imam (a.s.) mwanawe na kumwambia "Ewe ndugu yangu! Huyu mwanao, ana siku tatu hajaonja hata tone la maji, mchukue umuombee kinywaji cha maji."

Imam (a.s.) akamchukua mkononi mwake na kuwaambia maadui, "Enyi watu! Mumeshawauwa mashia wangu na watu wangu wa Nyumbani, na amebaki huyu mtoto mchanga anayekufa kwa kiu, basi mnyweshеni kinywaji cha maji." Akiwa katika hali hii ya kuwakhutubia, mtu mmoja alimtupia mwanawe mshale uliomrarua vibaya hata akafariki.[1]

---

[1]Waliuwawa wote hawakubaki ila watoto na wanawake
Watoto walilia na kupaza sauti kiu kiu ni nani atuokoe

Titi zilikuwa hazina hata tone la maziwa kiu wakitulize
Imamu kakabidhiwa mwanae kwa kuwa kiu kimemzidi

Kenda nae kwao kumuombea japo tone la maji au zaidi
Kawahubiria na kuwanasihia huenda wakangiwa imani

Walimjibu bila ya kuchelea mwisho wao utakaowafikia

Imam (a.s.) akawaombea laana kama alivyofanya kuwaombea Mukhtar na wengineo.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AMPANDA FARASI WAKE, NA KUELEKEA ALFURAT WAKIWA ABBAS (A.S.).

Mpokezi wa habari hizi anasema: Kiu kilipomzidi Imam Husein (a.s.) akapanda farasi wake na kuelekea alFurat (ili kuchota maji) huku Abbas (a.s.), nduguye, yuko mbele yake, lakini wapanda farasi wa lbn Sa'ad wakamzuia, na mtu mmoja katika Bani Daaram akamtupia Imam Husein mshale (a.s.), ukamchoma katika mdomo wake mtukufu.
Imam (a.s.) akauchomoa mshale huo na kuviweka viganja vyake chini ya mdomo wake, damu ikawa inatairirika ndani ya viganja, vilipojaa akairusha damu hiyo juu, kisha akasema "Ewe Allah! Hakika mimi nakushitakia mambo anayofanyiwa Mwana wa Binti ya Mtume wako."

## ABBAS (A.S.) AFA SHAHIDI

Kisha maadui hao wakamzuia Abbas ibni Ali (a.s.) akawa mbali na Imam (a.s.) na kumzingira kila upande na mwishowe wakamuuwa (Qaddasallahu ruhahu).
(Na katika upokezi mwingine: Abbas (a.s.) alipoona kuwa watu wengi katika jamaa zake wameuwawa, akawaambia

---

Wakampiga mwana mshale      shingoni mwake kamwingia

Mwana kalalama kaaga dunia      mikononi mwa babae kafiya
Damu zikamjaa Imam mikononi    kazitupa mbinguni hazikuregea

Wakamwamba katu maji hupati      chembe ya huruma haikubakia
Imamu kaomba laana iwashukie    kama alivyowaombea Mukhtari

ndugu zake wa baba na mama, A’bdullah na U’thman na Ja’afar, “ Tangulieni enyi wana wa mama yangu ili niaone kuwa mumetoa nasiha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake.”

Kisha akamwelekea A’bdullah, aliyekuwa mkubwa zaidi kumliko U’thman na Ja’afar, na kusema: Tangulia ewe ndugu ili nikuone ukiwa umeuwawa na kukufanyia subira (nikitaraji thawabu kwa Mwenyezi Mungu).

Basi wakapigana na maadui, mbele yake Abul Fadhl hadi wote kuuwawa.

Abbas (a.s.) hakuweza kuvumilia tena kubaki nyuma baada ya kuuwawa maswahibu wake na jamaa zake wa nyumbani, na huku anamuona Imam Husein (a.s.) amezidiwa idadi na maadui, hana wa kumsaidia, na huku kulia majonzi kwa wanawake na kulalama kwa watoto wakilia kiu kumemjaa kwenye masikio.Akaamua kumuomba Imam Husein (a.s.), ndugu yake, ruhsa ya kutoka kupambana.

Imam Husein akamwambia, “Ewe ndugu yangu! Wewe ndiwe mbebaji wa bendera yangu.”

Abbas (a.s.) akajibu, “Moyo wangu umekereka kutokana na hawa wanafiki, ninataka kuchukua kisasi changu kutoka kwao.”

Basi Imam Husein (a.s.) akamuamuru atafute njia ya kuwaletea watoto maji.

Abbas (a.s.) akaenda na kuwatolea wa’adhi wale watu na kuwatahadharisha kutokana na ghadhbu ya Mwenyezi Mungu Jabbari, lakini haukufaa.

Akaita kwa sauti ya juu:Yaa U’mar ibnu Sa’ad!Huyu ni Huseini, Mwana wa Binti ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, mumeshawauwa maswahaba wake na jamaa zake wa nyumbani, na hawa ayali wake na watoto wake wana kiu, basi wapeni maji wanywe, kwani kiu kinazichoma nyoyo zao, bali huku yeye anawaambieni, “Niacheni niende Roma au Uhindini, nami nitawaachieni Hijazi na Iraq.”

Shimru akapiga kelele kwa sauti ya juu kabisa na kusema, “Yabna Abi Turab! Lao kama ardhi yote ilikuwa maji, na (maji) yakawa mikononi mwetu hatungewanywesha hata tone moja, mpaka mtakapoingia kwenye bai’ah ya Yazid.” Abbas akarudi kwa Nduguye ili kumjulisha, akawasikia watoto wakilia kwa sauti kutokana na kiu, akachemkwa kwa ghera na hamasa ya Bani Hashim, akampanda farasi wake, na kukichukua kiriba na kuulekea Mto Furat.
Akazingirwa na majeshi elfu nne, wakampiga kwa mishale, lakini hakuwapatia umuhimu wowote, wala kutishwa na wingi wao, bali aliwashambulia akiwapiga kwa upanga wake, akawa hakuna anayebaki wima.Akawakimbiza toka kwenye Mto Furat, na kuweza kuchota maji kwa viganja vyake ili kuyanywa, lakini akakumbuka kiu cha Imam Husein (a.s.) na waliokuwa naye, akayamwaga maji yaliyokuwa mikonono mwake na kusema:

يا نفس من بعد الحسين هوني * و بعده لا كنتِ ان تكوني
هذا الحسين وارد المنون * و تشربون بارد المعين
تالله ما هذا فعال ديني

Ewe nafsi baada ya Husein jidhalilishe
Baada yake hukuwa ni mwenye kuwepo
Huyu ni Husein anaelekea kwenye mauti
Na huku unakunywa chemchemi baridi
Wallahi hiki si kitendo cha yangu dini.

Kisha akakijaza kiriba maji na kumpanda farasi wake na kuelekea upande zilipokuwa hema, lakini akazuiwa njiani.Akawashambulia na kuwapiga, na kuwauwa wengi kati yao, na kuwaondoa jiani, huku akisema:

لا ارهب الا الموت اذا الموت زقا

حتى أواري في المصاليت لقى
نفسي لسبط المصطى الطهر وقى
إني انا العباس أغدو بالسقا
و لا اخاف الشر يوم الملتقى

Siyaogopi kamwe mauti, mauti yanapopaza kuita
Hadi nitakapowazika mashujaa kwenye mapanga
Nafsi yangu ni himaya kwa Mjukuu wa Mustafa Mtoharifu
Mimi Ndiye Abbas nimetoka na chombo cha kuwanywesha
Wala siogopi shari siku hii ya mapambano

Zaid ibnur Ruqaad al-Jujani akamnyemelea toka nyuma ya mtende na kuupiga mkono wake wa kulia hata kuukata.Lakini akauchukua upanga kwa kushoto kwake, na kuwashambulia, huku akisema:

والله إنْ قطعتُمُ يميني * إني أُحامي ابداً عن ديني
وعن إمام صادق اليقين * نجل النبيِّ الطاهر الامين

Wallahi mkiukata mkono wa kuume
Mimi nitaihami daima dini yangu
Na Imamu mwenye yakini sadiki
Mjukuu wa Mtume Mtoharifu Amini

Wala hakuuujali mkono wake wa kuume, baada ya kuwa hamu yake yote ilikuwa kuwafikishia maji wana wake Imam Husein (a.s.) na ayali zake.
Lakini Hakiim ibnut Tufeil alijificha nyuma ya mtende, na kumpiga mkono wake wa kushoto na kuukata alipokuwa akipita karibu naye.
Akasimama na huku analisoma shairi:

يا نفس لا تخشي من الكفار وابشري برحمة الجبار
مع النبي السيد المختار قد قطعوا ببغيهم يساري
فأصلهم يا رب حر النار

Ewe nafsi usiwaogope makafiri
bali jibashirie Rehma ya Jabbari
Pamoja na Mtume Bwana Mteule
wamekata kidhulma wa kushoto
Basi Mola waingize mkali moto

Wakamshambulia kwa idadi kubwa!! Mishale ikammwagikia kama mvua.
Mshale mmoja ukakipata kiriba na kukitoboa, maji yake yakamwagika.
Mshale mwingine ukakipata kifua chake.
Na mwingine ukalipata jicho lake.
Mara mtu mwingine akampiga kwa nguzo ya chuma kwenye kichwa na kuupasua utosi wa kichwa chake!
Akaanguka chini huku akinadi:

عليك مني السلام يا ابا عبد الله، أدركني يا أخي!!

"Salamu kutoka kwangu zikufikie Ya Aba A'bdillah, nidiriki ewe ndugu yangu!!"
Imam Husein (a.s.) akamjia mbio, akampata katika hali hii, mikono yake miwili ikiwa imekatwa, na mshale umechomoza kwenye jicho lake.
Akasema, "Sasa ndipo mgongo wangu umevunjika, na njia zangu zimepungua, na maadui wangu wakafurahia mswiba wangu."
Imam (a.s.) akiwa katika hali hii karibu naye, mara Abul Fadhl (a.s.) akapatwa na fahamu na kusema, "Ya Seyyidi! (Ewe Bwana wangu!) unataka kufanya nini?"

Akamjibu, “Ninataka kukubeba nikupeleke kwenye hema.” Baada ya muda mfupi Abul Fadhl alikata roho kichwa chake kikiwa mapajani mwake Abu Abdillahil Husein (a.s.).
Imam Husein (a.s.) akarudi kwenye hema huku moyo umevunjika, mwenye huzuni, akilia, akiyafuta machozi yake kwa mkono wa nguo yake.[1])
Kuuwawa kwa Abbas (a.s.) kulimfanya Imam Husein (a.s.) kulia sana kwa kumpoteza.
Kuhusiana na hayo mwanashairi anasema:

---

| | |
|---|---|
| [1] Abbas Abbas | Madhlum ya Abbas |
| Natangaza waziwazi | huzuni na majonzi |
| | |
| Kumpoteza kipenzi | Abul Fadhli Abbas |
| Alipoikurubia Furati | kwa moyo wa hamasa |
| | |
| Kayachota hayo maji | kwa viganja kuyanywa |
| Kaiambia yake nafsi | simtangulie wako Imamu |
| | |
| Karibuni utayanywa | ya peponi maji matamu |
| kote kote limzingirwa | Abbas kipenzi Madhlumu |
| | |
| Wakamhujumu bila kite | wala kuonyosha huruma |
| Kiriba chake wakatoboa | na maji yake kumiminika |
| | |
| Viganja vyake wakavikata | shujaa Abbas kadhulimika |
| Kwa mishale wakamdunga | na jicho lake kulitoboa |
| | |
| Kwa nguzo walimpiga | baada ya kumvizia |
| Kaporomako kifudifudi | na mishale kuilalalia |
| | |
| Mbio Husein akamjia | mbeba bendera liyeanguka |
| Akalia kwa majonzi | kumpoteza kipenzi Abbas |

أحق الناس أن يبكى عليه * فتىً أبكى الحسين بكربلاء
أخوه و ابن والده علي * أبو الفضل المضرج بالدماء
و من واساه لا يثنيه شيء * و جاد له على عطش بماء

Mtu mwenye haki zaidi kuliliwa
Ni kijana aliyemliza Husein huko Karbala
Nduguye na mwana wa babaye Ali
Abul Fadhli aliyelowa kwa damu zake
Aliyemliwaza hakuna kitu cha kumzuia
Akamkirimu kwa maji huku kiu anacho.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Kisha Imam Husein (a.s.) aliwaita watu hao wapambane naye mmoja mmoja. Ikawa kila aliyejitokeza kupambana naye, Imam (a.s.) alimuuwa. Akawauwa watu wengi sana, na huku anasema:

القتل أولى من ركوب العار * و العار أولى من دخول النار

Kuuwawa nia bora kuliko kutenda cha aibu
Na aibu ni bora kuliko kuingia motoni.

## IMAM HUSEIN (A.S.) APAMBANA NA MAADUI MAPAMBANO MAKALI.

Mmoja kati ya wapokezi amesema: Sikuwahi kumuona mtu kamwe aliyezingirwa na watu wengi hivi na huku wameuwawa wanawe na watu wake wa nyumbani na maswahaba wake aliyekuwa na moyo shupavu kama yeye.Watu wale walikuwa wakimshambulia naye anawashambulia, wanamkimbia mfano wa mbuzi wanapokuwa wameshambuliwa na mbwa mwitu.Alikuwa akiwashambulia na hali ya kuwa ni watu zaidi ya elfu

thelathini, wanamkimbia kama nzige waliotawanyika kisha akirudi kwenye kituo chake huku akisema:

(لا حول ولا قوة إلا بالله العلي العظيم)

"Hakuna uwezo wala nguvu ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka aliye adhimu."

## **MAADUI WAMZUIA IMAM HUSEIN (A.S.) KUZIFIKIA HEMA.**

Mpokezi wa habari hizi anasema: Imam Husein (a.s.) aliendelea kupambana nao hadi wakakawa wamemzingira, akawa mbali na watu wake.Akapaza sauti na kuwaambia:

ويلكم يا شيعة آل أبي سفيان إن لم يكن لكم دين و كنتم لا تخافون المعاد فكونوا أحراراً في دنياكم هذه و ارجعوا إلى أحسابكم إن كنتم عرباً كما تزعمون

"Ole wenu enyi wafuasi wa kizazi cha Abu Sufiyan! Ikiwa nyinyi hamna dini na hamuogopi kwamba mtarudi (kwa Mwenyezi Mungu) basi kuweni watu huru katika dunia yenu hii, na zirudieni asili zenu sharifu ikiwa nyinyi ni waarabu kama mnavyodai."
Mpokezi anasema: Shimri alijibu kwa kusema: "Wasemaje, ewe mwana wa Fatima?"
Imam (a.s.) akasema: "Nasema kwamba, mimi ndiye ninayepigana nanyi, nanyi mnapigana nami, wanawake hawa hawana kosa lolote.Basi hebu wazuiyeni watu wenu hawa waovu na wajinga, wasiwasumbue mahaarimu wangu muda wote nitapokuwa niko hai."
Shimri akasema "Hilo tunakuahidi, ewe Mwana wa Fatima!"

Basi wakamuelekea ili wamshambulie, ikawa huwashambulia nao humshambulia huku akitafuta maji azime kiu alichokuwa nacho lakini alikuwa hapati.Akawa amepatwa na majeraha sabini katika mashambulizi haya. Imam (a.s.) alichoka na ikambidi asimame ili apumzike hali ya kuwa mnyonge kutokana na mapambano.
Wakati akiwa amesimama lilitupwa jiwe ambalo lilimpiga kwenye paji la uso wake.
Akachukua nguo yake kuipangusa damu iliyokuwa ikitiririka usoni, ghafla ukamjia mshale wenye sumu na wenye ncha tatu ukamchoma moyoni.Hapo Imam Husein (a.s.) akasema:

بسم الله و بالله و على ملة رسول الله (صلّى الله عليه وآله وسلّم)

“Kwa Jina la Mwenyezi Mungu na kwa Msaada wa Mwenyezi Mungu na katika Mila ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.”
Kisha akanyanyua kichwa chake juu na kusema: "EweAllah! Hakika wewe wajua ya kwamba, watu hawa wanamuuwa mtu ambaye hakuna kote ardhini Mwana wa Binti ya Mtume isipokuwa yeye.”
Kisha akaushika ule mshale na kuuchomoa kupitia mgongoni, damu nyingi ikamtoka kwa nguvu mfano wa bomba linavyotoa maji, akadhoofika sana kiasi cha kushindwa kuendelea na mapambano, akabaki amesimama. Maadui wale wakawa kila ajaye kutaka kumshambulia Imam (a.s.) humuepuka na kurudi kwa kuchelea kwamba jukumu la kumuua Imam Husein (a.s.) lisijekuwa juu yake atapokutana na Mwenyezi Mungu siku ya Qiyama.
Mwishowe akaja mtu mmoja wa mji wa Kinda aliyekuwa akiitwa Malik ibni Nasri (La’anahullah) akamtukana Imam Husein (a.s.) na kumpiga kuchwa chake kitukufu kwa upanga, ukapasua kifiniko cha kichwa cha nguo aliyokuwa

ameivaa na kumjeruhi kichwani.Kifiniko hicho kikajaa damu iliyokuwa inavuja.

Mpokezi wa habari hizi anaendelea kusema: Imam (a.s.) aliomba kitambaa ili afunge kichwa chake, kisha akaomba tena apewe kofia.Akaletewa na kuivaa, halafu juu yake akafunga kilemba chake.

Jamaa hao walikaa muda kidogo kisha wakamrudia tena Imam na kumzingira.

## KUTOKA KWA ABDULLAH IBNIL HUSEIN – KIJANA MCHANGA – NA KUFA KWAKE SHAHIDI.

(Mambo yalipofika hapa), Abdullah ibni Hasan ibni Ali (a.s.), kijana ambaye alikuwa hata bado hajafikia umri wa kubaleghe alitoka mahali walikokuwa wanawake akafanya mashambulizi hata na kuweza kusimama kando ya Imam Husein (a.s.).

Bibi Zainab bintu Ali (a.s.) akamfuata ili amzuie kwenda alikokuwa Imam Husein, lakini kijana huyo akakataa kamwe kurudi na kusema "Wallahi simuachi Ami Yangu (peke yake)."

Mara Bahri ibni Kaab, na katika mapokezi mengine wanasema Harmala ibni Kahili, akashuka kutoka kwenye farasi akiwa ameushika upanga ili kumpiga Imam Husein (a.s.), yule kijana akamwambia "Ole wako, ewe mwana wa Mwanamke khabithi! Unataka kumuuwa Ami Yangu?"

Huyu mtu alijaribu kumpiga Imam Husein (a.s.) kwa upanga wake lakini kijana huyu aliuzuia kwa mkono wake, ukamkata mkono wake ukabakia unaning'inia kwa kushikiliwa na kipande cha ngozi kilichobaki.

Kijana huyu akapiga ukelele kutokana na maumivu akisema "Ewe Ami Yangu!"

Imam Husein (a.s.) akamshika na kumkumbatia na kumwambia "Ewe mwana wa Ndugu yangu! Yavumilie

yaliyokupata na tarajia malipo mema kutokana nayo, kwani Mwenyezi Mungu atakukutanisha na Baba na Babu zako walio wema."
Mpokezi anaendelea kusema: Mara Harmala ibni Kahili (La'anahullah) akamtupia mshale kijana huyu hali akiwa amepakatwa na Imam Husein (a.s.) na kumuuwa.

## SHIMRI AZIVAMIA HEMA ZA IMAM HUSEIN (A.S.).

Kisha Shimr ibni Dhil Jaushan (la'anahullah) akaishambulia hema ya Imam Husein (a.s.) na kuipiga kwa mkuki, na kusema "Nileteeni moto niichome (hema hii) pamoja na walioko ndani yake."
Imam Husein (a.s.) akamwambia (Yabna Dhil Jaushan! Wewe ndie unaye itisha moto ili kuwachoma watu wangu wa Nyumbani!? Mwenyezi Mungu akuchome kwa moto (wake)."
Shibthi akamkaripia kutokana na maneno yake haya, akaona haya na kurudi.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AVAA NGUO ILIYORARUKA ILI ASIJE AKAPORWA AKAACHWA UCHI.

Mpokezi wa habari hizi anaendelea kusema: Baada ya hapo Imam Husein (a.s.) alisema "Nileteeni nguo isiyopendeza ili niivae chini ya nguo zangu, nisije (nikaibiwa nguo zangu) nikabakishwa uchi (baada ya kuuwawa)."
Basi akaletewa chupi akasema "La! Hayo ni mavazi ya watu walio dhalili."
Basi akaletewa nguo iliyozeeka, akaitia viraka kisha akaivaa chini ya nguo zake, lakini walipomuuwa walimvua nguo hii pia.
Kisha akaitisha suruali iliyokuwa imeshonwa kwa kitambaa kitokacho Yemeni kisha akairarua ili asivuliwe baada ya

kuuwawa.Lakini baada ya kuuwawa Bahri ibni Ka'ab (la'anahullah) alimvua na kumuacha Imam Husein (a.s.) bila mavazi.Ikawa baada ya kitendo hicho kichafu, mikono ya Bahri hukauka katika msimu wa kiangazi na kuwa kama vipande viwili vya mbao zilizokauka, na katika msimu wa kipupwe hulowana na kutokwa na damu na usaha, hata mwishowe akaangamizwa na Mwenyezi Mungu kwa adhabu hii.

## IMAM HUSEIN (A.S.) AFA SHAHIDI.

Mpokezi wa habari hizi anaendelea kusema: Baada ya Imam Husein (a.s.) kudhoofishwa na majeraha mengi aliyokuwa amepata, na baada ya mwili wake kuwa kama nungunungu kutokana na wingi wa mishale mwilini, Swalih ibni Wahab al-Mazni (la'anahullah) alimchoma kwa mkuki kiunoni. Imam Husein (a.s.) akadondoka kutoka juu ya farasi wake mpaka chini na kuanguka kwa shavu lake la kulia.Kisha akasimama (swalawatullahi aleihi).
Mpokezi anasema: Bibi Zainab bintu Ali alitoka kwenye hema huku analia na kusema, "Woi ndugu yangu!! Woi Seyyidi wangu!! Woi Ahlu Baiti wangu!! Laiti mbingu ingelianguka na kuifunika ardhi!! Laiti milima nayo ingeporomoka (kutokana na haya yaliyokufika)."
Mpokezi anasema: Shimri akawapigia kalele jamaa zake hao na kusema "Mnamchelewesha nini huyu mtu!?"
Mpokezi anasema: Basi wakamshambulia kutoka pande zote. Zar-a'h ibni Sharik (la'anahullah) akampiga kwenye bega lake la kulia, naye Imam Husein (a.s.) akampiga Zar-a'h, pigo hilo likamwangusha chini.
Naye mwingine akampiga Imam (a.s.) kwenye shingo yake tukufu kwa upanga, pigo ambalo lilimfanya kuteleza na kuanguka kifudifudi kwa uso wake.

Akiwa amechoka kutokana na mapambano alikuwa akisimama na kuteleza.
Sinan ibni Anas an-Nakha’i (la’anahullah) akaja na kumchoma kwenye mtulinga, kisha akauchomoa mkuki na kumchoma nao tena kwenye mifupa ya kifua chake.
Sinan pia akamtupia mshale ulioingia kwenye shingo yake tukufu.Imam (a.s.) akaanguka kisha akasimama na kuuvuta mshale ule na kuutoa kwenye shingo yake tukufu.Kisha akaviweka viganja vyake viwili karibu na jeraha, na kila vilipojaa kwa damu yake, aliichukua na kukipaka kichwa chake na ndevu zake na kusema “Hivi ndivyo nitakavyo kutana na Mwenyezi Mungu nikiwa nimepakwa damu (mwilini) na nikiwa nimenyang’anywa haki yaki.”
U’mar ibni Sa’ad akamwambia mtu aliyekuwa katika upande wake wa kulia “Wewe! Shuka kutoka kwenye farasi ukampumzishe Husein.”
(Kwenye upokezi mwingine imepokewa kuwa Umar ibnu Sa'ad aliwakemea majeshi wake na kusema: Shukeni mumpumzishe!!
Shimru akamkimbilia!!
Akampiga teke!!
Na kuketi juu ya kifua chake!!
Na kukikamata kidevu chake kitukufu!!
Na kumpiga kwa upanga dharuba kumi na mbili!!
Kisha akakita kichwa chake kitukufu!!
Woi Imamu wangu!! Woi Bwana wangu!!
Woi uliyechinjwa!! Woi uliyekufa mwenye kiu!!Woi Husein wangu!!)

(Na katika upokezi wa kitabu hiki anaendelea kusimulia kwa kusema.)
Khauli ibni Yazid al-Asbahi akamfwata haraka Imam Husein (a.s.) ili akikate kichwa chake, lakini akapatwa na woga akawa anatetemeka.

(Baada ya kuona hali ya Khauli) Sinan ibni Anas an-Nakha'i (la'anahullah) alishuka (kutoka kwenye farasi wake) na kumpiga Imam Husein (a.s.) kwenye koo yake tukufu, huku akisema "Wallahi! Hakika mimi ninakikata kichwa chako na huku ninanujua ya kwamba wewe ni Mwana wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na ya kwamba wewe ni Mbora wa watu wote kwa kuwa na Baba na Mama bora."
Kisha akakitaka kichwa chake kitukufu (swalallahu a'leihi wa aalih).
Mwana shairi kuhusiana na hayo anasema:

فأي رزيّة عدلت حسيناً غداة تبيره كفّا سنان

Ni msiba gani unaotoshana na msiba wa Husein
Kesho yake aliangamizwa na viganja vya Sinan.

Imepokewa kwamba huyu Sinan alichukuliwa na Mukhtar (baada ya matokeo ya Karbala) akazikata ncha za vidole vyake, moja baada ya nyingine.Kisha akaikata mikono na miguu yake, kisha akachemsha mafuta kwenye chombo kikubwa na kumtupa ndani, huku akiwa ameshachanganyikiwa.

## **MALAIKA WAANGUA KILIO BAADA YA IMAM HUSEIN (A.S.) KUFA SHAHIDI.**

Abu Twahir Muhammad ibni Husein al-Bursi amepokea riwaya katika kitabu chake
'Ma-a'limud Din kutoka kwa Imam as-Swadiq (a.s.) ya kwamba alisema "Baada ya kumfika Husein yaliyompata, Malaika walililia kwa sauti na kusema: Ewe Mola wetu! Huyu ni Husein Mteuliwa wako, Mwana wa Mteuliwa wako na wa Mwana Binti ya Mtume wako!"

(Kisha) akasema “Mwenyezi Mungu akakiweka kivuli cha al-Qaim (a.s.) mbele yao na kusema: Nitamlipizia kisasi huyu (Husein) kwa huyu (al-Qaim).”

Mpokezi wa habari hizi anasema: Katika wakati huo alipouwawa Imam Husein (a.s.) kulipanda hewani vumbi kali jeusi lenye giza na lenye upepo mwekundi ambao ilikuwa haiwezekani kuona chochote au athari yoyote ndani yake, hata wakadhani kuwa adhabu imewashukia.Wakabaki katika hali hii kwa muda, kisha vumbi likakwisha.

Naye Hilal ibni Nafii’ amepokea kwa usimulizi mwingine, anasema, “Nilipokuwa nimesimama pamoja na wafuasi wake U’mar ibni Sa’ad, mara mtu alipaza sauti na kusema “Pokea bishara njema ewe amiri! Ndiyo huyu Shimri, ameshamuuwa Husein.”

Kisha Hilal anasema “Basi nikatoka katikati ya safu za askari jeshi, na kusimama mbele yake Husein, huku anatoa pumzi zake za mwisho.Wallahi sikuwahi kumuona mtu mwenye kuuwawa aliyelowa mwili wake wote kwa damu yake, aneyependeza zaidi ya Husein, na mwenye uso wenye nuru zaidi yake.Nilishughulishwa sana na nuru ya uso wake na umbo lake lenye kupendeza kiasi cha kupotewa na fikra ya kuwa alikuwa katika hali ya kuuwawa.

Katika hali hii aliomba maji ya kunywa, nikamsikia mtu akimwambia “Wallahi! Hautayaonja maji mpaka utakapouingia (moto wa) Hamiya, utakakokunywa huko maji yake yenye kuchoma!!”

Imam Husein (a.s.) akamjibu “La, bali nitaingia kwa Babu yangu, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na kuishi naye katika pepo yake, katika makao mazuri karibu na Mfalme Mwenye Uwezo, ninywe (huko) maji yasiyoharibika na kumshtakia mliyonitendea na kunifanyia.”

Kisha Hilal anasema: Wote wakapatwa na hasira, wakawa kanakwamba Mwenyezi Mungu hakuwahi kuweka huruma

hata kidogo kwenye moyo wa yeyote kati yao.Kisha wakakikata kichwa chake Husein na hali huku anawazungumzia, nikashangazwa sana na hali yao ya kutokuwa na huruma, nikasema “Wallahi! Sitakusanyika nanyi katika jambo lolote kamwe.”

Kisha anasema: Kisha wakaanza kumpora Husein (a.s.) nguo zake alizokuwa amevaa. Is-haq ibni Hauba al-Hadhrami (la’anahullah) akachukua kanzu yake akaivaa, naye kutokana na kitendo hiki akapatwa na ukoma na nyele zake kumwagika.

Na imepokewa pia kuwa baada ya kuuwawa Imam (a.s.) kulipatikana kwenye kanzu yake alama zaidi ya mia moja na kumi za kutupiwa au kupigwa au kuchomwa (na mikuki au mishale).

Imam as-Swadiq (a.s.) anasema “ Husein(a.s.) alipatikana akiwa na majeraha thelathini na matatu ya kuchomwa (kwa mikuki na mishale) na majeraha thelathini na manne ya kupigwa (kwa mawe).”

## MAADUI WANAMPORA IMAM HUSEIN (A.S.).

Naye Bahr ibni Ka’ab at-Tamimi (la’anahullah) alizipora suruali zake Imam Husein (a.s.). Imepokewa kuwa naye (kutokana na tendo lake hili bovu) alipatwa na ugonjwa usiotibika akawa hawezi kusimama kwa miguu yake.

Naye Akhnas ibni Murthid ibni A’lqama al-Hadhrami (la’anahullah) ndiye aliyempora kilemba chake.Na inasemekana kwenye upokezi mwingine kuwa alikuwa Jabir ibni Yazid al-Audi (la’anahullah) akakivaa, naye (kutokana na tendo lake hili bovu) akapatwa na upungufu wa akili.

Naye As-wad ibni Khaalid (la’anahullah) alivipora viatu vyake.

Naye Bijdil ibni Saliim al-Kalbi (la’anahullah) ndiye aliyempora pete yake tukufu.Alikikata kidole chake Imam

(a.s.) kilichokuwa na pete, naye al-Mukhtar baada ya matokeo ya Karbala alimchukua na kuikata mikono na miguu yake na kumwacha akibingirika kwenye madamu yake hata mwishowe kuangamia.

Naye Qais ibni al-Ash-a'th (la'anahullah) akaipora nguo yake ya mahemali[1].

Naye U'mar ibni Sa'ad (la'anahullah) aliipora deraya yake iliyokuwa ikiitwa al-Batraa, lakini alipouwawa U'mar ibni Sa'ad, al-Mukhtar aliichukua na kumpa U'mra ambaye ndiye aliyemuuwa U'mar ibni Sa'ad.

Naye Jume'i ibni Khalq al-Audi (la'anahullah) ndiye aliyempora upanga wake Imam (a.s.).Na yasemekana kwenye upokezi mwingina kuwa aliyempora upanga alikuwa mtu mmoja wa Banu Tamim aliyeitwa As-wad ibni Handhala (la'anahullah).

Na katika upokezi wa Ibni Sa'ad, aliyeuchukua upanga alikuwa Falafis an-Nah-shali.Naye Muhammad ibni Zakaria ameongezea kwa kusema ya kwamba huu upanga baadaye ulianguka mikononi mwa binti ya Habib ibni Badil.

Kisha huu upanga ulioporwa sio upanga uliokuwa ukiitwa Dhul Fiqar, kwani huo ulikuwa umehifadhiwa na kuwekwa akiba katika akiba ya mabaki na kumbukumbu za Utume na Uimamu.Wapokezi wa habari hizi wamenukuu ukweli wa tuliyoyataja na kutoa picha sahihi ya tuliyoyasimulia.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Kisha alikuja mjakazi mmoja kutoka kwenye hema za Imam Husein (a.s.), mtu mmoja akamwambia "Ewe mjakazi wa Mwenyezi Mungu! Bwana wako ameshauwawa."

Mjakazi huyu anasema "Basi nikarudi haraka kwa Mabibi wangu huku ninalia kwa sauti, wakasimama mbele yangu nao pia wakapaza sauti zao kwa kilio."

[1] - Yaani velvet kwa kiingereza.

Mpokezi wa habari hizi anaendelea kusema: Hawa watu (baada ya kumuuwa Imam Husein (a.s.)) walishindana katika kuzipora hema za kizazi cha Mtume na vitulizo vya macho ya az-Zahra al-Batul, hata wakafikia kuwanyang'anya wanawake tandio zao toka begani.
Mabanati na mahramu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) wakatoka wakisaidiana katika kulia na kuomboleza kwa kuwapoteza watetezi na wapenzi wao.
Hamid ibni Muslim anasimulia kwa kusema: Nilimuona mwanamke wa Bani Bakr ibni Wa-il, aliyekuwa amekuja na mumewe, aliyekuwa katika wafuasi wa U'mar ibni Sa'ad.Huyu mwanamke alipoona kuwa watu hawa wamewashambulia wanawake waliokuwa na Husein (a.s.) kwenye hema zao na kuanza kuwapora mali yao, alichukua upanga na kusogea karibu na hema na kusema "Enyi kizazi cha Bakr ibni Wa-il! Je mnawapora mabanati wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?!Hakuna hukmu ila hukmu ya Mwenyezi Mungu! Ya lithaarati Rasulillah!! (Enyi walipiza kisasi cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu mko wapi?)"
Lakini mumewe akamchukua na kumrudisha kwenye msafara wake.

## MAADUI WAZITIA MOTO HEMA ZA IMAM HUSEIN (A.S.).

Mpokezi wa habari hizi anaendelea kusimulia: Kisha wakawatoa wanawake kwenye hema zao na kuziwasha moto, wanawake wakatoka vichwa wazi, wenye kuporwa, miguu wazi, wakilia, huku wakitembezwa kama mateka, katika udhalili.
Wakawaambia (watu hawa waliowachukua kama mateka), "Kwa haki ya Mwenyezi Mungu! Tupitishieni sehemu alikouwawa Husein (a.s.)."

Walipopitishiwa huko na kuiona miili ya wapenzi wao waliouwawa, walipaza sauti zao kwa kulia na kupiga nyuso zao.

## **BIBI ZAINAB (A.S.) AMUOMBOLEZA KWA SAUTI YENYE KUHUZUNISHA.**

Mpokezi anaendelea kusimulia: Wallahi siwezi kumsahao Zainab bintu Ali huku anamuomboleza Husein (a.s.) na kuita kwa sauti ya huzuni na moyo wenye majonzi:

يا محمداه ، صلى عليك ملائكة السماء ، هذا الحسين مرمل بالدماء ، مقطع الأعضاء ، و بناتك سبايا، إلى الله المشتكى ، و إلى محمد المصطفى ، و إلى علي المرتضى ، و إلى فاطمة الزهراء ، و إلى حمزة سيد الشهداء ، يا محمداه ، هذا حسين بالعراء ، تسفى عليه الصبا ، قتيل أولاد البغايا ، وا حزناه ، وا كرباه ، اليوم مات جدي رسول الله (صلّى الله عليه وآله وسلّم) ، يا أصحاب محمداه ، هؤلاء ذرية المصطفى يساقون سوق السبايا

“Woi Muhammad wangu! Mfalme wa binguni akuteremshia rehma yake!Huyu ni Husein chini ya mbingu, aliyepakwa mwili wote kwa mchanga na damu yake, aliyekatwakatwa viungo vyake.Waa thaklaah!(woi tumefelewa!) mabanati zako wamekuwa mateka.Kwa Mwenyezi Mungu tunashitakia, na kwa Muhammad al-Mustwafa na kwa Ali al-Murtadha na kwa Fatima az-Zahra na kwa Hamza Seyyidush Shuhada.
Woi Muhammad wangu! Huyu ni Husein chini ya mbingu, mwili unapeperushiwa mavumbi na Upepo wa mashariki, ameuwawa na wana wa makahaba.

Woi huzuni! Woi majonzi kwa ajili yako, ewe Aba A’bdillah! Leo hii amekufa Babu yangu, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).
Enyi wafuasi wa Muhammad, hawa ni Kizazi cha al-Mustwafa, wanaopelekwa kama mateka.”

Na katika baadhi ya riwaya nyinginezo alisema:

يا محمداه ، بناتك سبايا ، و ذريتك مُقتلة ، تسفى عليهم ريح الصبا ، و هذا حسين محزوز الرأس من القفا ، مسلوب العمامة و الرداء ، بأبي من أضحى عسكره في يوم الاثنين نهبا ، بأبي من فسطاطه مقطع العرى ، بأبي من لا غائب فيرتجى ، و لا جريح فيداوى ، بأبي من نفسي له الفداء ، بأبي المهموم حتى قضى ، بأبي العطشان حتى مضى ، بأبي من شيبته تقطر بالدماء ، بأبي من جده محمد المصطفى ، بأبي من جده رسول إله السماء ، بأبي من هو سبط نبي الهدى ، بأبي محمد المصطفى ، بأبي خديجة الكبرى ، بأبي علي المرتضى (عليه السلام) ، بأبي فاطمة الزهراء سيدة النساء ، بأبي من ردت له الشمس حتى صلى

Woi Muhammad wangu! Mabanati wako wamefanywa kuwa mateka, na kizazi chako kimeuwawa, upepo wa mashariki unaipiga miili yao kwa mavumbi, na huyu ni Husein aliyekatwa kichwa chake kwa kwa kupitia kishogo, aliyeporwa kilemba na nguo zake.
Baba yangu awe fidia kwa ambaye kulikucha siku ya juma tatu askari wake wakiwa wameporwa! Baba yangu awe fidia kwa ambaye hema yake imekatwa vitanzi vyake! Baba yanguawe fidia kwa ambaye hajaghibu ili atarajiwe kurudi, wala sio majeruhi ili aweze kutibiwa kwa dawa! Baba yangu awe fidia kwa ambaye nafsi yangu ni fidia kwake! Baba yangu awe fidia kwa ambaye alijawa na huzuni hadi akafariki! Baba yangu awe fidia kwa ambaye alipatwa na kiu

hadi akafiriki! Baba yangu awe fidia kwa ambaye ndevu zake zinatirikwa na damu (zake)! Baba yangu awe fidia kwa ambaye Babu yake ni Muhammad al-Mustwafa! Baba yangu awe fidia kwa ambaye Babu yake ni Mjumbe wa Mungu wa mbingu! Baba yangu awe fidia kwa ambaye ni Mjukuu wa Mtume wa uongofu! Baba yangu awe fidia kwa ajili yake Muhammad al-Mustwafa! Baba yangu awe fidia kwa ajili yake Khadija al-Kubra! Baba yangu awe fidia kwa ajili yake Ali al-Murtadhwa! Baba yangu awe fidia kwa ajili yake Fatima az-Zahra Bibi wa wanawake wa Peponi! Baba yangu awe fidia kwa ambaye jua lilirudishwa kwa ajili yake (baada ya kuzama) hata akaweza kuswali."

Mpokezi anasema: Wallahi! Aliwafanya wote kulia, maadui na marafiki.

## BI SUKEINA (A.S.) AUKUMBATIA MWILI WA IMAM HUSEIN (A.S.).

Kisha Bi Sakina aliukumbatia mwili wa Imam Husein (a.s.), lakini wakakusanyika baadhi ya mabedui wa kiarabu na kumvuta kutoka hapo.

## WALIMKANYAGAKANYAGA MGONGONI IMAM HUSEIN (A.S.) KWA FARASI.

Mpokezi anaendelea kuelezea: Kisha U'mar ibni Sa'ad aliwaita wafuasi wake kwa sauti na kusema, "Ni nani atakaye jitolea kwenda kwa Husein, na kumkanyagakanyaga mgongoni kwa farasi?"
Watu kumi kati yao wakajitolea, nao ni Is-haq ibni Hauba aliyempora Imam Husein (a.s.) kanzu yake, na Akhnas ibni Murthid, na Hakiim ibni Tufeil as-Subei'i, na U'mar ibni Subeih as-Swaidawi, na Rajaa ibni Munqidhi al-A'bdi, na

Saalim ibni Khaithama al-Ju'ufi, na Swalih ibni Wahab al-Ju'ufi, na Waahidh ibni Ghaanim, na Haani ibni Thabiit al-Hadhrami, na Usaid ibni Maalik (la'anahumullah), Wakamkanyagakanyaga Imam Husein (a.s.) kwa kwato za farasi zao hadi kuuponda mgongo wake na kifua chake.
Mpokezi anasema: Kisha wale watu kumi walikuja na kusimama mbele yake Ibnu Ziyad (la'anahullah).Useid ibni Maalik aliyekuwa miongoni mwa wale kumi, akasema:

نحن رضضنا الصدر بعد الظهر بكل يعبوب شديد الأسر

Sisi tumekipondaponda kifua baada ya mgongo
Kwa mbubujiko wenye nguvu nyingi.

Ibnu Ziyad (la'anahullah) akawaambia "Nyinyi ni akina nani?"
Wakajibu, "Sisi ndio ambao tulioupondaponda mgongo wa Husein kwa farasi wetu hadi kuvisaga vikoromeo vya kifua chake."
Mpokezi anasema: Basi akaamrisha kuwa wapewe zawadi kidogo (kwa kitendo chao hicho).
Abu U'mar az-Zahid anasema "Tulipochunguza kuwahusu watu hawa kumi tulipata kuwa wote walikuwa watoto wa zina."
Watu hawa (baada ya matukio ya Karbala) Mukhtar aliwachukua na kuifunga mikono na miguu yao kwa vipande vya vyuma, kisha kuwapondaponda migongo ya kwa farasi hadi wakaangamia.

## MTU KATIKA JESHI LA IBNI SA'AD AMUONA MTUME (S.A.W.A.) KWENYE NDOTO NA MTUME

## **KUMPAKA KWENYE MACHO YAKE WANJA WA DAMU KISHA KUAMKA AKIWA AMEPOFUKA.**

Naye Ibni Rabaah amesema “Nilikutana na mtu kipofu aliyekuwa ameshudia mauwaji ya Husein (a.s.), akaulizwa sababu ya kupofuka kwake, akajibu: Nilishudia mauwaji yake, nikiwa wa kumi kati ya watu kumi, lakini mimi sikudunga (kwa mkuki) wala kupiga (kwa upanga) wala kutupa (mshale).Baada ya kuuwawa, nilirudi nyumbani kwangu nikaswali swala ya Ishaa na kulala.Akanijia mtu kwenye ndoto na kusema: Mjibu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (swallalahu aleihi wa aalihi wa sallam).Nikajibu: Nina nini naye?

Akaukamata ukosi wa shingo yangu na kuniburuta hadi alikokuwa Mtume (s.a.w.w.), nikamkuta Mtume (s.a.w.w.) akiwa ameketi jangwani huku ameuwacha mkono wake wazi hadi kwenye kiwiko, na huku ameushika mkuki mdogo, na Malaika amesimama mbele yake, mkononi mwake akiwa na upanga wa moto, huku anawauwa wenzangu wale tisa, kila alipopiga pigo nafsi zao zilitokwa miali ya moto.

Basi nikamkurubia na kupiga magoti mbele yake, na kusema: As-Salaamu a’leika ya Rasulallah, (amani ya Mwemyezi Mungu iwe juu yako, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu), lakini hakunijibu.Akabaki kimya kwa muda mrefu, kisha akakiinua kichwa chake, na kusema: Ewe adui wa Mwenyezi Mungu! Umevunja heshima yangu na kukiuwa kizazi changu, na wala hukuichunga haki yangu, bali ulifanya ulivyofanya.

Nikasema: Ya Rasulallah! Wallahi sikupiga kwa upanga wala kudunga kwa mkuki wala kutupa mshale.

Akanijibu: Lakini uliongeza idadi yao.Njoo karibu nami. Nikasonga karibu naye, mara nikaona bakuli iliyojaa damu, akaniambia: Hii ni damu ya Mwanangu Husein (a.s.).

Kisha akanipaka macho kwa damu hiyo, nikagutuka kutoka usingizini na mpaka sasa sioni chochote.

## KATIKA SIKU YA QIYAMA BIBI FATIMA (A.S.) ATAWEKEWA HEMA YA NURU AMBAPO ATATAKA KISASI CHA IMAM HUSEIN (A.S.) KULIPIZIWA KUTOKA KWA WAUWAJI WAKE.

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Swadiq (a.s.) kwa sanadi marfu'u (ambayo haikutajwa silsila yote ya wapokezi) kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) ya kwamba alisema "Itakapokuwa siku ya Qiyama, Fatima (a.s.) atawekewa hema ya nuru, kisha atakuja Husein (a.s.) huku kichwa chake kiko mkononi mwake.Fatima (a.s.) atakapomwona atapiga ukulele kwa kulia, ambao kutokana nao hatabaki Malaika Muqarrab wala Nabi Mursal katika kikundi hicho ila tu atalia kwa kuona kilio chake.Kisha Mwenyezi Mungu Azza wa Jalla ataweka mfano wake Husein mbele ya Fatima akiwa mwenye sura nzuri kabisa, huku akigombezana bila kichwa na waliomuuwa.Kisha Mwenyezi Mungu atanikusanyia wauwaji wake na waliotayarisha mambo dhidi yake na walioshiriki katika kuimwaga damu yake, kisha nitawauwa mmoja mmoja hadi kumfikia wa mwisho wao.Kisha watafufuliwa, kisha Amirul muumini (a.s.) atawauwa.Kisha watafufuliwa, kisha Hasan (a.s.) atawauwa.Kisha watafufuliwa, kisha Husein (a.s.) atawauwa.Kisha watafufuliwa, na hatabaki katika kizazi changu yeyote ila tu atawauwa, na wakati huo ndipo hasira itamalizwa na huzuni kusahaolika."

Kisha Imam as-Swadiq (a.s.) akasema, "Mwenyezi Mungu awarehemu mashia wetu.Hao wallahi ndio waumini, na ndio waliotushiriki katika msiba kwa wingi wa huzuni na kuhasirika."

Imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) ya kwamba amesema, “Itakapokuwa siku ya Qiyama, Fatima (a.s.) atakuja katika kikundi cha wanawake wenzake, kisha ataambiwa: Ingia Peponi.
Naye atasema: Sitongia hadi nitakapojua alichofanyiwa mwanangu baada yangu.
Naye ataambiwa: Hebu angalia katikati ya Qiyama. (Atakapoangalia) atamuona Husein (a.s.) huku akiwa hana kichwa, kisha atapaza sauti ya kili, nami nitapaza sauti ya kilio kutokana na kilio chake, nao Malaika vilevile watapiga ukulele wa kilio kutokana na kilio chake.”
Katika riwaya nyingine imepokewa kuwa alisema, “Kisha (Bibi Fatima (a.s.)) ataita kwa sauti: Woi Mwanangu! Woi Tunda la moyo wangu!”
Imam as-Swadiq (a.s.) anaendelea kusema, “Na hapo Mwenyezi Mungu atadhihirisha ghadhabu kwa (uchungu alio nao) Fatima, na kuuamuru Moto unaoitwa Hab-hab, uliowashwa kwa muda wa miaka elfu hadi ukawa mweusi, haupatwi na furaha kamwe wala hautokwi na ghamu kamwe. Kisha utaambiwa: Wachukue wauwaji wa Husein (a.s.). Basi Moto utawachukua, nao watakapofika kwenye umio wake Moto huo, utatoa ukulele kama wa farasi, nao pia watatoa pamoja na Moto ukulele kama huo. Kisha utatoa ukulele kama anayetoa pumzi kwa nguvu, nao pia watatoa pumzi kwa nguvu pamoja na Moto. Kisha utatoa ukulele kama anayevuta pumzi ndani kwa nguvu, nao pia watavuta pumzi kwa nguvu pamoja na Moto.
Kisha watazungumza kwa ndimi kali zenye kutamka kwa ufasaha: Ewe Mola wetu! Mbona umetuwajibishia (adhabu ya) Moto kabla ya kuwaadhibu wanaoabudu masanamu? Halafu jawabu litawajia kutoka kwa Mwenyezi Mungu Azza wa Jallah: Anayejua sio kama asiyejua.”
Ibni Babaweihi amezitaja hadithi hizi mbili katika kitabu chake ‘I’qabul a’amal’.

# MLANGO WA TATU.

# MAMBO YALIYOJIRI BAADA YA KUUWAWA KWA IMAM HUSEIN (A.S.)

## MAMBO YALIYOJIRI BAADA YA KUUWAWA KWA IMAM HUSEIN (A.S.)

Tuliyoyataja hapa ni yote yaliyojiri baada ya kuuwawa kwa Imam (a.s.).

## UMAR IBNU SA'AD AMTUMIA IBNU ZIYAD KICHWA CHA IMAM HUSEIN (A.S.) PAMOJA NA VICHWA VYA MASHAHID WENGINEO.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Kisha U'mar ibni Sa'ad (la'anahullah) alikituma kichwa cha Imam Husein (a.s.) katika siku hiyo ya A'shura, pamoja Khauli ibni Yazid al-Asbahi na Hamid ibni Muslim al-Azdi kumpelekea U'beidullah ibni Ziyad, na akaamrisha pia vichwa vya wengineo, katika maswahaba wake na watu wake wa nyumbani, vikatwe.Vikakatwa na kuvituma pamoja na Shimr ibni Dhil Jaushan (la'anahullah) na Qais ibnil Ash-ath na U'mar ibnil Hajjaj, wakaenda navyo hadi mji wa al-Kufa.

## IBNU SA'AD AWABEBA AYALI WA IMAM HUSEIN (A.S.) NA KUWAPELEKA KWA IBNU ZIYAD.

Ibnu Sa'ad alibaki huko Karbala siku hiyo na siku iliyofwata hadi adhuhuri, kisha akaondoka pamoja na waliobaki katika ayali wake Imam Husein (a.s.).
Akawabeba wanawake kwa ngamia kwa kuwaweka juu ya saruji za ngamia bila tandiko za kukalia wala kitu cha kujifinikiza, nyuso zao zikiwa wazi mbele ya maadui, na hali ya kuwa wao ni amana ya Mbora wa Mitume (s.a.w.a.) aliyowaachia waislamu.Kisha wakawavuta kama wanavyo vutwa mateka wa Uturuki na Roma, wakafanywa mateka katika uzito wa misiba na majonzi.
Ameswibu kweli aliyesema:

يصلى على المبعوث من آل هاشم      و يغزى بنوه أن ذا لعجيب

Anaswaliwa Mtume wa Aali Hashimi
Huku wanawe wavamiwa.Ajabu kweli.

Naye mwengine amesema:

أ ترجو أمة قتلت حسينا      شفاعة جده يوم الحساب

Je, unataraji umma uliomuuwa Huseini
Uombezi wa Babu yake siku ya hesabu.

## MAKABILA YANAGAWANA VICHWA ILI KUMPELEKEA IBNU ZIYAD.

Imepokewa kuwa vichwa vya maswahaba wa Imam Husein (a.s.) vilikuwa vichwa sabini na nane, makabila yale yakagawana baina yao vichwa hivi ili kujikurubisha kwa U'beidullah ibni Ziyad na kwa Yazid ibni Mua'wiya.
Kabila la Kinda likaja na vichwa kumi na vitatu, kiongozi wao akiwa Qais ibnil Ash-a'th.
Nalo kabila la Hawazin likaja na vichwa kumi na viwili, kiongozi wao akiwa ni Shimr ibni Dhil Jaushan.
Nalo kabila la Tamim likaja na vichwa kumi na saba.
Banu Asad wakaja na vichwa kumi na sita.
Nao Madh-haj wakaja na vichwa saba.
Nao watu waliobaki walikuja na vichwa kumi na vitatu.

## WATU KATIKA KABILA LA BANI ASAD WAIZIKA MIILI YA MASHAHIDI.

Mpokezi anasema: Ibnu Sa'ad alipoondoka Karbala, walikuja watu wa kabila la Banu Asad, wakaiswalia hiyo miili toharifu iliyopakwa kwa mchanga na damu na kuizika kwa hali tunayoiona hivi leo. Naye Ibnu Sa'ad aliondoka na mateka tuliowataja, na walipoikaribia al-Kufa watu wa mji huo walikusanyika ili kuwatazama.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Mwanamke mmoja wa al-Kufa akiwa juu ya dari aliwazungumzia na kusema, "Nyinyi ni mateka wa kutoka wapi?"

Wakajibu, "Sisi ni mateka wa aali Muhammad (s.a.w.w.)"

Mwanamke huyu alishuka kutoka kwenye dari ya nyumba yake na kukusanya tandio, vikoi na shungi na kuwaletea hawa mabibi watukufu, wakajisitiri nazo.

## MIONGONI MWA MATEKA ALIKUWA IMAM SAJJAD (A.S.) NA HASAN ALMUTHANNA NA ZAID NA AMRU.

Mpokezi anaendelea kusimulia: Vile vile pamoja na wanawake alikuweko Imam Ali ibni Husein (a.s.), aliyekuwa amezidiwa na ugonjwa, na Hasan al-Muthanna aliyekuwa amemtetea Ami yake na Imamu wake kwa kustahamili machungu ya mikuki, na alikuwa karibu kukata roho baada ya kuwa amejeruhiwa sana.

Mwandishi wa kitabu 'al-Maswabih' anasimulia ya kwamba al-Hasan ibnil Hasan al-Muthanna alipigana mbele ya ami yake, na kuwauwa al-Husein (a.s.) katrika siku hiyo na kuwauwa watu kumi na saba, na kupatwa na majeraha kumi na nane na kuanguka, kisha alichukuliwa na mjomba wake Asmaa ibnu Kharija akampeleka mji wa al-Kufa na kumtibu hadi akapona, kisha akampeleka Madina.

Vile vile walikuwa pamoja nao Zaid na A’mru wana wa Imam Hasan (a.s.) Mjukuu wa Mtume (s.a.w.w.).
Baada ya kuwatambua hawa ni akina nani, watu wa al-Kufa walianza kuomboleza na kulia.
Imam Ali ibnil Husein (a.s.) akawaambia, “Je, mnaomboleza na kulia kwa ajili yetu?!! Basi ni nani aliyetuuwa?!!”

**KHUTBA YA BIBI ZAINAB (A.S.) ALIPOINGIA MJI WA AL-KUFA.**

Bashir ibni Khuzaim al-Asadi anasema, “Nilimwangalia Zainab bintu Ali (a.s.) siku hiyo, sikuwahi kumwona kamwe mwanamke mwenye ufasaha zaidi yake, alikuwa kana kwamba anazungumza kwa ulimi wa Amirul Muumini (a.s.).Baada ya kuwaashiria watu kuwa wanyamaze, watu walirudisha pumzi zao na kengele zikatulia, kisha akasema:

الحمد لله و الصلاة على أبي محمد و آله الطيبين الأخيار أما بعد يا أهل الكوفة يا أهل الختل و الغدر أ تبكون فلا رقات الدمعة و لا هدأت الرنة إنما مثلكم كمثل التي نقضت غزلها من بعد قوة أنكاثا تتخذون أيمانكم دخلا بينكم؟ ألا و هل فيكم إلا الصلف و النطف و الصدر الشنف و ملق الإماء و غمز الأعداء أو كمرعى على دمنة أو كفضة على ملحودة ألا ساء ما قدمت لكم أنفسكم أن سخط الله عليكم و في العذاب أنتم خالدون.

أ تبكون و تنتحبون؟ إي و الله فابكوا كثيرا و اضحكوا قليلا فلقد ذهبتم بعارها و شنارها و لن ترحضوها بغسل بعدها أبدا و أنّى ترحضون قتل سليل خاتم النبوة و معدن الرسالة و سيد شباب أهل الجنة و ملاذ خيرتكم و مفزع نازلتكم و منار حجتكم و مدرة سنتكم ألا ساء ما تزرون و بعدا لكم و سحقا فلقد خاب السعي و تبت الأيدي و خسرت الصفقة و بؤتم بغضب من الله و ضربت عليكم الذلة و المسكنة. ويلكم يا أهل الكوفة أ تدرون أي كبد لرسول الله فريتم و

أي كريمة له أبرزتم و أي دم له سفكتم و أي حرمة له انتهكتم و لقد جئتم بها صلعاء عنقاء سواء فقماء.
و في بعضها خرقاء شوهاء كطلاع الأرض أو ملاء السماء أ فعجبتم إن مطرت السماء دما و لعذاب الآخرة أخزى و أنتم لا تنصرون فلا يستخفنكم المهل فإنه لا يحفزه البدار و لا يخاف فوت الثأر و إن ربكم لبالمرصاد.

"Himidi zote njema ni za Mwenyezi Mungu, na Rehma zimshukie Babu yangu pamoja na Aali zake Wazuri Waliowema.
Ama baadu, enyi watu wa al-Kufa! Enyi watu wa hila na khiana! Eti mnalia? Basi machozi yasikome kutiririka, wala sauti zisitulie.
Kwa hakika mfano wenu ni mfano wa mwanamke aliyekata uzi wake vipande vipande, baada ya kuusokota kuwa mgumu, mnavifanya viapo vyenu kuwa ni njia ya kudanganyana kati yenu.
Bali, je kati yenu kuna kitu ila kujigamba na ufisadi, na kifua chenye chuki, na kujipendekeza kama wafanyavyo wajakazi, na kukonyezea kwa maadui! Au kama malisho kwenye sehemu chafu za takani, au kama fedha (zilizowekwa) juu ya kaburi (ili kuipamba).Tambeuni wazi kuwa ni mabaya yaliyotangulizwa na nafsi zenu kwa kumfanya Mwenyezi Mungu akawakasirikia na (hakika) katika adhabu mtabaki milele.
Eti mnalia na kuomboleza? Naam, wallahi! Basi lieni sana na chekeni kidogo, kwani kwa hakika mmeibeba aibu yake na fedheha yake, na wala hamtoweza kamwe baada yake kuisafisha.Na mtawezaje kuyasafisha mauaji ya kizazi cha Mwisho wa Utume, na mahala pa kushukia Ujumbe (wa Mwenyezi Mungu) na Bwana wa vijana wa Peponi, na makimbilio ya wema wenu, na mwenye kuwaondolea misiba

yenu, na mahala zinapopata nuru hoja zenu, na sababu ya kuzidi kwa rizki katika mwaka wenu.

Tambueni kuwa ni mabaya sana mliyoyabeba.Muangamizwe na kutupwa mbali.Juhudi (zenu) zimepotea , na mikono (yenu) imeangami na biashara yeni imepata hasara, na mumerudi na ghadhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na ukapigwa juu yenu udhalili na umaskini.

Ole wenu enyi watu wa al-Kufa! Je, mnajua ni ini lipi la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, mmelipasua, na Binti yupi wake mliyetoa kwenye sitara, na damu ipi yake mliyoimwaga, na ni heshima ipi yake mliyoivunja?! Kwa hakika mumekitenda (kitenda hiki) cha ujinga kisicho kuwa na asili, kiovu, chenye kujaa shari."

Na kwenye upokezi mwingine, "(kitenda hiki) chenye (sura ya) kuchukiza yenye kupenyeza kote kuenea kwa ardhi na mbingu.Basi je mlishangazwa kwamba mbingu ilinyesha damu, na kwa hakika adhabu ya akhera ni yenye balaa zaidi, nanyi hamnusuriwa.Basi kupewa muhula kusiwafanye kuyaona mambo kuwa mepesi, kwani Yeye hana kinachomharakisha, wala haogopi kuwa atashindwa kulipiza kisasi, na kwa hakika Mola wenu ni Mwenye kuvizia."

Mpokezi anasema: Basi wallahi, niliwaona watu siku hiyo wakiwa wametahayari, wakilia huku wameiwekelea mikono yao kwenye midomo yao.

Na nilimuona mzee mmoja ambaye alikuwa amesimama kando yangu, aliyekuwa akilia mpaka ndevu zake zikawa zimelowa na huku anasema, "Baba yangu na mama yangu wawe fidia kwa ajili yenu.Wazee wenu ndio wazee bora, na vijana wenu ndio vijana bora, na wanawake wenu ndio wanawake bora, na kizazi chenu ndicho kizazi bora, hakipatwi na udhalili wala udhaifu.

**KHUTBA YA BIBI FATIMA AS-SWAGHIRA (A.S.).**

Naye Zaid ibnu Musa amepokea habari hizi kwa kusema: Baba yangu alinihadithia kutoka kwa Babu yake (aleihimas salaam) ya kwamba alisema, “Fatima as-Sughra (a.s.) alikhutubia baada ya kuingia kutoka Karbala, na kusema:

الحمد لله عدد الرمل و الحصى و زنة العرش إلى الثرى أحمده و أومن به و أتوكل عليه و أشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له و أن محمدا عبده و رسوله (صلّى الله عليه وآله وسلّم) و أن أولاده ذبحوا بشط الفرات بغير ذحل و لا ترات اللهم إني أعوذ بك أن أفتري عليك الكذب أو أن أقول عليك خلاف ما أنزلت عليه من أخذ العهود لوصية علي بن أبي طالب (عليه السلام) المسلوب حقه المقتول من غير ذنب -كما قتل ولده بالأمس- في بيت من بيوت الله فيه معشر مسلمة بألسنتهم تعسا لرءوسهم ما دفعت عنه ضيما في حياته و لا عند مماته حتى قبضته إليك محمود النقيبة طيب العريكة معروف المناقب مشهور المذاهب لم تأخذه اللهم فيك لومة لائم و لا عذل عاذل هديته اللهم للإسلام صغيرا و حمدت مناقبة كبيرا و لم يزل ناصحا لك و لرسولك حتى قبضته إليك زاهدا في الدنيا غير حريص عليها راغبا في الآخرة مجاهدا لك في سبيلك رضيته فاخترته فهديته إلى صراط مستقيم أما بعد يا أهل الكوفة يا أهل المكر و الغدر و الخيلاء فإنا أهل بيت ابتلانا الله بكم و ابتلاكم بنا فجعل بلاءنا حسنا و جعل علمه عندنا و فهمه لدينا فنحن عيبة علمه و وعاء فهمه و حكمته و حجته على الأرض في بلاده لعباده أكرمنا الله بكرامته و فضلنا بنبيه محمد (صلّى الله عليه وآله وسلّم) على كثير ممن خلق تفضيلا بينا فكذبتمونا و كفرتمونا و رأيتم قتالنا حلالا و أموالنا نهبا كأننا أولاد ترك و كابل كما قتلتم جدنا بالأمس و سيوفكم تقطر من دمائنا أهل البيت لحقد متقدم قرت لذلك عيونكم و فرحت قلوبكم افتراء على الله و مكرا مكرتم و الله خير الماكرين فلا تدعونكم أنفسكم إلى الجذل بما أصبتم من دمائنا و نالت أيديكم من أموالنا فإن ما أصابنا من

المصائب الجليلة و الرزايا العظيمة في كتاب من قبل أن نبرأها إن ذلك على الله يسير لكيلا تأسوا على ما فاتكم و لا تفرحوا بما آتاكم و الله لا يحب كل مختال فخور تبا لكم فانتظروا اللعنة و العذاب فكان قد حل بكم و تواترت من السماء نقمات فيسحتكم بعذاب و يذيق بعضكم بأس بعض ثم تخلدون في العذاب الأليم يوم القيامة بما ظلمتمونا ألا لعنة الله على الظالمين ويلكم أ تدرون أية يد طاغتنا منكم و أية نفس نزعت إلى قتالنا أم بأية رجل مشيتم إلينا تبغون محاربتنا و الله قست قلوبكم و غلظت أكبادكم و طبع على أفئدتكم و ختم على سمعكم و بصركم و سول لكم الشيطان و أملى لكم و جعل على بصركم غشاوة فأنتم لا تهتدون فتبا لكم يا أهل الكوفة أي ترات لرسول الله (صلّى الله عليه وآله وسلّم) قبلكم و دخول له لديكم بما عاندتم بأخيه علي بن أبي طالب جدي و بنيه و عترته الطيبين الأخيار فافتخر بذلك مفتخر و قال:

نحن قتلنا عليا و بني علي *** بسيوف هندية و رماح

و سبينا نساءهم سبى ترك *** و نطحناهم فأي نطاح

بفيك أيها القائل الكثكث و الأثلب افتخرت بقتل قوم زكاهم الله و طهرهم الله و أذهب عنهم الرجس فأكظم و أقع كما أقعى أبوك فإنما لكل امرئ ما كسب و ما قدمت يداه أ حسدتمونا ويلا لكم على ما فضلنا الله .

**فما ذنبنا إن جاش دهرا بحورنا *** و بحرك ساج ما يواري الدعامصا**

ذلك فضل الله يؤتيه من يشاء و الله ذو الفضل العظيم و من لم يجعل الله له نورا فما له من نور.

Alhamdulillahi kwa idadi ya ramli na changarawe, na kwa wizani wa arshi yake na ardhi.Ninamhimidi na kumuamini na kumtegemea, na ninashuhudia ya kwamba hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah, wa pekee

asiyekuwa na mshirika, na ya kwamba Muhammad (s.a.w.w.) ni Mja wake na Mjumbe wake, na ya kwamba Dhuria wake walichinjwa kwenye ufuo wa al-Furat bila ya kuwepo na chuki (hapo kati) wala (kuwa wana) kisasi (cha kulipa).

Ewe Allah! Hakika mimi ninajilinda kwako nisije nikazusha uongo juu yako, au nikasema kukuhusu kinyume cha yale uliyoyateremsha na kuchukua ahadi (kutoka kwa waislamu) kwa wasiya (wa Mtume kumteuwa) Ali ibni Abi Twalib (a.s.) aliyenyang'nywa haki yake, aliye uwawa bila dhambi yoyote- kama alivyo uwawa Mwanawe hapo jana- ndani ya nyumba katika nyumba za Mwenyezi Mungu[1], na huku kuna kikundi cha waislamu wenye (kudai ni waislamu kwa) ndimi zao, vichwa vyao na viangamizwe!! Hawakumwepushia dhulma katika uhai wake wala katika wakati wa kufa kwake, hadi ukamrudisha kwako akiwa mwenye nafsi yenye kuhimidika, mwenye tabia njema, mwenye sifa zilizo maarufu, mielekeo iliyomashuhuri.Ewe Allah, hakujali kwa ajili yako lawama ya mwenye kulaumu, wala kemeo la mwenye kukemea.

Ulimwongoza, Ee Mola wangu, kwenye uislamu tangu akiwa mchanga, na ukamadihi sifa zake katika ukubwani. Hakuacha kutoa nasaha kwa ajili yako na Mjumbe wako (rehma yako imshukie pamoja na Aali zake) hadi ulipomrudisha kwako, akiwa mwenye kuifanyia dunia zuhudi, bila kuwa na pupa nayo, bali hamu yake ni Akhera, mwenye kupigana jihadi kwenye njia yako kwa ajili yako.Ulimridhia ukamchagua, na ukamwongoza kwenye njia iliyonyooka.

Ama baadu, enyi watu wa al-Kufa, enyi watu wa njama na khiana na kiburi.Kwa hakika sisi ni Ahlu Baiti, Mwenyezi Mungu ametufanyia mtihani kwa kupitia kwenu, na kuwafanyia nyinyi mtihani kwa kutupitia sisi, na ameijaalia

---

[1]Imam  Ali ibni Abi Twalib (a.s.) aliuwawa ndani ya Kaaba.

balaa yetu kuwa balaa njema, na ameijaalia elimu yake kuwa kwetu, na fahamu iwe kwetu, basi tukawa sisi ndio Mahala pa elimu yake, na chombo kibebacho fahamu ya elimu yake na chombo cha elimu yake na hujja yake juu ya ardhi katika nchi zake kwa waja wake.Mwenyezi Mungu ametukirimu kwa karama yake, na kutufadhilisha kwa Mtume wake, Muhammad (s.a.w.w.) juu ya wengi miongoni mwa viumbe wake, kwa fadhila iliyowazi.

Lakini nyinyi mumetukadhibisha na kutukufurisha, na kuona kuwa kupigana nasi ni halali, na mali yetu inajuzu kuporwa, kana kwamba sisi ni wana wa Uturuki au Kabul.Kama mlivio muuwa Babu yetu hapo jana, na mapanga yenu yangali yanatona kutokana na damu zetu (mlizomwaga) kutokana na chuki ya tangu (mliyokuwa nayo) mkajituliza macho yenu kwa kitendo hicho, na nyoyo zenu zikafurahia, kwa kumzulia Mwenyezi Mungu, na kwa njama mliyoipanga, (lakini) Mwenyezi Mungu ni Mbora wa wenye kupanga njama.

Basi nafsi zenu zisiwaite kuyafurahia mliyozifanyia damu zetu na mliyoyachukua kwa mikono yenu katika mali zetu, kwani misiba mikubwa na maafa makubwa yaliyotupata yameandikwa kwenye Kitabu (cha Mwenyezi Mungu) (Kabla ya Sisi kuyafanya kuhakikika, hakika hilo kwa Mwenyezi Mungu ni jepesi, ili msije mkasikitishwa kwa lile mlilokosa wala mkafurahi kwa kile mlichopewa.Na kwa hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila mwenye kiburi, mwenye kujifakhiri.)

Ole wenu!!Ingojeni laana na adhabu, bali ni kana kwamba imeshawafikia, na zimefululizana ghadhabu kutoka mbinguni, ili awaangamize kwa adhabu, na wengine kati yenu wawaonjeshe wengineo makali yao, kisha muishi milele katika adhabu iliyo kali siku ya Qiyama kwa ajili ya mlivyo tudhulumu.Tambueni kuwa laana ya Mwenyezi Mungu itawafikie walio madhalimu.

Ole wenu, je mnajua ni mkono upi kati yenu uliotudunga?! Na ni nafsi ipi iliyotoka kupigana nasi?! Au ni pamoja na mguu upi mlikuja mkitaka kupigana vita nasi?!
Wallahi nyoyo zenu zimekuwa sugu, na maini yenu yamekauka[1], nyoyo zenu zimewekewa kizuizi, na masikio na macho yenu yamepigwa muhuri, naye shetani amewahadaa na kuwaamuru na kuwawekea kwenye macho yenu kizuizi, hivyo basi hamuongoki.
Muaangamizwe (na Mwenyezi Mungu) enyi watu wa al-Kufa!Ni kisasi gani ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kabla yenu, na chuki ipi mliyonayo ya kumchukia, ikawafanya kumfanyia inadi ndugu yake, (yaani) Ali ibni Abi Twalib (a.s.) Babu yangu, na (mkawafanyia) wanawe na Kizazi Kitukufu cha Mtume (swalawatullahi wa salamuhu aleihim), kisha akajifakhiri mwenye kujifakhiri kati yenu kwa kusema:

Sisi tulimuuwa Ali na wanawe Ali
kwa mapanga toka India na mikuki
Tuliteka wanake zao kama waturuki
na tukawapiga, kupiga aina gani?

Mdomo wako ujazwe mawe na mchanga !!, umejifakhiri kwa kuwauwa watu ambao Mwenyezi Mungu amewatakasa na kuwaondolea uchafu, na kuwatakasa mtakaso mkuu, basi nyamaza na ufunge kidomo chako kama alivyofunga babako kidomo chake, kwani kila mtu atalipwa kile alichokichuma na yalichokitanguliza mikono yake.
Je mumetuhusudu –ole wenu- kwa kile Mwenyezi Mungu ametufadhilisha kwacho?

[1] Yaani, mmetokwa na huruma kabisa.

**Shairi:**

Basi nini dhambi yetu ikiwa bahari zetu zitafanya mawimbi daima
Na huku bahari yako imetulia haiyafichi mabuu[1].

Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu, na ambaye Mwenyezi Mungu hakumjaalia nuru, basi huyo hana nuru." Mpokezi anasema: Watu wakaangua kilio kwa sauti, na kusema, "Yatosha!!Ewe binti ya walio wema, kwani umezichoma nyoyo zetu na kuziunguza koo zetu na kuzichemsha tumbo zetu." Basi akanyamaza.

## KHUTBA YA BIBI UMMU KULTHUM BINTU ALI (A.S.).

Mpokezi anasema: Ummu Kulthuma bintu Ali (aleihimas salaam) pia, alikhutubia siku hiyo toka nyuma ya sitara yake, huku ameipaza sauti yake kwa kilio, na kusema,:

يا أهل الكوفة سوأة لكم ما لكم خذلتم حسينا و قتلتموه و انتهبتم أمواله و ورثتموه و سبيتم نساءه و نكبتموه فتبا لكم و سحقا ويلكم أ تدرون أي دواة دهتكم و أي وزر على ظهوركم حملتم و أي دماء سفكتموها و أي كريمة أصبتموها و أي صبية سلبتموها و أي أموال انتهبتموها قتلتم خير رجالات بعد النبي (صلّى الله عليه وآله وسلّم) و نزعت الرحمة من قلوبكم ألا إن حزب الله هم الفائزون و حزب الشيطان هم الخاسرون ثم قالت :

---

[1] Aina fulani ya wadudu.

قتلتم أخي صبرا فويل لأمكم *** ستجزون نارا حرها يتوقد
سفكتم دماء حرم الله سفكها *** و حرمها القرآن ثم محمد
ألا فأبشروا بالنار أنكم غدا *** لفي سقر حقا يقينا تخلدوا
و أني لأبكي في حياتي على أخي *** على خير من بعد النبي سيولد
بدمع غريز مستهل مكفكف على *** الخد مني دائما ليس يجم

"Enyi watu wa al-Kufa! Ole wenu! Ni kwa nini mlikosa kumnusuru Husein, (bali) mlimuuwa, na kumpora mali yake, na kumrithi, kisha mkawafanya mateka wanawake zake na kumletea maafa. Basi na muangamizwe (na Mwenyezi Mungu) na mdidimizwe.

Ole wenu! Je mwajua ni balaa gani imewafikieni? Na mzigo gani mmeubeba kwenye migongo yenu? Na ni damu gani mliyoimwaga? Na ni binti yake nani mliyemdhulumu? Na ni mwanamwali yupi mliyempora? Na ni mali ipi mliyowanyang'anya?

Mliwauwa watu bora baada ya Mtume (s.a.w.w.), mkatolewa huruma kwenye nyoyo zenu.

Tambueni kuwa, kwa hakika Kikundi cha Mwenyezi Mungu ndicho chenye ushindi, na kikundi cha shetwani ndicho chenye kupata khasara."

Kisha akasema shairi hili:

Mlimuuwa ndugu yangu mwenye subira ole wenu kwa maishilio yenu
Mtalipwa moto wenye joto la kuchoma
Mlizimwaga damu alizoharamisha Mwenyezi Mungu kuzichoma
Na Qurani imeziharamisha kisha Muhammad
Basi jibashirieni moto, hakika kesho
Mtatumbukizwa kwenye kina cha moto ambao joto lake linapanda
Hakika mimi nitamlilia ndugu yangu maishani mwangu wote
Nitamlilia atayezaliwa aliye mbora baada ya Mtume
Kwa machozi mengi na kwa kupaza sauti nitafuta
Shavu langu kwa uvumilivu usiohimidika

Mpokezi anasema:Watu wakaangua kilio na kulalama na kuomboleza.Wanawake wakayafungua (mafundo ya) nyele zao[1] na kuvipaka vichwa vyao kwa mchanga, na kuzikwaruza nyuso zao, na kuyapiga mashavu yao, na kuwaombea waangamizwe.Wanaume pia walilia na kuzing'oa ndevu zao, na hakukuwahi kuonekana wanaume na wanawake wenye kulia (na kuomboleza) zaidi ya siku hiyo.

**KHUTBA YA IMAM ZAINUL ABIDIN (A.S.).**

Kisha Imam Zainul A'bidin (a.s.) aliwaashiria watu hao kuwa wanyamaze. Waliponyamaza akasimama na kumhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifia na kumtaja Mtume kwa sifa anazostahiki, kisha akamswalia, kisha akasema:

أيها الناس من عرفني فقد عرفني، ومن لم يعرفني فأنا أعرفه بنفسي: أنا علي بن الحسين بن علي بن أبي طالب، أنا ابن المذبوح بشط الفرات من غير ذحل ولا ترات ، أنا ابن من انتهك حريمه وسلب نعيمه وانتهب ماله وسبي عياله، أنا ابن من قتل صبراً وكفى بذلك فخراً.

أيها الناس، ناشدتكم الله هل تعلمون أنكم كتبتم إلى أبي وخدعتموه وأعطيتموه من أنفسكم العهد والميثاق والبيعة وقاتلتموه وخذلتموه؟! فتباً لما قدمتم لأنفسكم وسوءاً لرأيكم، بأية عين تنظرون إلى رسول الله صلى الله عليه وآله اذ يقول لكم: قتلتم عترتي وانتهكتم حرمتي فلستم من أمتي؟!

[1] Ni katika ada za waarabu kwamba mwanamke anapokuwa katika msiba huzifungua nyele zake (zilizosukwa) kama alama ya kupatwa na majonzi.(mutarjumi)

"Enyi watu, anayenijua ananijua, na asiyenijua basi mimi ninajiarifisha binafsi kwake.Mimi ni Ali mwana wa Husein mwana wa Ali mwana wa Abi Twalib (a.s.).Mimi ni mwana wa aliyechinjwa kando ya mto al-Furat bila ya kuwepo na chuki (hapo kati) wala (kuwa ana) kisasi (cha kulipa).Mimi ni mwana wa aliyevunjiwa heshima ya harimu wake, na kupokonywa neema zake na kuporwa mali yake, na jamaa zake kufanywa mateka.Mimi ni mwanaa wa aliyeuliwa akiwa mwenye subira, na yatosha hiyo kuwa fakhari.
Enyi watu, nakuapieni Mwenyezi Mungu, je mwajua ya kwamba mlimwandikia Baba yangu na mkamuhadaa na kumpa kutoka kwenye nafsi zenu ahadi na mkataba na baia'h, kisha mkapigana naye na kukosa kumnusuru? Ole wenu kwa yale mliyozitangulizia nafsi zenu na aibu kwa rai yenu.Ni kwa jicho lipi mtamwangalia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu atakapowauliza: Mmekiuwa kizazi changu na kuivunja heshima yangu, basi nyinyi si katika umma wangu?!"
Mpokezi anasema: Sauti za watu zikapaa, toka pande zote, wakawa wanaambiana wenyewe kwa wenyewe, "Mmekwishaangamia na huku hamjui."
Kisha Imam (a.s.) akasema:

رحم الله أمرءاً قبل نصيحتي وحفظ وصيتي في الله وفي رسوله وأهل بيته، فان لنا في رسول الله أسوة حسنة. فقالوا بأجمعهم: نحن كلنا يابن رسول الله سامعون مطيعون حافظون لذمامك غير زاهدين فيك ولا راغبين عنك، فأمرنا بأمرك يرحمك الله، فإنا حرب لحربك وسلم لسلمك، لنأخذن يزيد ونبرأ ممن ظلمك وظلمنا.

"Mwenyezi Mungu amrehemu mtu ambaye ataikubali nasiha yangu na wasia wangu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na

Mjumbe wake na Watu wake wa Nyumbani, kwani hakika sisi tuna mfano bora katika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu." Wakasema wote kwa pamoja, "Sisi sote, ewe Mwana wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, tunakusikiza na tunakutii na tunachunga haki yako yako wala hatukupuuzi, wala kuwa na raghba ya asikuwa wewe.Basi tuamuru kwa amri yako, Mwenyezi Mungu akurehemu, kwani sisi ni vita kwa mwenye kuwa na vita nawe, na ni amani kwa mwenye kuwa na amani nawe.Kwa yakini tutamkamata Yazid (la'anahullah) na kumshutumu (na kujitenga na) mwenye kukudhulumu na kutudhulumu."
Imam (a.s.) akasema:

هيهات هيهات، أيها الغدرة المكرة، حيل بينكم وبين شهوات أنفسكم، أتريدون أن تأتوا إلي كما أتيتم إلى أبي من قبل؟! كلا ورب الراقصات، فان الجرح لما يندمل، قتل أبي صلوات الله عليه بالأمس وأهل بيته معه، ولم ينسني ثكل رسول الله صلى الله عليه وآله وثكل أبي وبني أبي، ووجده بين لهواتي ، ومرارته بين حناجري وحلقي، وغصصه تجري في فراش صدري.ومسألتي أن لا تكونوا لنا ولا علينا.

"Ni mbali sana, mbali sana, mnayoyadai, enyi watu wa khiana na njama, msifanikiwe kuyafikia matamanio ya nafsi zenu.Je mnataka kunijia kama mlivyowajia Baba zangu hapo awali?!Kamwe (siwakubali) kwa haki ya Mola wa nyota! kwani kidonda kingali hakijapona.Baba yangu (swalawatullahi aleihi) aliuwawa hapo jana, pamoja na watu wake wa nyumbani, na huku bado hakijasahaolika kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na kifo cha Baba yangu na wana wa Baba yangu, na huzuni yake ingali kwenye kimio changu, na uchungu wake ungalu upo baina ya kikoromeo na koo yangu, na majonzi yake yangali yananipita

kwenye ndani ya kifua changu.Ombi langu kwenu nikuwa msitufaidi wala kutudhuru.”

Kisha akasema:

لا غرو إن قتل الحسين وشيخه * قد كان خيراً من حسين وأكرما
فلا تفرحوا يا أهل كوفان بالذي * أصاب حسيناً كان ذلك أعظما
قتيل بشط النهر روحي فداؤه * جزاء الذي أراده نار جهنما

Si ajabu akiuwawa Husein kwani Babake
Alikuwa kuliko Husein Mbora na Mtukufu
Basi msifurahi enyi watu wa al-Kufa kwa yale
Yaliyompata Husein yalikuwa makuu zaidi
Aliyeuwawa kando ya mto, roho yangu fidia kwake
Malipo ya aliyemuuwa ni moto wa jahanamu.

Kisha Imam (a.s.) akasema

رضينا منكم رأساً برأس فلا يوم لنا ولا علين.

“Tumeridhia kutoka kwenu kichwa kwa kichwa, basi hakuna siku kwa faida yetu wala siku dhidi yetu.”

## IBNU ZIYAD AKETI KWENYE IKULU NA KUWAPA WATU WOTE IDHINI KUJA KUWAONA MATEKA.

Mpokezi anasema: Kisha Ibnu Ziad alikaa kwenye ikulu, na kutoa idhini kuwa watu wote waje, kisha kikaletwa kichwa cha Imam Husein (a.s.) na kuwekwa mbele yake, kisha akaamrisha, wakaletwa wanawake na watoto wa Imam Husein (a.s.).

Bibi Zainab (a.s.) akaketi huku hatambuliki. Ibnu Ziad akaulizia kuwa huyu ni nani, akaambiwa, “Huyu ni Zianab bintu Ali (a.s.).”

## BIBI ZAINAB (A.S.) ASEMEZANA NA IBNU ZIYAD.

Akaja upande alikokuwa na kumwambia, “Himidi kwa Mwenyezi Mungu ambaye amewafedhesha na kukadhibisha madai yenu ya uongo!!!”
Bibi Zainab akamjibu,” Bila shaka anafedheheshwa fasiki na anakadhibishwa mfisidi, naye ni mtu mwengine asiye kuwa sisi.”
Ibnu Ziyad akamwambia, “Je umeona Mwenyezi Mungu alivyo mfanya Ndugu yako na watu wako wa nyumbani?”
Bibi Zainab (a.s.) akamjibu, “ Sikuona kutoka kwa Mwenyezi Mungu ila Jamala[1].Hao ni watu walioandikiwa na Mwenyezi Mungu kuuwawa, basi wakatoka ili kwenda mahali pa maangamizo yao, naye Mwenyezi Mungu atakukusanya wewe pamoja nao ili utolewe hoja na kuhukumiwa.Basi angalieni ni nani atakeyepooza siku hiyo.Mama yako akumbwe na mswiba wako, ewe Ibnu Marjana.
Mpokezi anasema: Ibnu Ziad akakasirika, na ni kana kwamba alitamani kumuuwa.
Amru ibnu Hureith akasema, “Ewe amiri! Huyu ni mwanamke, na mwanamke halaumiwi kwa chochote anachosema.”
Basi Ibnu Ziad akamwambia Bibi Zainab (a.s.), “Mwenyezi Mungu ameutuliza moyo wangu kutokana na dhalimu wako Husein, na kutokana na waasi wapita mipaka, miongoni mwa watu wako wa nyumbani!

---

[1] Uzuri.

Akamjibu, “Wallahi! Umemuuwa Mzee wangu, na umelikata tawi langu, na umeung’oa mzizi wa asili yangu, basi ikiwa huku kunatuliza moyo wako basi umetulia.”
Ibnu Ziaad (la’anahullah) akasema, “Hili ni shairi, wallahi Baba yako alikuwa mwanashairi.”
Bibi Zainab akamwambia, “Yabna Ziad, mwanamke anashughuli gani na mashairi.”

## IMAM SAJJAD (A.S.) ASEMEZANA NA IBNU ZIYAD NA AZIMIO LAKE KUTAKA KUMUUWA IMAM (A.S.).

Kisha Ibnu Ziaad (la’anahullah) akamona Ali ibni Husein na kusema, “Ni nani huyu?”
Akaambiwa, “Ni Ali ibni Husein.”
Akasema, “Kwani si Mwenyezi Mungu alishamuuwa Ali ibnil Husein?!”
Imam Ali (a.s.) akamwambia, “Nilikuwa na ndugu aliyekuwa akiitwa Ali ibnil Husein, aliuliwa na watu.”
Akajibu, “Bali Mwenyezi Mungu ndiye alimuuwa.”
Imam Ali (a.s.) akasema, “Mwenyezi Mungu huzichukua nafsi wakati zinapokufa.”
Ibnu Ziad akamwambia, “Unafanya ujasiri wa kunijibu! Mchukueni muikate shingo yake.”
Shangazi yake, Bibi Zainaab akamsikia, akasema, “Yabna Ziad, hakika wewe hukumbakisha yeyote kati yeyu, basi ikiwa unaazimia kumuuwa, basi niuwe pamoja naye.”
Imam Ali (a.s.) akamwambia shangazi yake, “Tulia ewe shangazi, ili nizungumze nao.”
Kisha akamwelekea na kusema, “Eti unanitisha kwa kifo, yabna Ziad.Je hujajua kwamba kuuwawa kwetu ni ada na karama yetu ni katika kupata shahada.”

Kisha Ibnu Ziad aliamrisha kuwa Ali ibnu Husein achukuliwe, yeye pamoja jamaa zake, wakapelekwa kwenye nyumba moja iliyokuwa kando ya msikiti mtukufu.
Zainab bintu Ali (a.s.) akasema, “Asije kututembelea mwanamke yeyote mwarabu, ila tu mjakazi mwenye moto[1], au anayemilikiwa, kwani hawa ni mateka kama tulivyo fanywa mateka.”

## **KICHWA CHA IMAM HUSEIN (A.S.) CHAZUNGUSHWA KWENYE MJI WA AL-KUFA.**

Kisha Ibnu Ziad akatoa amri kuwa kichwa cha Imam Husein (a.s.) kiletwe, kialetwa kisha kikazungushwa kwenye vichochoro vya mji wa al-Kufa.
Na hapa panastahiki kuzisoma baadhi ya beti za mtu katika wenye akili, alizozitunga katika kumuomboleza aliyeuwawa katika kizazi cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), kwa kusema:

رأس ابـن بنت محمد ووصيـه * للناظرين على قنـاة يرفـع
والمسلمون بمنظـر وبسمـع * ا منكر منهـم ولا متفجـع
كحلت بمنظرك العيون عمايـة * واصم رزؤك كل أذن تسمـع
أيقظت أجفاناً وكنت لها كـرى * وأنتم عيناً لم تكن بك تهجـع
ما روضة إلا تمنـت أنـها * لك حفرة ولخط قبرك مضجع

Kichwa cha mwana wa Binti ya Muhammad na Wasia wake
Kinatungikwa kwenye mkuki ili wakione wenye kuona
Na huku waislamu ni wenye kuyaona yote na kuyasikia
Na wala hakuna mwenye kupinga wala kuangua kilio

[1] Yaani ummu walad naye ni mjakazi ambaye mtoto wake ni mwanahuru kwani baba yake ni bwana mmiliki, anayemmliki yule mjakazi.(mtarjumi)

Kwa kukuona macho yamepakwa wanja wa upofu
Na msiba wako umelifanya ziwi kila sikio lisikialo
Umeziamsha kope na kwazo ulikuwa mwenye kulala
Na umelilaza jicho lililokuwa halijalal kwa ajili yako
Hakuna bustani yeyote ila tu ilitamani kuwa
Iwe ni shimo lako na kaburi utakapo lazwa.

## UPINZANI WA ABDULLAH IBNU AFIF KWA IBNU ZIYAD ALIPOMSHUTUMU IMAM HUSEIN (A.S.), KISHA KUFA KWAKE SHAHIDI.

Mpokezi anasema: Kisha Ibnu Ziad (la'anahullah) alipanda juu ya membar, akamhimidi Mwenyezi Mungu, na kumsifu, kisha akasema katika baadhi aliyoyasema, "Himidi yote ni ya Mwenyezi Mungu, ambaye ameidhihirisha haki na watu wake, na akamnusuru Amirul Mu-uminina na wafuasi wake, na akamuuwa mwongo mwana wa muongo!!."
Kabla ya kutamka maneno zaidi, alisimama A'bdullah ibnu A'fif al-Azdi- aliyekuwa miongoni mwa mashia wema na wenye zuhdi, ambaye alikuwa amelipoteza jicho lake la kushoto katika vita vya al-Jamal, na la kulia katika vita vya as-Swiffin, ambaye alikuwa anamazoea ya kukaa msikitini mtukufu akiswali hadi usiku- akasema, "Yabna Marjana!Hakika mwongo, mwana wa mwongo ni wewe na babako, pamoja na aliyekuteuwa wewe na (vilevile) babake, ewe aduwi wa Mwenyezi Mungu, mnawauwa Wana wa Mitume kisha mnazungumza kwa maneno haya juu ya membari za waislamu!!"
Mpokezi anasema: Ibnu Ziad akakasirika (kwa maneno haya) na kusema, "Ni nani huyo aliyezungumza?"
Akajibu, "Ni mimi niliyezungumza, ewe adui ya Mwenyezi Mungu! Unakiuwa kizazi kitoharifu, kilichoondolewa uchafu na Mwenyezi Mungu, kisha unadai kuwa wewe unaifwata dini ya uislamu.

Waa ghaothaa!! Wako wapi wana wa muhajirina na answar waje walipize kisasi kutoka kwako na kutoka kwa dhalimu wako, malu-uni mwana wa malu-uni (aliyelaaniwa) kwa ulimi wa Muhammad, Mjumbe wa Mola wa walimwengu?"

Mpokezi anasema: Maneno haya yalimfanya Ibnu Ziad (la'anahullah) kukasirika zaidi hata mishipa yake kuvimba kwa hasira.Akasema, "Mleteni hapa."

Walinzi wakamvamia toka pande zote ili kumchukua, lakini masharifu wa kabila la Azdi miongoni mwa wana wa ami yake walisimama haraka na kumuokoa kutoka mikononi mwa walinzi, na kumtoa kupitia kwenye mlango wa msikiti na kuondoka naye hadi nyumbani kwake.

Ibnu Ziad akasema, "Nendeni kwake huyu kipofu- kipofu wa kabila la Azdi, Mwenyezi Mungu aupofushe moyo wake kama alivyopofusha macho yake- kisha mumlete kwangu."

Mpokezi anaendelea kusimilia: Basi wakatoka kumfwata.Kabila la Azdi waliposikia habari, wakakusanyika na yakakusanyika pamoja nao makabila ya Yemen, ili kumlinda swahibu wao.

Anaendelea kusimulia: Mambo haya yakamfikia Ibnu Ziad, akayakusanya makabila ya Mudhar na kumfanya Muhammad ibnul Ash'ath kuwa kiongozi juu yao na kuwaamuru kupigana na kikundi kile.

Msimulizi anaendelea kusema: Basi wakapambana mapambano makali, wakauwawa baadhi ya waarabu.

Anasimulia kuwa: Wafuasi wa Ibnu Ziad (la'anahullah) wakafika kwenye nyumba ya A'bdullah ibnu A'fif, wakauvunja mlango na kumshambulia.Binti yake akapaza sauti na kusema, "Maadui wamekujia kupitia upande unaotahadhari."

Naye akamjibu, "Usijali chochote, nipatie upanga wangu."Akampa upanga wake, akawa anaipigania nafsi yake huku akisema:

Mimi ni mwana wa mwenye fadhila Afif aliye twahiri

Afif ni Mzee wangu mwana wa Ummu Aa’mir
Ni wangapi waliovaa deraya na wasiovaa
Na majasiri niliowashinda kwenye mapambano wengi
Anaendelea kusimulia:Binti yake akawa anamwambia, “Ewe baba, laiti nilikuwa mwanamume, ili nipambane na hawa watu mafasiki, mbele yako, wauwaji wa kizazi chema (cha Mtume).”
Watu wale wakawa wanajaribu kumzunguka pande zote, naye huku anaipigania nafsi yake, wala hakuna amuwezaye.Nao kila walipomjia kwenye upande mojawapo binti yake alimwambia, “Ewe baba wamekujia kupitia upande Fulani.”Hadi walipomzidia na mwishowe kumzingira kote.
Binti yake akasema, “Woi udhalili! Baba yangu anazingirwa na wala hana wa kumnusuru ili amuombe msaada.”
Basi akaanza kuuzungusha upanga wake huku akisema:

أقسم لو يفسح لي عن بصري * ضاق عليكم موردي ومصدري

Ninaapa kuwa lao kama ningefunguliwa macho yangu
Kuingia kwanngu na kutoka kwangu kungewabana kweli

Mpokezi anasema: Waliendelea kupigana naye hadi kumkamata, kisha wakampeleka kwa Ibnu Ziad.
Ibnu Ziad alipomwona akasema, “Himidi kwa Mwenyezi Mungu aliyekufedhehesha.”
A’bdullah ibnu A’fif akamwambia, “Ewe adui wa Mwenyezi Mungu, na ni kwa nini Mwenyezi Mungu amenifedhehesha?”
Wallahi lao kama ningefunguliwa macho yangu
Kuingia kwangu na kutoka kwangu kungewabana kweli.
Ibnu Ziad akamwambia, “Unasemaje ewe Abdullah kumhusu Amirul Muuminin U’thman ibnu A’ffan?”

Akamjibu, “Ewe Mtumwa wa Bani I’laaj, ewe Ibnu Marjana”- na akamshutumu- “anakuhusu nini U’thman ibnu A’ffan, ikiwa amefanya mabaya au amefanya mema, ametengeza au ameharibu?Mwenyezi Mungu ndiye walii wa viumbe vyake, atahukumu baina yao na U’thman ibnu A’ffan kwa uadilifu na kwa haki, lakini niulize kukuhusu wewe na kumhusu baba yako na Yazid na baba yake.”

Ibnu Ziad akasema, “Wallahi sikuulizi chochote mpaka utakapo onja mauti kwa machungu baada ya machungu.”

Abdullah ibnu A’fif akamwambia, “Alhamdullah Rabbil A’lamin, ama mimi, nilikuwa nikimuomba Mwenyezi Mungu aniruzuku shahada kabla ya mama yako kukuzaa, na nilimuomba Mwenyezi Mungu aijaaliye shahada hiyo niipate mkononi mwa aliyemaluuni zaidi katika viumbe vyake, na aneyemchukia zaidi.Nilipopatwa na upofu nilikata tama ya kupata shahada, na sasa hivi namhimidi Mwenyezi Mungu aliyeniruzuku shahada baada ya kukata tama, na kunijulisha majibu ya dua yangu ya tangu kwa fadhila yake.

Ibnu Ziad akasema, “Ikateni shingo yake.”

Akakatwa shingo yake kisha kusulubishwa huko Sabkha.[1]

Mpokezi anasema: Kisha Ubeidullah ibnu Ziad alimwandikia Yazid ibnu Mua’wiya akimjulisha kuuwawa kwa Imam Husein, na habari za watu wake wa nyumbani.

Alimwandikia pia A’mru ibnul Aa’s, aliyekuwa amiri wa Madina akimjulisha habari hizo pia.

Ama A’mru, alipopokea habari hizo, alipanda juu ya membar na kuwahutubia watu, na kuwajulisha habari hizo, zikawafanya Bani Hashim kulia sana, wakaomboleza na kutekeleza suna na ada za misiba na matanga.

---

[1] Jina la sehemu mojawapo huko Basra au Bahrain au baina na al-Kufa na Sahla.

## ZAINAB BINTU A'QIL (A.S.) AMUOMBOLEZA IMAM HUSEIN (A.S.).

(a.s.) alikuwa Naye Zainab binti A'qil ibni Abi Twalib akimuomboleza Imam Husein (a.s.) kwa kusema:

ماذا تقولــون إذ قال النبي لكم * ماذا فعلتمو أنتـم آخــر الأمم

بعترتـي وبأهلي بعـــد مفتقدي * منهـم أسارى ومنهم ضرجوا بـدم

**ماكان هذا جزائي إذ نصحت لكم * أن تخلفوني بسوء في ذوي رحمي**

Mtasema nini atakapowaambieni Mtume
Mlifanya nini nanyi ndio umma wa mwisho
Kwa kizazi changu na ahli wangu baada ya kuondoka kwangu
Baadhi yao mateka na baadhi walipakwa kwa damu zao
Hii haikuwa ndio jazaa yangu nilipowanasihi
Mkanilipa kwa mabaya katika kizazi changu

Mpokezi anasema: Usiku ulipoingia wakazi wa mji wa Madina walisikia sauti ikinadi na kusema:

أيها القاتلون ظلماً حسينـاً * ابشروا بـالعذاب والتنكيـل

كل من في السماء يبكـي عليـه * مـن نبي وشاهد ورسول

قد لعنتم على لسان ابـن داود * وموسى وصـاحب الإنجيل

Enyi mlio muuwa Husein kwa dhulma
Jibashirieni kupata adhabu na mateso
Kila aliye binguni anamlilia
Katika Mitume na Mashahidi na Marasuli

Mmeshalaaniwa kwa ulimi wa Ibnu Dawud
Na Musa na Yule aliyepewa Injili.

## MSAFARA WA MATEKA HADI MJI WA SHAM.

Ama Yazid ibnu Mua'wiya, yeye alipopokea barua kutoka kwa Ibnu Ziyad na kuisoma, alimtumia majibu na kumuamuru kuwa akibebe kichwa cha Husein (a.s.) na vichwa vya walio uwawa pamoja naye, na vilevile avibebe vitu alivyoviacha nyuma pamoja na wanawake zake na ayali wake.
Ibnu Ziyad akamwita Muhaffaz ibnul A'idhi na kumkabidhi vichwa vile pamoja na mateka na wanawake.Muhaffaz akasafiri nao hadi Sham kama wanavyosafirishwa mateka walio makafiri,na huku watu wa kila miji wanawapekua nyuso zao.

## MTU MIONGONI MWA WALIOKIBEBA KICHWA CHA IMAM HUSEIN (A.S.) ASIMULIA ALIVYOONA KUSHUKA KWA MITUME (A.S.) NA MALAIKA (A.S.) KANDO YA KICHWA CHAKE KITUKUFU.

Ibnu Lahi'ah na wengineo wamepokea hadithi ambayo tutaitaja tu sehemu tunayoihitajia.
Anasema: Nilikuwa katika hali ya kutufu Nyumba Tukufu (Kaaba), ghafla nikakutana na mtu aliyekuwa akisema: "Ewe Allah! Nisamehe, na wala sioni kuwa utanisamehe."
Nikamwambia "Ewe mja wa Mwenyezi Mungu, ittaqillah (muogope Mwenyezi Mungu) na wala usiseme hivyo, kwani madhambi yako lao kama yatakuwa mfano wa matone ya mvua na majani ya miti,kisha ukamuomba akusamehe atakusamehe, hakika Yeye ni msamehevu, mwenye kurehemu."

Kisha akasema: Akaniambia, “Njoo karibu nami ili nikusimulie kisa changu.”
Basi nikamkaribia.
Akasema, “Jua kwamba, sisi tulikuwa watu hamsini, tuliosafiri pamoja na kichwa cha Husein hadi Sham.Jioni ilipokuwa ikitufika tulikuwa tukikiweka kichwa kwenye sanduku, kisha tunakunywa pombe kando ya sanduku lile. Katika usiku mojawapo, masahibu wangu walikunywa hadi wakalewa, lakini mimi sikunywa pamoja nao.Kulipokuwa usiku wa manane, nilisikia sauti ya radi na kuona umeme, mara milango ya mbingu ikafunguka, wakashuka Adam na Nuhu na Ibrahim na Is-haq na Isma’il na Mtume wetu Muhammad (swalallahu a’leihi wa aalihi wa a’leihim ajma’in) na wakiwa pamoja nao Jibrail na kikundi cha Malaika.
Jibrail (a.s.) aliikaribia sanduku, akakitoa kichwa na kukikumbatia na kukibusu.Kisha Mitume wote wakafanya vivyo.Mtume (s.a.w.w.) akakililia kichwa cha Husein, nao Mitume wakampa taazia[1].
Jibrail akamwambia, “Ya Muhammad! Hakika Mwenyezi Mungu ameniamuru ya kwamba nikutii katika utakachaniamuru kuhusiana na umma wako.Basi ukiniamuru, nitaitetemesha ardhi pamoja nao, na kuipendua ya juu kuwa chini, kama nilivyowafanya qaumu ya Lut.”
Mtume (s.a.w.w.) akasema, “La, ewe Jibrail! Kwani nitakuwa na kesi nao mbele ya Mwenyezi Mungu, siku ya Qiyama.”
Kisha Malaika wakaja upande wetu ili watuuwe.
Nikasema, “Naomba amani!! Ya Rasulallah!!”
Akajibu, “Nenda!! Na wala Mwenyezi Mungu asikusamehe.”
Mpokezi anaendelea kusema: Wale watu walisafiri na kichwa cha Imam Husein (a.s.) na wanawake na mateka wa

[1] Rambirambi.

kiume.Walipokaribia Damaskas[1], Ummu Kulthum akamkaribia Shimri, aliyekuwa miongoni mwao, na kumwambia, "Nina haja kutoka kwako."

Akasema, "Ni nini haja yako."

Akajibu, "Utakapotuingiza mjini, basi tupitishe kwenye njia yenye watazamaji wachache, na nenda mbele kidogo uwaambie kwamba waviondoe vichwa hivi na kuviweka mbali nasi, kwani tumefedheheka kutokana na kutazamwa kwingi nasi tuko katika hali hii."

Katika kumjibu maombi yake, aliamrisha kuwa vichwa vitungikwe kwenye mikuki na kuwekwa katikati ya msafara wao, kwa ujeuri na ukafiri wake, kisha akawapitisha karibu na watu wenye kuwatazama wakiwa katika hali hiyo, hadi kuwafikisha kwenye maingilio ya Damaskas na kusimama kwenye ngazi za mlango wa msikiti mkuu, mahala wanaposimamishwa mateka.

Inapokewa kuwa mmoja wa tabi'ina alipokiona kichwa cha Imam Husein (a.s.) huko Sham, alijificha kwa muda wa mwezi mmoja mbali na maswahibu wake wote.Walipomwona baada ya kumkosa kwa muda huo, wakamuuliza sababu ya kupotea, akajibu, "Hamuoni kilichotufikia?" Kisha akasoma beti hizi:

جاؤوا برأسك يا بـن بنت محمد * متزملاً بدمائـه تزميـلا

وكأنما بك يا بـن بنت محمد * قتلوا جهاراً عامديـن رسـولا

قتلوك عطشاناً ولمـا يرقبوا * في قتلك التنزيـل والتأويـلا

ويكبرون بـأن قتلت وإنمـا * قتلو بك التكبيـر والتهليـلا

Wamekuja na kichwa chako Yabna binti Muhamad

[1] - Damascus (sham).

Kikiwa kimefinikwa kwa damu yake kikamilifu
Kana kwamba wewe Yabna binti Muhamad
Walikuuwa waziwazi wakimkusudia Mtume
Walikuuwa kwa kiu na wala hawakuchunga
Katika kukuuwa Qurani na ta-awili yake
Huku wanapiga takbiri kuwa umeuwawa bali
Kwa kukuuwa wameiuwa takbiri na tahlili.

## IMAM SAJJAD (A.S.) ASEMEZANA NA MTU ALIYEONYESHA FURAHA KWA KUUWAWA IMAM HUSEIN (A.S.).

Mpokezi anasema: Mzee mmoja alikuja na kuwakaribia wanawake wa Imam Husein (a.s.) na ayali wake, wakiwa katika sehemu ile, na kusema, “Himidi kwa Mwenyezi Mungu ambaye amewauwa na kuwaangamiza na kuipumzisha miji kutokana na rijali wenu na kumwezesha Amirul Muuminina (Yazid) kuwashinda nyinyi!!”
Ali ibnil Husein (a.s.) akamjibu, “Ewe mzee, je umesoma Quran?”
Akasema, “Na’am.”
Akasema, “Basi, je unaijua aya hii (Sema: siwaulizi malipo yoyote juu yake ila tu kuwapenda alqurba (jamaa wangu wa karibu.)”
Mzee akajibu, “Nimewahi kuisoma.”
Basi Imam Ali (a.s.) akamwambia, “Sisi ndio alqurba (jamaa wangu wa karibu), ee mzee.Na je umewahi kuisoma (aya) katika (sura ya) Bani Israil (Na mpe alqurba (jamaa wa karibu.) haki yake)?”
Mzee akajibu, “Nimewahi kuisoma.”
Akasema, “Sisi ndio alqurba, ee Mzee.Na je umewahi kuisoma aya hii (Na jueni ya kwamba, chochote mnachofaidika kama ngawira, basi khumsi yake ni ya

Mwenyezi Mungu na ya Mtume na ya dhil qurba (jamaa wa karibu.)”

Akasema, “Na’am.”

Imam (a.s.) akasema, “Sisi ndio alqurba, ewe mzee.Na je, umewahi kuisoma aya hii (Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu enyi Ahlul Beit (Watu wa Nyumba), na kuwatakasa mtakaso mkuu.)?”

Mzee akasema, “Nimewahi kuisoma hiyo.”

Imam (a.s.) akasema, “Sisi ndio Ahlul Beit, ambao Mwenyezi Mungu ameiteremsha aya ya twahara khasa kwa ajili yetu, ewe mzee.”

Mpokezi anasema: Yule Mzee alibaki amenyamaza na mwenye kujuta kwa yale aliyoyasema, na kusema, “Tallahi!!Hakika nyinyi ndio wao?!!”

Imam Ali ibnil Husein (a.s.) akamwambia, “Tallahi sisi kwa hakika ndio wao bila shaka.Kwa haki ya Babu yetu, sisi kwa hakika ndio wao.”

Mpokezi anaendelea kusimulia: Mzee akaanza kulia na kukitupa kilemba chake, kisha akakiinua kichwa chake kuelekea mbinguni na kusema: Ewe Allah! Hakika mimi najiweka kwako mbali na adui wa Aali Muhammad (s.a.w.w.) katika majini na watu.”

Kisha akasema, “Je ninaweza kutubiwa.”

Akamjibu, “Na’am, ukitubu Mwenyezi Mungu atakutubia, na utakuwa pamoja nasi.”

Kisha akasema, “Mimi ni mwenye kutubu.”

Yazid ibnu Mu’awiya akafikiwa na habari za mzee, akaamuru kuwa aletwe kisha akaamuru kwa auwawe, akauliwa.

## MATEKA WAINGIZWA NA KULETWA MBELE YA YAZID HUKU WAKIWA WAMEFUNGWA KWA MAKAMBA.

Mpokezi anaendelea kusimulia: Kisha Yazid akaletewa mizigo yake Imam Husein (a.s.) pamoja na wanawake zake na wengine waliobaki hai miongoni mwa ahli wake, huku wamefungwa kwa kamba.
Walipofika mbele yake, wakiwa katika hali hii, Imam Ali ibnil Husein (a.s.) akamwambia, “Ninakuapizia Mwenyezi Mungu, ewe Yazid, unamdhania nini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu lao kama atatuona katika hali hii?”
Yazid akaamrisha kamba zile zikatwe, zikakatwa.
Kisha akakiweka kichwa cha Imam Husein (a.s.) mbele yake, na kuwafanya wanawake kuketi nyuma yake ili wasije wakakitazama, lakini Imam Ali ibnil Husein alikiona, na baada yake hakuweza kula tena vichwa.

## ALIYOYASEMA BIBI ZAINAB (A.S.) ALIPOKIONA KICHWA KITUKUFU CHA IMAM HUSEIN (A.S.).

Ama Zainab (a.s.) alipokiona aliikamata nguo yake na kuipasua kwenye kifua, kisha akaita kwa sauti ya huzuni yenye kuzijeruhi nyoyo, “Woi Husein wangu!! Ewe kipenzi cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!! Ewe mwana wa Makka na Madina!! Ewe mwana wa Fatima az-Zahra Bibi wa wanawake wa Peponi!! Ewe Mwana wa Bintul Mustafa!!”
Mpokezi anasema: Akamliza, wallahi, kila aliyekuwa kwenye kikao, huku Yazid amenyamaza.

## MWANAMKE KATIKA BANI HASHIM AMUOMBOLEZA IMAM HUSEIN (A.S.) KATIKA NYUMBA YA YAZID (LA’ANAHULLAH).

Kisha mwanamke mmoja wa bani Hashim aliyekuwa kwenye ikulu ya Yazid, akaanza kumuomboleza Imam Husein (a.s.) huku akinadi, “Ewe Husein wangu! Ewe kipenzi changu! Ewe Bwana wangu! Ewe Bwana wa Ahlu Baiti wangu! Ewe

Mwana wa Muhammad wangu! Ewe mlezi wa wajane na mayatima, ewe aliyeuwawa na wanaharamu.”
Mpokezi anasema: Akamliza kila aliyemsikia.

## ABU BARZA AL-ASLAMI APINGA KITENDO CHA YAZID ALIPOMWONA AKIYACHOKORA MENO YA IMAM HUSEIN (A.S.) KWA KIJITI.

Kisha Yazid akaitisha kijiti cha khairazan, akawa anayachokora kwa kijiti hicho meno ya Imam Husein (a.s.). Abu Barza al-Aslami akaja karibu naye na kumwambia, “Ole wako ewe Yazid, Unauchokora kwa kijiti chako mdomo wa Husein (a.s.), mwana wa Fatima?!. Ninashuhudia kwamba nilimuona Mtume (s.a.w.w.) anaibusu meno yake na meno ya ndugu yake, Hasan (a.s.), huku akisema, “Nyinyi wawili ni Mabwana wa vijana wa Peponi.Mwenyezi Mungu awaangamize watakaowauwa (nyinyi) na awalaani na kuwaingiza Jahanamu, na hakika (Jahanamu) ni maishilizio mabaya kweli.”
Mpokezi anasema: Yazid akakasirika na kuamuru kuwa aondolewe, akaondolewa kwa kuburutwa.

## YAZID ASOMA BETI ZA MASHAIRI YA IBNUZ ZAB’ARI.

Anaendelea kusimulia: Yazid (la’anahullah) akawa ni mwenye kumathilisha kwa beti za Ibnuz Zab-a’ri kwa kusema:

ليت أشياخي ببدر شهدوا * جزع الخزرج من وقع الأسل
فأهلوا واستهلوا فرحاً * ثم قالوا: يا يزيد لا تشل
قد قتلنا القرم من ساداتهم * وعدلناه ببدر فاعتد
لعبت هاشم بالملك فلا * خبر جاء ولا وحي نزل
لست من خندف إن لم أنتقم * من بني أحمد ما كان فعل

Laiti wazee wangu walokuwa Badri wangeshuhudia
Majonzi ya Khazraji kwa makali ya mapanga
Wangeingia na kupaza sauti kwa furaha
Kisha wakasema: Ewe Yazid usifariki!
Tumemuuwa mkuu katika viongozi wao
Tukawaadili[1] walotufanya Badri kukaadilika
Banu Hashim waliuchezea ufalme na wala
Hakuna habari wala wahyi uliyoshukia
Sikutokana na Khandaf nikikosa kulipiza kisasi
Kutoka kwa Bani Ahamad kwa yale aliyofanya.

## KHUTBA YA BIBI ZAINAB (A.S.) AKIMKUMBUSHA KUFURU YAKE NA MAOVU YAKE.

Mpokezi anasema: Bibi Zainab bintu Ali (aleihimas salaam) akasimama na kusema:

الحمد لله رب العاليمن، وصلى الله على محمد وآله أجمعين، صدق الله كذلك يقول: **(ثم كان عاقبة الذين أساؤا السوءى أن كذبوا بآيات**

[1] - Yaani tukawalipiza kisasi.

**الله وكانوا بها يستهزؤون)** ، أظننت يا يزيد . حيث أخذت علينا أقطار الأرض وآفاق السماء فأصبحنا نساق كما تساق الإماء . أن بنا على الله هواناً، وبك عليه كرامة!! وأن ذلك لعظيم خطرك عنده!! فشمخت بأنفك ونظرت في عطفك ، جذلاً مسروراً،حين رأيت الدنيا لك مستوسقة، والأمور متسقة، وحين صفا لك ملكنا وسلطاننا، فمهلاً مهلاً، أنسيت قول الله عزوجل: **(ولا يحسبن الذين كفروا أنما نملي لهم خير لأنفسهم إنما نملي لهم ليزدادوا إثماً ولهم عذاب مهين)**.

أمن العدل يا بن الطلقاء تخديرك إماءك ونساءك وسوقك بنات رسول الله سبايا؟!، قد هتكت ستورهن، وأبديت وجوههن، تحدو بهن الأعداء من بلد إلى بلد، ويستشرفهن أهل المنازل والمناهل، ويتصفح وجوههن القريب والبعيد، والدني والشريف، ليس معهن من رجالهن ولي، ولا من حماتهن حمي.

وكيف ترتجى مراقبة من لفظ فوه أكباد الأزكياء، ونبت لحمه بدماء الشهداء؟!

وكيف يستظل في ظلمنا أهل البيت من نظر إلينا بالشنف والشنآن والإحن والأضغان؟!

ثم تقول غير متأثم ولا مستعظم:

فأهلوا واستهلوا فرحاً * ثم قالوا: يا يزيد لا تشل

منتحياً على ثنايا أبي عبد الله عليه السلام سيد شباب أهل الجنة تنكتها بمخصرتك.

وكيف لا تقول ذلك، وقد نكأت القرحة، واستأصلت الشأفة، بإراقتك دماء ذرية محمد صلى الله عليه وآله ونجوم الأرض من آل عبد المطلب؟! وتهتف بأشياخك، زعمت أنك تناديهم!
فلتردن وشيكاً موردهم، ولتودن أنك شللت وبكمت ولم تكن قلت ما قلت وفعلت ما فعلت.
اللهم خذ بحقنا، وانتقم ممن ظلمنا، واحلل غضبك بمن سفك دماءنا وقتل حماتنا.
فوالله ما فريت إلا جلدك، ولاحززت إلا لحمك، ولتردن على رسول الله صلىالله عليه وآله بما تحملت من سفك دماء ذريته، وانتهكت من حرمته في عترته ولحمته، وحيث يجمع الله شملهم ويلم شعثهم، ويأخذ بحقهم **(ولا تحسبن الذين قتلوا في سبيل الله أمواتاً بل أحياء عند ربهم يرزقون)**.
وحسبك بالله حاكماً، وبمحمد صلى الله عليه وآله خصيماً، وبجبرئيل ظهيراً، وسيعلم من سول لك ومكنك من رقاب المسلمين، بئس للظالمين بدلاً وأيكم شر مكاناً وأضعف جنداً.
ولئن جرت علي الدواهي مخاطبتك، أني لأستصغر قدرك، وأستعظم تقريعك، واستكثر توبيخك، لكن العيون عبرى، والصدور حرى.
ألا فالعجب كل العجب لقتل حزب الله النجباءبحزب الشيطان الطلقاء، فهذه الأيدي تنضح من دمائنا، والأفواه تتحلب من لحومنا، وتلك الجثث الطواهر الزواكي تتناهبها العواسل وتعفوها أمهات

الفراعل، ولئن أتخذتنا مغنماً لتجدنا وشيكاً مغرماً، حين لا تجد إلا ما قدمت يداك، وما ربك بظلام للعبيد، فإلى الله المشتكى، وعليه المعول.

فكد كيدك، واسع سعيك، وناصب جهدك، فوالله لا تمحو ذكرنا، ولا تميت وحينا، ولا تدرك أمدنا، ولا ترحض عنك عارها.

وهل رأيك إلا فندا، وأيامك إلا عددا، وجمعك إلا بددا، يوم ينادي المناد: ألا لعنة الله على الظالمين.

فالحمد لله الذي ختم لأولنا بالسعادة والمغفرة، ولآخرنا بالشهادة والرحمة.

ونسأل الله أن يكمل لهم الثواب، ويوجب لهم المزيد، ويحسن علينا الخلافة، إنه رحيم ودود، وحسبنا الله ونعم الوكيل.

"Himidi yote ni ya Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu, na rehma ya Mwenyezi Mungu imshukie Muhammad na aali zake wote.Amesema kweli Mwenyezi Mungu aliposema **(Kisha ukawa mwisho wa wale waliofanya uovu ni kuzikadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu na wakawa ni wenye kuzifanyia kejeli)**[1].
Je unadhania, ewe Yazid - kwa kuwa umetubania ardhi na mbingu, kisha tukawa tunasukumwa kama wanavyosukumwa wajakazi - ya kuwa sisi ni madhalili mbele ya Mwenyezi Mungu, na ya kuwa wewe una utukufu

[1] - Rum – 10.

kwake?!!na ya kwamba hilo ni kutokana na cheo chako kitukufu mbele yake (Mwenyezi Mungu) ?!!Ndio ukaliinua pua lako kwa kiburi na kujiangalia kwa furaha na sururi, ulipoiona dunia imekufanyia utiifu na mambo pia kukuelekea, na pindi ulipoyafikia mamlaka yetu na ufalme wetu bila mpinzani.Basi nenda pole, wala usiharakishe! Je umeisahao kauli ya Mwenyezi Mungu, (Wala wasidhani waliokufuru kwamba muda tunaowapa (wakaishi kwa starehe) ni bora kwao, hakika tunawapa muda ili wazidishe madhambi, na wana adhabu yenye kudhalilisha.)[1].
Je ni uadilifu, ewe mwana wa "Tulaqaa",[2] wewe kuwasitiri (nyumbani) wajakazi wako na wanawake zako na huku unawatembeza mabanati wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wakiwa mateka?!.Umewavunjia sitara yao, na kuzidhihirisha nyuso zao, unawatoa kwa maadui toka mji hadi mji mwingine, wakiwatizama watu kutoka majumbani mwao na wanaoishi pembeni mwa mapito ya maji ya kunywa,na huku watu wa karibu na wa mbali wakizichunguza nyuso zao, na walio duni na masharifu, na hali ya kuwa hawana pamoja nao mlinzi wala wa kuwahami, katika wanaumu waliokuwa nao.
Na itawezekan kutarajia kuhifadhi na mtu ambaye mdomo wake ulioyatoa na kuyatema maini ya watu wema, na nyama za mwili wake zimekuwa kwa damu za mashahidi?![3]
Na watawezaje kukipata kivuli chetu sisi Ahlul bait (siku ya Qiyama) wenye kutuangalia kwa chuki na bughudhi na uadui na dharao?! Kisha wasema, na huku huoni kuwa una kosa lolote wala kuoni kuwa ni jambo kubwa:

---

[1] - Aali Imran – 178.
[2] - Tulaqaa ni walioachwa huru baada ya kufanywa mateka baada ya Mtume (s.a.w.a) kuuteka mji wa Makka. (Mtarjumi).
[3] - Anamkusudia nyanya yake Yazid aliyekuwa akiitwaHind, aliyefanya mbinu za kumuuwa Hamza (a.s.) katika vita vya Uhud, kisha akaupasua mwili wake na kulitafuna ini lake.

Wangeingia na kupaza sauti kwa furaha
Kisha wakasema: Ewe Yazid usifariki

Huku unayaegemea meno ya Abu Abdillah (a.s.) Bwana wa vijana wa Peponi na kuyachokora kwa kijiti chako.
Na utakosaje kusiseme vivyo na hali ya kuwa umekichibua kidonda kabla ya kupona, na umekikata kwenye asili yake, kwa kuimwaga kwako damu ya kizazi cha Muhammad (s.a.w.a.) na nyota za ardhi katika kizazi cha Abdul Muttalib?!Eti unawapazia sauti wazee wako, huku unadhani kuwa unawanadi!
Bila shaka karibuni utaingia walipoingia, na kwa hakika utatamani kuwa ulikuwa umepooza na kuwa bubu na ulikuwa hujasema uliyoyasema na kufanya uliyoyafanya.
Ewe Allah! Tuchukulie haki yetu na tulipizie kutokana na aliyetudhulumu na iteremshe ghadhabu yako juu ya aliyezimwaga damu zetu na kuwauwa wenye kutuhami.
Wallahi haukuichuna ila ngozi yako na wala hukukikata ila kiwiliwili chako.Utakutana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ukiwa huku umeyabeba yale uliyohimili katika kuzimwaga damu za kizazi chake, na kumvunjia heshima yake kwa uliyowafanyia jamaa zake na kizazi chake, ambapo Mwenyezi Mungu atawakusanya na kuunganisha kutengana kwao na kuwachukulia haki yao **(Wala usiwadhani wale walio uliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu, bali wanaruzukiwa kwa Mola wao)**.
Na yakutosha kuwa Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuhukumu na Muhammad (s.a.w.w.) ndiye mdai wako, na Jibrail (a.s.) ndiye mtetezi wake. Na (karibuni) aliyekuhadaa na kukuwezesha kuwakalia waislamu, atajua ni baya mno walilojichagulia madhalimu kuwa badala, na atajua ni nani kati yenu ndiye mwenye makao mabaya na mwenye askari dhaifu zaidi.

Hata ikiwa nitakumbwa na mashaka kwa kukuhutubia, hakika mimi nitafanya duni thamani yako, na kuzidisha kukuumiza kwa kukulaumu na kuzidisha kukukebehi, lakini macho yana majonzi na vifua vina machungu.
Hakika ni ajabu, na ajabu kweli, kuuliwa kwa Hizbullah (kundi la Mwenyezi Mungu) walio wema na Hizbush shaitwan (kundi la shetani) ambao ni "Tulaqa".Hii ni mikono yao iliyolowa kwa damu zetu, na midomo inachuruzika (inatona) kwa miili yetu, na ile ni miili toharifu na takasifu inayotekwa nyara na mbwa mwitu, na kuvamiwa na fisi.
Ikiwa umetuchukulia kuwa ghanima, utatupata karibuni kuwa ni magharimio, utakapokosa kuyapata ila tu yaliyoitanguliza mikono yako, **(Na wala Mola wako si mwenye kuwadhulumu waja (wake))**.Basi ni kwake mashtaka, naye ndiye mtegemewa.
Basi panga njama yako na fanya bidii yako, na jitahidi juhudi yako, lakini wallahi hautoweza kamwe kufuta kutajwa kwetu na wala kuuangamiza wahyi wetu, na wala kuudiriki upeo wetu, na wala hutoweza kujisafisha kutokana na fedheha (uliyoipata).
Rai yako si kitu zaidi ya ubovu, na siku zako hazina ila idadi chache, na kundi lako halina ila kutawanyika, siku ambayo atanadi munadi, “Tambueni kuwa la’ana ya Mwenyezi Mungu itawashukia walio madhalimu!!”
Basi Himidi yote ni Mwenyezi Mungu ambaye alimuishilizia wa mwanzo wetu aliyetutangulia, kwa sa’ada na maghfira, na wa mwisho wetu kwa shahada na rehma.
Tunamuomba Mwenyezi Mungu awakamilishie thawabu na awawajibishie kupata ziada, na atupe mahala pao walio wema, hakika Yeye ni mwenye huruma na Mpenzi (wa waja wake), naye ni mwenye kututosha na mbora wa kutegemewa.”

Yazid (la’anahullah) akasema:

يا صيحة تحمد من صوائح * ما أهون الموت على النوائح

Ajabu kilio cha kusifika cha waliaji
Ni wepesi ulioje wa mauti kwa wenye majonzi.

Mpokezi anasema: Kisha akawaomba ushauri watu wa Shamu kuwa awafanye nini.
Wakasema, “Usimchukue mtoto wa mbwa mbaya."
Nu’uman ibnu Bashir akamwambia, “Angalia ni nini alivyokuwa Mtume akiwatendea (mateka) nawe pia uwafanyie vivyo.

## YALIYOJIRI MTU MMOJA ALIPOMWAMBIA YAZID, NIPE HUYU MJAKAZI, AKIMKUSUDIA FATIMA.

Naye mtu mmoja katika watu wa Sham alimwangalia Fatima bintul Husein (a.s.) na kusema, “Ewe Amirul Mu-uminin nipe huyu mjakazi.”
Fatima akamwambia Shangazi yake “Ewe Shangazi!! Kwani nimekuwa yatima ili nifanywe mtumishi?”
Zainab (a.s.) akamwambia, “La, na wala huyu fasiki hana heshima yoyote.”
Yule mshami akasema, “Ni nani huyu mjakazi?”
Yazid (la’anahullah) akamwambia, “Huyu ni Fatima bintul Husein, na yule ni Shangazi yake, Zainab bintu Ali.”
Yule mshami akasema, "Husein ibnu Fatima na Ali ibnu Abi Twalib!!”
Akajibu, “Na’am.”
Mshami akasema, “Mwenyezi Mungu akulaani, ewe Yazid, Unakiuwa Kizazi cha Mtume wako na kuwafanya mateka

dhuria wake.Wallahi sikudhania ila kuwa wao ni mateka wa kutoka Urumi.
Yazid akasema, “Wallahi nitakuunganisha pamoja nao.”Kisha akaamuru kuwa akatwe shingo yake.

## **YAZID AMUAMURU KHATIBU KUKHUTUBU NA KUMUAMURU KUMTUKANA IMAM HUSEIN (A.S.) NA MAJIBU YA IMAM SAJJAD (A.S.).**

Mpokezi anasema:Yazid akamwita khatibu, na kumuamuru apande kwenye membar na kumtukana Imam Husein na Baba yake (aleihimas salaam).Akapanda kwenye membar na kumtusi Amirul Mu-uminin na Husein as-Shahid (aleihimas salaam) kwa aina za matusi, na kumsifu Mu’awiya na Yazid (aleihima la’ainullah).
Ali ibnil Husein (a.s.) akampazia sauti na kumwambia, “Ewe khatibu!! Umeinunua radhi ya kiumbe kwa hasira ya Muumba.Basi jiandalie makao yako huko motoni.”
Ibnu Sinan al-Khaffaji alifanya vema katika kumsifu Amirul Mu-uminin (a.s.) aliposema:

Je juu ya membar mnamtukana
ilhali mmesimamishiwa kwa upanga wake.

Mpokezi anasema: Kisha Yazid (la’anahullah) akamuahidi Imam Ali ibnil Husein (a.s.) katika siku hiyo ya kwamba atamtekelezea haja tatu.Kisha akaamuru kuwa wapelekwe kwenye nyumba ambayo ilikuwa haiwazuii kutokana na joto wala baridi, wakaishi huko kwa muda hata wakachubuka ngozi za nyuso zao.Na walikuwa katika muda walioishi katika mji tuliotaja, wakimuomboleza Imam Husein (a.s.).

## ALIYOYAONA BI SAKINA (A.S.) KWENYE NDOTO.

Sakina amesema, “Ilipokuwa siku ya nne ya makazi yetu niliota ndoto.” Kisha akataja ndoto ndefu ambayo mwisho wake anasema, “Nilimwona mwanamke akiwa amebebwa kwenye haodaj [1] na huku ameuwekelea mkono wake kichwani mwake, nikaulizia kumhusu, nikaambiwa, “Huyu ni Fatima bintu Muhammad (s.a.w.w.) Mama ya Baba yako.” Nikasema, “Wallahi nitamfuata, nikamwambiye tuliyofanyiwa.”
Nikaharakisha nikielekea upande aliokuwa, hadi kumfikia na kusimama mbele yake huku nikilia na kusema, “Ee Mama! Waliipinga wallahi haki yetu! Ee Mama! Waliuvunja wallahi umoja wetu! Ee mama! Walivunja wallahi harimu yetu! Ee mama! Walimuuwa wallahi Husein (a.s.) Baba yetu. Akasema, “Yatosha sauti yako, ewe Sakina umeikata mishipa ya moyo wangu, hii ni shati ya Baba yako, Husein (a.s.) sitengani nayo hadi nitakapokutana na Mwenyezi Mungu nikiwa nayo.”

## RA-ASUL JAALUT ASHANGAZWA NA WAISLAMU KUMUUWA MWANA WA BINTI YA MTUME WAO (S.A.WA.).

Ibni Lahi’ah amepokea kutoka kwa Abu aswad Muhammad ibnu Abdur Rahman, anasema, “Ra-asul Jaalut[2] alikutana nami na kusema: Wallahi, baina yangu na Dawud kuna mababu sabini, lakini mayahudi wanapokutana nami hunitukuza, nanyi hakuna baina ya Mwana wa Mtume wenu

[1]- Haodaj ni aina ya kiti mfano wa chumba kinachobebwa na ngamia ambacho hutumiwa kuwabebea wanawake.
[2] - Kiongozi wa dhehebu la kiyahudi.

na baina ya Mtume wenu ila baba mmoja, kisha mumemuuwa mwanawe.”

## ALIYOSEMA MFALME WA ROMA KUMWAMBIA YAZID BAADA YA KUKIONA KICHWA CHA IMAM HUSEIN (A.S.).

Na imepokewa kutoka kwa Imam Zainul A’bidin (a.s.) ya kwamba amesema, “Yazid alipokuwa akiletewa kichwa chake Husein (a.s.) alikuwa kwenye vikao vya kunywa pombe, kisha alikuwa akija na kichwa cha Husein (a.s.) na kukiweka mbele yake, na kunywa pombe juu yake.Siku moja alihudhuria kwenye kikao chake mjumbe wa mfalme wa Urumi, ambaye alikuwa ni katika watukufu wa Urumi na masharifu wake, akamwambiya: Ewe mfalme wa waarabu, hiki ni kichwa cha nani? Yazid akamwambia: Una umuhimu gani na kichwa hiki? Akajibu: Mimi nitakaporudi kwa mfalme wetu ataniuliza kuhusu kila kitu nilichokiona, nami ningependa kumjulisha kisa cha kichwa hiki na kumhusu mwenyewe, ili ashiriki nawe katika furaha yako.Yazid (aleihilla’ana) akamwambia: Hiki ni kichwa cha Husein ibni Abi Twalib (a.s.).

Mrumi akasema: Na ni nani mama yake? Akasema: Fatima binti ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).

Mnaswara akamwambia: Ole wako pamoja na dini yako.Mimi nina dini bora kuliko dini yako.Baba yangu ni katika wajukuu wa Dawuud (A.S.), na hata ingawa baina yangu naye kuna mababu wengi, manaswara wananitukuza na wanachukua udongo wa miguu yangu ili kupata baraka kwa kuwa mimi ni katika wajukuu wa Dawuud (a.s.).Nyinyi mnamuuwa mwana wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na hali ya kuwa baina yenu naye hakuna ila mama mmoja.Basi dini yenu ni dini ipi!?.

Kisha akamwambia Yazid: Umewahi kusikia habari za kanisa la Hafir?
Akasema: Sema ili nisikie.
Akasema:Baina ya Oman na China kuna bahari yenye umbali wa mwaka mmoja.Hakuna mji uliojengwa, ila mji mmoja katikakati ya maji, ambao upano wake ni farsakh thamanini katika farsakh thamanini, hakuna ardhini mji mkubwa zaidi yake, na kaafur na yaaqut hebebwa kutoka kwenye mji huo.Miti yao ni udi na ambary, na iko mikononi mwa manaswara (wakristo) wala hakuna ufalme wa wafalme ila ufalme wao.Katika mji huo kuna makanisa mengi, ambapo kanisa iliyokuu zaidi ni kanisa ya Hafir, ambayo kwenye mehrabu yake kuna gudulia la dhahabu liliyoningi'nizwa, ndani yake kuna ukwato .Wanasema kuwa, huu ni ukwato wa punda aliyekuwa akimpanda Isa (a.s.).Na wamelipamba lile gudulia kando yake  kwa dhahabu na Hariri. Katika kila mwaka maelfu ya wakristo huja kulizuru, na kulitufu na kulibusu na kuomba haja zao kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika sehemu hiyo.Hii ndiyo hali yao na maoni yao kuhusu ukwato wa punda, na wanadai kuwa ni ukwato wa punda aliyekuwa Isa (a.s.) akimpanda, Mtume wao, lakini nyinyi mnamuuwa Mwana wa Binti ya Mtume wenu, Mwenyezi Mungu asiwabariki wala asiibariki dini yenu.
Yazid akasema: Muuenu huyu mnaswara, asije akanifedhehesha nchini mwake.
Mnaswara (mkristo) alipohisi hatari hiyo akamwambia: Je unataka kuniuwa?
Akajibu: Na'am.
Akamwambia: Jua ya kwamba jana usiku nilimuona Mtume wenu kwenye ndoto, huku akisema: Ewe mnaswara, wewe ni katika watu wa peponi. Nikashangazwa na maneno yake, nami nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na ya kwamba Muhammad (s.a.w.w.) ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Kisha akakirukia kichwa cha Husein (a.s.) na kukikumbatia kifuani mwake na akawa ni mwenye kukibusu na kulia hadi alipouwawa.

## AL-MINHAL IBNI AMRU AKIWA PAMOJA NA IMAM SAJJAD (A.S.).

Mpokezi anasema: Zainul Abidin (a.s.) alitoka siku moja akitembea kwenye masoko ya Damaskas[1], al-Minhal bin Amru akamkabili na kumwambia “Umeshindaje, yabna Rasulillah!!”

Akasema, “kumekutwa huku tukiwa kama Bani Israil walivyokuwa kwa Aali Fir’aun, waliwachinja watoto wao wa kiume na kuwaacha hai wanawake zao.Ewe Minhal, kumekutwa huku waarabu wakijifakhiri kwa waajemi ya kwamba Muhammad ni mwarabu, nao wakureshi wakijifakhiri kwa waarabu wote wengine kuwa Muhammad anatokana nao.Na kumekutwa huku, sote Ahlul Bait tukiwa tumeporwa, tumeuwawa na tumekimbizwa, basi Inna lillahi wa inna ileihi raji’un (sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea) kutokana na hali ambayo mchana umekutwa tukiwa nayo.”

Mwenyezi Mungu amlipe kheri, Mahyar kwa alichosema katika shairi:

يعظمون له أعواد منبره * وتحت أقدامهم أولاده وضعوا

بأي حكم بنوه يتبعونكم * وفخركم أنكم صحب له تبع

Wanazitukuza mbao za membari yake
Wakawaweka wanawe chini ya miguu

[1] - Sham.

Ni kwa ulazima gani wanawe wawafuate
Na mwajifakhiri kuwa sahaba wamfataye

## YAZID AMWITA IMAM SAJJAD (A.S.) NA KUMWAMBIA ATAJE HAJA TATU.

Siku moja Yazid (aleihi la'ainullullah) alimwita Ali ibnil Husein (a.s.) na Amru ibnil Hasan[1] (a.s.) - na Amru wakati huo alikuwa mchanga, inasemekana alikuwa miaka kumi na moja- kisha akamwambia, "je utapigana mweleka na huyu?" Yaani mwanawe Yazid aitwaye Khalid.
Basi Amru akamwambia, "La, lakini nipe kisu, naye (pia) mpe kisu, kisha nipigane naye."
Yazid (la'anahullah) akasema:

شنشنة أعرفها من أخزم * هل تلد الحية إلا الحية

Ada ya Akhzam ninayoijua
Nyoka hamzai ila nyoka.

Kisha akamwambia Ali ibnil Husein (a.s.), "Taja haja zako tatu nilizokuahihidi kukidhia."
Akamjibu, "Ya kwanza, ni kwamba unionyeshe uso wa Seyyid wangu na Bwana wangu na Baba yangu, Husein (a.s.) ili nguvu na utulivu kwa kuutazama.Na ya pili,ni kwamba uturudishie tuliyopokonywa.Na ya tatu, ya kwamba, ikiwa unaazimia kuniuwa, basi mtume pamoja na hawa wanawake atakayewarudisha kwenye Haram ya Babu yao (s.a.w.w.)."
Akajibu, "Ama uso wa Baba yako, hautauona kamwe.Na ama kuhusiana na kukuuwa, mimi nimeshakusamehe.Na ama wanawake hakuna atakayewarudisha huko Madina ila wewe.

[1] - Kwenye nuskha nyingine imeandikwa Amru ibnil Husein.

Na ama yaliyochukuliwa kutoka kwenu, nitawapa badala yake yenye thamani maradufu zaidi yake."
Akamjibu, "Ama mali yako, sisi hatuna haja nayo, ni yako mwenyewe.Bali niliitisha yaliyochukuliwa kutoka kwetu kwani miongoni mwake kuna kitambaa kilichofumwa na Bibi Fatima bintu Muhammad (s.a.w.w.) na hijabu yake ya kichwani na ushanga wake na nguo yake."
Akaamuru kuwa virudishwe na kuzidisha dinari mia mbili kutoka kwake, Imam Zainul Abidin (a.s.) akazichukua na kuzigawanya baina ya mafukara.

## MATEKA WAONDOKA SHAM NA KUFIKA KATIKA MJI WA IRAQ KISHA KWENDA KARBALA.

Kisha akaamuru kuwa mateka wa Imam Husein (a.s.) warudishwe kwao mjini wa Madinatur Rasul (s.a.w.w.).
Na ama kichwa cha Imam Husein (a.s.) imepokewa kuwa kilirudishwa na kuzikwa Karbala pamoja na mwili wake mtukufu, na mashia kwa ujumla wamekuwa wakitenda kufwatana na riwaya hii iliyotajwa.
Na kumepokewa riwaya nyingi ambazo hatukuzitaja, tumeacha kuzitaja ili yasitanguke tuliyoahidi, yaani kuandika kitabu hiki kwa mukhtasari.
Mpokezi anasema: Wanawake wa Imam Husein (a.s.) na iyali wake waliporudi kutoka Sham na kufika Iraq, walimwambia dalali wao, "Tupitishie kwenye njia ya Karbala."
Walipofika mahala alipouwawa Imam Husein (a.s.), walimkuta Jabir ibni Abdillah al-Answari pamoja na kikundi cha Bani Hashim nabaadhi ya wanaume wa Aali Rasulillah (s.a.w.w.) wakiwa wamekuja kuizuru kaburi ya Imam Husein (a.s.), wakawa wamefika kwa wakati mmoja na kukutana kwa kilio na huzuni na kwa kujipiga vifua na mashavu.Wakafanya maombolezi yenye kujeruhi maini,

wakakusanyika pamoja nao wanawake wa vijiji vya karibu na maeneo hayo, wakabaki katika maombolezo hayo kwa muda wa masiku.

## MAJINI WAMUOMBOLEZA IMAM SAJJAD (A.S.).

Na imepokewa kutoka kwa Abi Habbab al-Kalbi, ya kwamba alisema: Watu wanaofanya kazi ya kupaka chokaa wametuhadithia kwa kusema:? Tulipokuwa tukitoka al-Jibbana wakati wa usiku alpouwawa Husein (a.s.), tukawasikia majini wakimuomboleza huku wakisema:

مسح الرسول جبينه          فله بريق في الخدود

أبواه من أعلى قريش       و جده خير الجدود

Mtume alikipangusa kipaji chake
anameremeta kwenye mashavu yake

Na Babu yake ni mbora wa mababu
Wazazi wake ni masharifu wa makureshi.

## MATEKA WAIACHA KARBALA NA KUELEKEA MADINA, KISHA BISHRU AMWOMBOLEZA IMAM HUSEIN (A.S.).

Mpokezi anaendelea kusimulia: Kisha waliondoka wakielekea mji wa Madina.
Bashir ibnu Jadhlim anasema, "Tulipokaribia huko, Ali ibnil Husein (a.s.) alitua na kusimamisha hema yake, kisha akawateremsha wanawake na kusema, "Ewe Bishru,

Mwenyezi Mungu amrehemu baba yako, alikuwa mwanashairi, je una uwezo wa kusoma kitu katika ushairi huo?"
Akajibu, "Ndio yabna Rasulillah (s.a.w.w.) mimi ni mwanashairi."
Imam (a.s) akasema, "Ingia katika mji wa Madina umuomboleze Abu Abdillah (a.s.)"
Bishru anasema, "Basi nilimpanda farasi wangu nikakimbia hata kuingia mji wa Madina.Nilipofika msikiti wa Mtume (s.a.w.w.) nikapaza sauti yangu kwa kilio na kusema:

يا أهل يثرب لا مقام لكم بها　　　قُتل الحسين فادمعي مدرارُ

الجسم منه بكربلاء مضرجُ　　　و الرأس منه على القناة يدارُ

Enyi wakazi wa Yathrib hakuna makazi kwenu
Husein ameuwawa mlilieini kwa machozi mengi

Mwili wake umelowa kwa damu huko Karbala
kichwa kimetungikwa mkukini chazungushwa.

Anaendelea kusema: Kisha nikasema, "Huyu ni Ali ibnil Husein (a.s.) pamoja na mashangazi wake na dada zake wamefika kwenye maeneo yenu na wametua kwenye mji wenu, nami ni mjumbe wake kwenu, ili niwajulisheni mahala alipo."
Anaendelea kusema, "Basi hakukubaki kwenye mji wa Madina mwanamke asiyetoka nyumbani kwake wala mwenye kujisitiri kwa hijabu ila tu walitoka kwenye nyumba zao huku wakiwa wamezifunua nyele zao wakiwa wanazikwaruza nyuso zao na wakiyapiga mashavu yao na kuwambea (madhalimu) hilaki na maangamizo.Basi

sikuwahi kuona wenye kulia zaidi kuliko siku hiyo, na wala siku yenye machungu kwa waislamu zaidi ya siku hiyo."

## MJAKAZI AMUOMBOLEZA IMAM HUSEIN (A.S.).

Na nilimsikia mjakazi mmoja akimuomboleza Imam Husein (a.s.) kwa kusema:

Muombolezaji alimlilia Bwana wangu akanitia machungu
Akanifanya mgonjwa muombolezaji akanitia machungu
Enyi macho nikirimuni kwa machozi muyatoe kwa wingi
Kisha mnikirimu kwa machozi zaidi baada ya machozi yenu
Kumlilia ambaye msiba wake uliitetetemesha arshi ya Mola
Na kuuwawa kwake kuliitia kasoro dini na utukufu
Kumlilia Mwana wa Mtume na Mwana wa Wasii wake
Hata kama makazi yake ni ya mbali kutokana nasi

Kisha Yule mjakazi akasema, "Ewe muombolezaji umeirudisha upia huzuni yetu ya Abu Abdillah (a.s.) na kuvikwaruza vidonda vyetu ambavyo vilikuwa bado havijakauka.Wewe ni nani, Mwenyezi Mungu akurehemu?" Nikajibu, "Mimi ni Bishru ibnu Jadhlam.Bwana wangu, Ali ibnil Husein (a.s.) amenituma huku, naye ametua katika sehemu fulani pamoja na ayali wake Abu Abdillah (a.s.) na wanawake zake."

## WATU WAMTOLEA RAMBIRAMBI IMAM SAJJAD (A.S.), KISHA IMAM AWAKHUTUBIA.

Mpokezi anaendelea kusimulia:Waliniacha mahala pangu na kuharakisha kwenda huko, nami nikampiga farasi wangu na kurudi walilipokuwa Ahlul Bait, nikawakuta watu wakiwa wameshajaa kwenye njia na sehemu zote.Basi nikashuka kutoka kwenye farasi wangu, na kuwapita watu wote hadi

nilipoikurubia mlango wa hema.Ali ibnil Husein (a.s.) alikuwa ndani, akatoka na huku ana tambara alilokuwa akilipanguzia machozi yake, na nyuma yake kuna mtumishi aliyekuwa na kiti, akakiweka mbele yake, akaketi huku ameshindwa kujizuia na kilio.Watu wakaangua kilio na sauti za kilio cha wanawake na majakazi zikaenea, huku watu toka pande zote wakimpa rambirambi zao.Seheme hiyo ikaangua kwa kilio kikubwa.
Aliwaashiria kwa mkono wake ya kwamba wanyamaze, kilio chao kikatulia, kisha akasema:

“Himidi yote ni ya Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu, Muumba wa viumbe wote, aliyembali akanyanyuka katika mbingu za juu, na amekurubia akashuhudia manong'onezo ya nafsi. Twamhimidi kwa mambo haya yalio adhimu, na kwa misiba ya zama, na machungu ya misiba, na kwa makali ya balaa, na kwa uzito wa majonzi, na kwa uzito wa misiba mikubwa iliyoenea, yenye kushuka na kuangamiza.
Enyi watu, hakika Mwenyezi Mungu aliyetukuka - na Himidi yote ni yake - ametufanyia mtihani kwa kwa misiba mizito na kwa pengo kubwa katika uislamu. Abu Abdillah al-Husein (a.s.) ameuwawa pamoja na kizazi chake, na wanawake zake na wanawe wamefanywa kuwa mateka, na walikizungusha kichwa chake kwenye miji kikiwa kimetungikwa juu ya mkuki, na huu ni msiba usiokwa na mfano wake.
Enyi watu! Ni nani kati ya wanaume wenu watapatwa na furaha baada ya kuuwawa kwake? Au ni moyo upi hutopatwa na huzuni kwa ajili yake? Na ni jicho lipi kati yenu linayazuia machozi yake na kuyabana yasitiririke?!
Basi tambueni, kuwa mbingu saba zilizokakamaa zimelia kwa ajili ya kuuwawa kwake, na bahari zimelia kwa mawimbi yake, na mbingu kwa nguzo zake, na ardhi kwa pembezoni zake, na miti kwa matawi yake, na samaki wote

walioko ukingoni mwa mabahari, na Malaika mukarrabina, na wakazi wote wa mbinguni.
Enyi watu, ni moyo upi usioumia kwa mauaji yake, na ni moyo upi usiyomtamani, au ni sikio lipi litasikia kuhusu pengo hili lililoupata uislamu kisha likakosa kupatwa na uziwi.
Enyi watu, tumefukuzwa, tumekimbizwa, tumetupwa mbali na miji yetu, kana kwamba sis ni wana wa Uturuki na Kabul, bila ya kuwa tumefanya hatia yoyote, au kufanya kosa lolote, au kuwa tumeingiza pengo kwenye uislamu (hatukusikia hili katika babu zetu waliotangulia, halikuwa hili ila uzushi).
Wallahi, lau kama Mtume angekuwa amewaamuru kutuuwa kama alivyokuwa amewausia kutuhusu sisi (watufanyie wema), hawangezidisha zaidi ya walivyotufanyia, basi inna lillahi wa inna ileihi raji'un (hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na hakika kwake tutarejea) kwa msiba ambao kwa hakika ni mkubwa, wenye kuumiza na kusikitisha na (ambao ni) mzito na wenye kuenea na wenye chungu na wenye kuangamiza.
Basi kwa Mwenyezi Mungu twaweka matarajio yetu kwa yale yaliyotusibu na yaliyotufikia, kwani hakika Yeye ni Azizi Mwenye kulipiza kisasi."

## SWAUHAN IBNI SWA’ASWA’A AMUOMBA IMAM (A.S.) AMUWIYE RADHI.

Mpokezi wa habari hizi anasema: Swauhan ibni Swa'aswa'a ibni Swauhan - aliyekuwa ameptawa na ugonjwa usiopona- akasimama na kumuomba Imam (a.s.) amuwiye radhi kwa ugonjwa aliokuwa nao miguuni usiopona.Akamjibu kwa kumuwiya radhi, na kumdhania vyema na kumshukuru na kumwombea rehma baba yake.

## ALIYOSEMA SEYYID IBNI TWAAWUS KATIKA KHATIMA YA KITABU CHAKE KUHUSU KUOMBOLEZA KWA NYUMBA NA MAJENGO KWA AJILI YA KUWAPOTEZA WENYE KUZIHAMI.

Ali ibni Musa ibni Ja'afar ibni Muhammad ibni Twawus mwandishi wa kitabu hiki anasema: Kisha Imam (a.s.) alisafiri pamoja na ahli zake na ayali wake hadi Madina na kuziangalia nyumba za watu wake na rijali wake, akazipata nyumba hizo ni kana kwamba zinalia, kwa lugha ya hali yazo, na kudhihirisha, kwa kumwaga machozi na kuyatiririsha, kuwakosa watu waliokuwa wakizihami na rijali wake, na kuwaomboleza mfano wa kuomboleza kwa wajane, huku zikiwaulizia kutoka kwa watu wanaoishi kando ya mapito ya maji, na huku zikichemkwa na huzuni kwa kushuhudia sehemu za kuuwawa kwao, kisha zikanadi katika kuwaomboleza:Waa thakla!! (Woi nimefelewa!!)
Na kusema,"Enyi watu wangu nipeni auni katika kuomboleza na kulia, na nisaidieni kuustahamili msiba huu ulio adhimu, kwani watu ninao waomboleza kwa kuwakosa, na walikuwa kitulizo cha usiku kuzitamani tabia zao kiramu, wangu na mchana wangu, na nuru za giza langu na katika ukungu wa alfajiri, na kamba za sharafa yangu, na fakhari yangu, na sababu za nguvu yangu na ushindi wangu, na kizazi kilichobaki cha Jua zangu na Miezi yangu[1]. waliukimbiza Ni nyusiku ngapi kwa kunikirimu kwao upweke wangu, na kwa kunineemesha kwao wakaiinua heshima yangu, na wakanifanya kusikia mazungumzo yao ya siri na Mola wao katika macheo ya alfajiri, na kunionjesha utamu wa kuzihifadhi siri zao.

---

[1] - Anamkusudia Mtume na Ahlul Bait (swalawatullah aleihim) ambao ndio Jua na Miezi kutokana na wingi wa Nuru yao.

Na ni siku ngapi waliimarisha kwa vikao vyao robo yangu, na kuitia marashi maumbile yangu kwa fadhila zao, na kulikuza tawi langu majani kwa maji ya ahadi zao, na kuniondolea bahati yangu mbaya kwa kukua kwa saada yao. Ni kiasi gani cha sifa njema walizipanda ndani yangu, na kunichungia mahala pangu kutokana na balaa.

Na ni kiasi gani nimekuwa na sharafa zaidi ya nyumba na kasri nyinginezo na kujivuna kwa vazi la furaha na sururi.

Na ni kiasi gani cha zama zisizokuwa na uhai wamehuisha katika mapito yangu, na kiasi gani kwenye kizingiti changu wamewaokoa wengi kutokana na hatari ya mauti.

Basi kwa ajili yao mshale wa mauti ukanielekea, na hukumu ya masiku ikanihusudu, wakawa gharibu baina ya maadui na hadafu za mishale ya maadui, na mema yakakatwa kwa kukatwa ncha za vidole vyao, na fadhila zikashitakia kwa kuikosa miili yao, na mazuri yakaondoka kwa kuondoka kwa viungo vyao, nazo hukumu za kiislamu zinaomboleza kutokana na upweke wa makazi yao.

Basi ni ajabu iliyoje, kwa kumwagwa damu ya uchaMungu katika vita hivyo, na kwa kushushwa bendera ya ukamilifu katika magumu hayo.

Hata ukikosekana msaada wa wenye akili na ujahili wa hizo akili ukakosa kuninusuru katika misiba huu, nitajituliza kwa sunna zilizoachwa na nyota zilizodidimia,kwani hizo zinaomboleza kama kuomboleza kwangu na kuhuzunika kama kuhuzunika na kuteseka kwangu.

Basi lao kama mungesikia vipi swala zinawaomboleza na kuwalilia, na mtu anayekaa upwekeni anavyowatamani, na mkusanyiko wa fadhila ulivyo na hamu nao, na vikao vya watukufu vinavopatwa nautulivu kwa kuwa nao, na mihrabu za misikiti zinavyowalilia, na michirizi ya moyo inavyowanadi, kungewaliza kukisikia kilio hicho kilichoshukia, na mngelijua makosa yenu katika huu msiba uliotuenea.

Bali, lao kama mngeiona huzuni yangu na majonzi yangu na upweke wa vikao vyangu na athari zangu, mngeliona kinachouumiza moyo wenye wa subira nyingi na kinachozichemsha huzuni za vifuani, kwani, hakika nyumba nyinginezo zilizokuwa zikinihusudu zimekwisha furahia msiba wangu, na mikono ya khatari imeninyakua.
Basi ni shauku iliyoje, niliyonayo kwa nyumba waliyoishi ndani yake, na mapito ya maji walipoishi na kupafanya makazi yao, laiti nilikuwa mwanadamu niwahami kutokana na kukatwa kwa mapanga, na kuwazuia kutokana na makali ya kifo, na kuingilia kati yao na watu wenye chuki nao, na kuwakinga kutokana na mishale ya uadui.
Basi kwa kuwa nimekosa utukufu wa kutoa rambirambi zilizo wajibu juu yangu, kwa nini nisiwe mahala pa kuihifadhi miili yao dhaifu, na mwenye kustahiki kuyahifadhi maungo yao kutokana na balaa, na mwenye kuhifadhika kutokana na khofu ya kugurwa na kuachwa.
Basi ole, kisha ole, lao kama ningekuwa kaburi kwa miili hiyo na makazi kwa nafsi hizo tukufu za hao wakarimu, ningelitoa juhudi zote katika kuzihifadhi, na ningelitekeleza ahadi za tangu, na kuzilipia baadhi ya haki za awali, na kuzililinda kwa juhudi zote kutokana na machungu ya miamba hiyo, na kuzihudumia kuhudumia kwa mja mtiifu, na ningezitolea juhudi za mwenye uwezo, na kuzitandazia hizo shavu na hivyo viungo busati la utukufu na heshima, na ningefikia matumaini yangu ya kuzikumbatia, na kulinawirisha giza langu kwa kuangaza kwao.
Basi ni shauku iliyoje, niliyo nayo ya kufikia matumaini hayo, na ni wasiwasi ulioje niliyo nao kwa kughibu kwa watu wangu na wakazi wangu.Kila uchu ni duni kuliko uchu nilio nao, na kila dawa ghairi yao hainitibu.Kwa hakika nimekwisha vaa kwa kuwakosa mavazi ya huzuni, na kuzoea baada yao nguo za maombolezi, na nimekata tama ya kuwa

na uvumilivu na subira, nikasema: Ewe majonzi ya siku zote, miadi yako ni siku ya ufufuo.
Na amefanya vema Ibnu Qittah (rahmatullah aleihi)) alipozililia hizo nyumba zilizoashiriwa kwa kusema:

مررت علــى أبيــات آل محمــد * فلــم أرهــا أمثالهــا يوم حُلــتِ

فلا يُبعــد الله الديـــار وأهلهـــا * وإن أصبحت منهم برغمي تخلت

ألا إن قتلــى الطــف مـن آل هاشم * أذلــت رقاب المسلميـــن فذلــتِ

وكانوا غياثاً ثم أضحــوا رزيـــة * لقد عظمــت تلك الرزايا وجلــتِ

**ألم تر أن الشمس أضحــت مريضــة * لفقــد حسين والبلاد اقشعـــرتِ**

Nimezipitia nyumba za Aali Muhammad
Sikuziona kama zilivyokuwa zilipoingiwa

Mola asiziweke nyumba mbali na wakazi wake
Hata ingawa - sio matakwa yangu – wamezihama

Hakika watu wa Twaffu katika Aali Hashim kuuliwa
Kuliwadhalilisha waislamu wakawa madhalili

Walikuwa wasaidizi kisha wenyewe wakawa msiba
Hakika ni adhimu hiyo misiba ni mikubwa kweli

Je huoni kuwa jua hili limepatwa na maradhi
Kwa kumpoteza Husein na nchi zote kutetema

Ewe uliyeusikia msiba huu ufwate mfano bora wa wanaoshikamana na kitabu.

Imepokelewa kuhusina na Imam Zainul Aabidin (a.s.) – hata ingawa alifanya upole usiyoweza kusifika – ya kwamba alikuwa mwingi wa kulia kwa misiba hiyo iliyowashukia, na mwingi wa kushitakia.

## IMAM SAJJAD (A.S.) AMUOMBOLEZA BABAKE ALIYEUWAWA SHAHIDI.

Na imepokelewa kutoka kutoka kwa Imam Swadiq (a.s.) ya kwamba alisema, "Zainul Aabidin (a.s.) alimlilia Baba yake miaka arobaini, akifunga mchana na kukesha usiku katika ibada, na unapomfikia wakati wa kufuturu mtumwa wake alikuwa akimletea chakula chakula na kinywaji chake na kuviweka mbele yake na kusema: Kula ewe Bwana wangu.Naye alikuwa akisema:Mwana wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliuwawa akiwa mwenye njaa, Mwana wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliuwawa akiwa mwenye kiu.Na aliendelea kukariri ksema vivyo, huku akilia hadi kinalowa chakula chake kwa machozi yake na kinywaji chake kuchanganyika na machozi yake.Aliendelea katika hali hii hadi aliporudi kwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka na Alitakasika."
Mtumwa katika watumwa wake Imam Zainul Aabidin (a.s.) anahadithia kuwa siku moja Imam (a.s.) alienda jangwani, kisha anasema: Basi nikamfwata, nikamkuta akiwa amesujudu juu ya jiwe gumu, nikasimama huku ninakusikia kupuma kwake na kulia kwake, nikamhesabu mara elfu akisema:

لا إله إلا الله حقاً حقاً لا إله إلا الله تعبداً ورقاً لا إله إلا الله إيماناً وصدقاً

Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah, kwa haki, " kwa haki. Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah, (nashuhudia hivi) katika hali ya uja na utumwa. Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah, (nashuhudia hivi) "katika hali ya imani na kusadiki.

Kisha akaiinua kichwa chake kutoka kwenye sijda, na huku ndevu zake na uso wake vimelowa kwa machozi.

Nikamwambia: Ewe Bwana wangu, je haujafika wakati wa huzuni yako kufikia kikomo?.

Akanijibu: Ole wako! Hakika Yaaqub ibni Is-haq ibni Ibrahim (aleihimus salaam) alikuwa Mtume, mjukuu wa Mtume na mwana wa Mtume, alikuwa na wana kumi na wawili, kisha Mwenyezi Mungu aliyetukuka, akamfanya mmoja kati yao kughibu, basi nywele zako zikawa nyeupe kwa huzuni, na mgongo wake kupinda kwa ghamu na hamu, na macho yake kupotea kwa kulia, na hali ya kuwa (mwanawe[1]) yuko hai katika dunia hii. Ama mimi, nimemuona Baba yangu na ndugu yangu na watu kumi na saba katika Ahlu beiti zangu wakiwa wameangushwa na kuuwawa, basi vipi huzuni yangu itafikia kikomo na kilio change kupungua?

Na hapa nitamathili na kuwaashiria (swalawatullahi wa salamuhu aleihim) katika shairi lisemalo:

**من مخبر الملبسينـــا بانتزاحهـــم * ثوباً من الحزن لا يبلـــى ويبلينـــا**

**إن الزمان الذي قــد كان يضحكنـــا * بقربهم صار بالتفريـــق يبكينـــا**

**حالت لفقدانهم أيامنـــا فغـــدت * سوداً وكانت بهم بيضـــاً ليالينـــا**

Ni nani atawajulisha ambao kuondoka kwao kumetuvisha
Vazi la huzuni lisilochanika kulivaa bali sisi latuchanisha

[1] - Yaani Nabii Yusuf (a.s.).

Hakika wakati ambao ulituchekesha na (kutufurahisha)
Kuwepo kwao umekuwa kwa kutengana nao watuliza
Michana yetu kwa kuwakosa imebadilika na kupata kiza
Ambapo kuwepo kwao nyusiku zetu zilikuwa mwangaza

Na hapa ndipo kikomo cha tuliyotaka na mwisho wa tuliyokusudia.Basi mwenye kuifahamu taratibu ya kitabu hiki na mpangilio wake pamoja na mukhtasari wake (katika kunukuu mambo yaliyojiri) na hajmu yake ndogo, atatambua tofauti iliyoko baina yake na vitabu vinginevyo vyenye maudhuu haya, na atatambua ubora wake juu ya vitabu hivyo.
Himidi yetu nay a Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu, kisha swala na salamu zimshukie Mtume Muhammad na Aali zake waliowema na walio watoharifu.

# MAMBO YA AJABU YALIYODHIHIRI BAADA YA IMAMHUSEIN (A.S.) KUUWAWA SHAHIDI.

## MAMBO YA AJABU YALIYODHIHIRI BAADA YA IMAM HUSEIN (A.S.) KUUWAWA SHAHIDI.

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu.
Himidi yote ni ya Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu, kisha swala na salamu zimshukie Mjumbe wake, ambaye ni Mtume, Muonyaji, na Muaminifu, pamoja na Aali zake, Mabwana, walio watukufu.
Dhalimu vyovyote atakavyo kuwa mwenye nguvu na vyovyote akavyokuwa na wasaidizi wengi, na vyovyote atakavyo baki hai, uhakika ni kwamba, yeye ni dhaifu, kwani anayekabiliana naye ni Mwenyezi Mungu (s.w.t.) mwenye Nguvu zote, naye – Aliyetukuka na Aliyetakasika – daima ni mwenye kuwavizia madhalimu na waovu, atawaadhibu na kuwateremshia aina za balaa humu duniani na huko akhera. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa hukmu ya Mwenyezi Mungu kwa wale waliomdhulumu Imam Husein (a.s.) na kumuuwa na kumvunjia heshima yake, aliwaonjesha adhabu na balaa humu duniani na siku ya Qiyama adhabu yao itakuwa kali na yenye uchungu zaidi.
Mwenyezi Mungu daima ni msaidizi kwa madhulumu waliodhulumiwa katika njia ya kuitetea haki na katika kuinyanyua dini yake, na kwa sababu hii alidhihirisha kudhulumiwa kwao hapa duniani na akaonyesha kwamba wao ndio wenye haki na ya kwamba waliowadhulumu watadumbukizwa kwenye kina cha jahannam, na kuishi huko milele,kwa hakika ni maishilio yaliyo mabaya.
Baada ya Imam Husein (a.s.) kuuwawa shahidi, Mwenyezi Mungu aliyadhirisha mambo mengi ya ajabu yaliyoshuhudiwa na watu wote na kuwafikia yakini.Mambo yaliyo kuwa yakionyesha haki aliyokuwa nayo Imam Husein (a.s.) na cheo chake cha juu mbele ya Mwenyezi Mungu,

yeye pamoja na maswahaba wake waliouwawa shahidi pamoja naye, na ndio sababu kumbukumbu zao na majina yao yakabaki milele, na mfumo wao ukabaki unafwatwa na watu wote wa ulimwengu wenye dhamiri zilizo huru katika karne zote zilizokuja baada yao, na watabaki hivi hadi Mwenyezi Mungu atakapomdhihirisha al-Qaim wa Aali Muhammad (Mwenyezi Mungu aiharakishe faraja yake) atakayekilipiza kisasi chake Imam Husein (a.s.).
Hapa tutataja baadhi ya mambo ya ajabu yaliyotokea baada ya Imam Husein (a.s.) kufa shahidi, yaliyotajwa kwenye vitabu vya madhehebu yote ya kiislamu:

1. Kichwa cha Imam Husein (a.s.) chazungumza kwa kutumia aya za Qurani, kikiwa katika hali ya kutungikwa juu ya mkuki.

*Miftahun najaa fi manaqibil a'baa:135, al-Khaswaisul kubra: 2/127, alKawakibud durriyya: 57, Is-a'fur raghibin: 218, Nurul abswar: 125, Ihqaqul haq: 11/452-453.*

2. Imam Husein (a.s.) aliitupa damu yake juu mbinguni na wala hakuna tone hata moja lililomwagika ardhini.

*Kifayatut twalib: 284, Ihqaqul haq: 454.*

3. Imam Husein (a.s.) alipouwawa mbingu ilinyesha mvua ya damu, watu na vitu vyote vikalowa kwa damu, na athari ya damu ikabaki kwenye nguo zao kwa muda wote hadi zilipozeeka na kuchanika, na wekundu huu unaoonekana mbinguni ulidhihiri katika siku alipouwawa na wala hukuwahi kuonekana kabla yake.

*Maqtalul Husein: 2/89, Dhakhairul uqba: 144-145 na 150, Tarikhu dimishq-kama ilivyo katika "Muntakhabu yake"- :4/339, as-Swawai'qul muhriqa: 116 na 192, al-Khaswaisul kubra: 127, Wasilatul ma-aal: 197, Yanabi'ul mawadda: 320 na356, , Nurul abswar:123, al-Ittihaf bihubbil ashraf:12, Tarikhul islam:2/349,Tadhkiratul khawass:284, Nadhmu duraris simtwain:220, Ihqaqul haq:11/458-462.*

4. Kila jiwe duniani lilipoinuliwa katika siku alipokufa shahidi Imam Husein (a.s.) kulipatikani chini yake damu mbichi.

*Tadhkiratul khawass:284, Nadhmu duraris simtwain:220,Yanabi'ul mawadda:320 na 356, Tarikhul islam:2/349,Kifayatut twalib: 29, al-Ittihaf bihubbil ashraf:12,Is-a'fur raghibin:215, as-Swawai'qul muhriqa:116 na 192, Miftahun najaa:makhtut( yaani nuskha iliyochapishwa kwa khati ya mkono),Tafsiru ibni kathir 9/162, Ihqaqul haq:11/462 na 481- 483.*

5. Kichwa cha Imam Husein (a.s.) kilipoletwa darul imara (ikulu) kuta zilionekana zinachuruza kwa damu.

*Dhakhairul uqba: 144, Tarikhu dimishq-kama ilivyo katika "Muntakhabu yake":4/339, as-Swawai'qul muhriqa: 192, Wasilatul ma-aal: 197, Yanabi'ul mawadda: 322, Ihqaqul haq: 11/463.*

6. Imam Husein (a.s.) alipouwawa shahidi mbingu ilibadilika na kuwa nyekundu, na kubaki siku nyingi kama pande la damu.Mbingu ilikuwa ni kana kwamba imepatwa na ugonjwa.

*Almu'ujamul kabir: 145, Majma'uz zawaid: 9/196, al-Khaswaisul kubra: 2/127, Ihqaqul haq: 11/464.*

7. Imam Husein (a.s.) alipouwawa shahidi watu walibaki siku saba wanaposwali alasiri kisha wakilitazama miali ya jua kwenye kuta waliona kuwa ni kana kwamba ni blanketi nyekundu, na walipozitazama syari za mbinguni waliziona kana kwamba zinagongana zenyewe kwa zenyewe.

*Almu'ujamul kabir: 146, Majma'uz zawaid: 9/197, Tarikhul islam: 2/348, Siyaru a'alamin nubalaa:3/210, Tarikhul khulafa:80, as-Swawai'qul muhriqa: 192, Is-a'fur raghibin:251, Ihqaqul haq: 11/465-466.*

8. Imam Husein (a.s.) alipouwawa shahidi watu walibaki miezi miwili au mitatu kana kwamba kuta zimepakwa damu, siku zote toka wakati wa swala ya alfajiri hadi kughibu kwa jua.

*Tadhkiratul khawass: 284, alKamil fit tarikh: 3/301, alBidaya wan nihaya: 8/171, alFusulul muhimma: 179, Akhbarud duwal: 109, Ihqaqul haq: 11/466-467.*

9. Imam Husein (a.s.) alipouwawa pembezoni mwa mbingu kukawa kwekundu, ambako ni alama ya kilio cha mbingu.Manjano waliyaipora kutoka kwa Imam Husein (a.s.) ilibadilika na kuwa jivu, pia walimchinja ngamia wa kike waliomchukua kutoka kwenye kambi ya jeshi la Imam Husein (a.s.) lakini walipotaka kumla wakapata kuwa nyama zake zinaotoa moto.

*Maqtalul Husein: 2/90, Tarikhul Islam: 2/348, Siyaru a'alamin nubalaa: 3/311, Tafsirul Quran libni kathir: 9/162,*

10. Imam Husein (a.s.) alipouwawa mbingu yote, kwa upeo wa macho, ilikuwa nyekundu, na kuwa kama damu, kwa miezi sita.

    *Tarikhul Islam*: 2/348, *Siyaru a'alamin nubalaa: 3/ 210, as Sawaiqul muhriqa: 192, Majma'az Zawaid: 9/197, Tarikhul Khulafaa: 80, Miftaahun najaa, Yanaabi'ul Mawaddah: 322, Is-a'fur raghibin: 215, Ihqaqul haq: 11/469-470.*

11. Mbingu haikuwahi kuwa nyekundu hadi Imam Husein (a.s.) alipouwawa, na kila mwanamke katika utawala wa kirumi alipopatwa na hedhi alipatwa na ugonjwa wa ukoma, mfalme wa urumi akamwandikia mfalme wa waarabu, na kumwambia: Je mumemuuwa Nabii au Mwana wa Nabii?

*Almu'ujamul Kabir: 146, Maqtalul Husein: 2/90, Almahaasin wal Masaawi: 62, Tarikhu dimishq: 4/ 339, Tarikhul Islam: 2, p.348, Siyaru a'alamin nubalaa: 3/211, as Sawaiqul muhriqa: 192, Majmauz zawaaid: 9/l97, Muntakhabu kanzul ummaal: 5/112, Yanaabi'ul mawaddah: 322-356, Miftaahun najaa: almakhtut (yaani nuskha iliyochapishwa kwa khati ya mkono), Ihqaqul haq: 11/ 471-473.*

12. Imam Husein (a.s.) alipouwawa dunia ilipatwa na giza kwa siku tatu, kisha wekundu ukadhihiri

mbinguni, na kila aliyeigusa zaafarani ya Imam Husein (a.s.) aliungua.

*Tadhkiratul khawass: 283, as Sawaiqul muhriqa: 192, Nadhmu duraris simtwain: 220, Miftaahun najaa: almakhtut (yaani nuskha iliyochapishwa kwa khati ya mkono), Nurul Abswaar: Tarikhu dimishq* 4/339, *Ihqaqul haq: 11/ 474-475.*

13. Mbingu haikumlilia yeyote ila watu wawili: Nabii Yahya ibnu Zakariya na Imam Husein (a.s.).

    Kulia kwa mbingu ni kwa kupatwa na wekundu na kubadilika kuwa kama ngozi nyekundu.

*Tarikhu dimishq: 4/339, Kifayatut twalib: 289, Siyaru a'alamini nubalaa: 3/210, Tadhkiratul khawass: 283, Nadhmu durarus simtwain: 220, as Sawaiqul muhriqa: 192, Miftaahun najaa: almakhtut (yaani nuskha iliyochapishwa kwa khati ya mkono), Yanaabi'ul mawaddah: 322, Nurul Abswaar: 123, Tafsirul Qur'an ya ibnu Kathir, Ihqaqul haq: 11/ 476-478.*

14. Imam Husein alipouwawa jua lilishikwa, kushikwa ambako kulizifanya sayari za mbinguni kudhihiri katika nusu ya mchana, watu wakadhani kuwa Qiyama kimefika.

*Almu'ujamul kabir: 145, Kifayatut twalib: 296, Maqtalul Husein: 2: 89, Nadhmu duraris simtwain: 220, Majmauz zawaaid: 9/I97, al-Ittihaf bihubbil ashraf: 23I, Is-a'fur raghibin: 111, Yanaabi'ul mawaddah: 321, Ihqaqul haq: 11/479-480.*

15. Imam Husein alipouwawa mbingu ilipatwa na weusi ulionea kote, na sayari za mbinguni zikadhihiri mchana, hata Jaoza ikaonekana wakati wa alasiri, na mchanga mwekundu ukamwagika toka mbinguni, mbingu ikabaki siku saba, mchana na usiku, kana kwamba ni kipande cha damu.

*Tarikhu dimishq* 4/339 *as Sawaiqul muhriqa:* 116.

16. Kila jiwe katika mji wa Sham na Baitul maqdis lilipoinuliwa katika siku alipouwawa Imam Husein (a.s.) kulipatikana chini yake damu mbichi.

*Almu'ujamul kabir: I45, Dhakhairul uqba:145, al-Unsul jalil: 252,Wasilatul ma' aal: l97, Tah-dhibut tah-dhibu: 2/353, Kifayatut twalib: 296, Tarikhul Islam: 2/348, Siyaru a'alamin nubalaa: 3/212, Maqtalul Husein: 2/89, 90, al-Aqdul Farid: 2/220, al-Khaswaisul kubra: 2/126, Majmauz zawaaid: 9/196, Tarikhul khulafaa: 80, Miftaahun najaa:almakhtut (yaani nuskha iliyochapishwa kwa khati ya mkono), Nurul Abswaar: 123, Ihqaqul haq:11/484-488.*

17. Ndege walisusia kula katika siku ya Ashura.

*Maqtalul Husein:* 2/91 *Ihqaqul haq:* 11/.490.

18. Nuru iliangaza hadi mbinguni kutoka kwenye beseni ambayo kichwa cha Imam Husein (a.s.) kilikuwa kimewekwa, na ndege weupe walikua wakipeperuka juu ya kichwa hicho.

*Maqtalul Husein: 2/101, alKamil fit tarikh: 3/ 296, Ihqaqul haq: 11/491.*

19. Katika siku aliyouwawa Imam Husein (a.s.) kunguru alikuja na kuanguka kwenye damu yake, kisha akajipakapaka damu ile, na kupuruka hadi kwenye mji wa Madina na kujiangusha kwenye ukuta wa nyumba ya Fatima bintul Husein.

*Maqtalul Husein: 2/*92 *Ihqaqul haq: 11/*492 - 493.

20. Alipouwawa Imam Husein (a.s.) watu wengi walisikia sauti ya kilio cha majini wakimuomboleza kwa kusema:

ألا يا عين فاحتفلي بجهد * ومن يبكي على الشهداء بعدي

على رهط تقودهم المنايا * إلى متحير في ملك عبد

***

Ee jicho basi omboleza kwa juhudi
Nani awaliliae mashahidi baadangu

Minajli ya kundi liongozwalo na kifo
Huku waelekezwa kwa aliyetahayari
Katika ufalme wa mtumwa

أيهـــا القاتلون جهلاً حسيناً * أبشـروا بالعذاب والتنكيـل

كـل أهل السماء يدعو عليكم * ونبـي مرســـل وقبيل

لُعنتم على لسان ابن داود قد * وموســى وصـاحب الإنجيل

***

Enyi mliomuuwa Huseini kwa ujinga
Jibashirieni kwa adhabu na mateso
Wakazi wote wa mbinguni wawalaani
Na kila Mtume Rasuli na kila kundi
Mmelaaniwa kwa ulimi wa Ibni Dawud
Na Musa na Mtume mwenye Injili.

ويلطمن خدوداً كالدنانير نقيات * خير نساء الجن يبكين شجيات

ويلبسن ثياب السود القصيات

***

Wanawake bora majini wanalia wakiomboleza
Na kupiga mashavu yaliyosafi kama dinari
Na kuvaa nguo nyeusi walio mbali

كان حسين رجلا * أنعى حسيناً هبلا

***

Namuomboleza Husein kama chizi
Husein kweli alikuwa mwanamume

**بالطلف منعفر الخدين منحـورا * والله ما جئتكم حتى بصرت به**

**مثل المصابيح يغشون الـدجى نورا * وحــوله فتية تدمى نحورهم**

**الله يعلم أني لم أقـــل زورا * كان الحسين سراجاً يستضاء بـه**

**مات الحسين غريب الدار منفرداً * ظامي الحشاشة صادي القلب مقهورا**

*******

Wallahi sikuwajieni hadi nilipomwona Karbala

Mashavu mejaa mchanga na huku kachinjwa
Memzunguka vijana damu zawachuruza shingoni
Kana kwamba ni taa gizani zenye kujaza nuru
Husein alikuwa taa yenye kuwatia watu nuru
Mwenyezi Mungu ajua kuwa sikusema uzushi
Huseini alikufa akiwa gharibu akiwa pweke
Na ini lenye kiu, moyo ulovunika alodhulumiwa

فله بريق في الخدود * مسح النبي جبينـه

جده خير الجـدود * أبواه من عليا قريش

فأُسكِنوا نار الخلـود * قتلوك يا بن الرسول

***

Mtume kakipangusa kipaji chake
Mashavu yake yana meremeta
Wazaziwe masharifu wa Qureishi
Babu yake ni mbora wa mababu
Wamekuuwa ee Mwana wa Mtume
Wakaingizwa milele motoni

وجرت سوانحهم بغير الأسعد * عقرت ثمود ناقة فاستوصلوا

وأجل من أم الفصيـل المقعد * فبنو رسول الله أعظم حرمة

والله يملي للطغاة الجهـد * عجباً لهم لما أتوا لم يمسخوا

Thamud walimuuwa ngamia nao wakaangamizwa
Nao zikawashukia balaa bila kuwa na bahati njema
Lakini Wana wa Rasulillah wana heshima zaidi
Na watukufu kuliko mama ya mwanangamia dhaifu
Ajabu hawakubadilishwa umbo kwa kumuuwa (Husein)
Na Allah huwapa muhula madhalimu lakini hawakomi

*Almu'ujamul kabir: 147, Dhakhairul uqba:150, Tarikhul Islam:.2/349, Asmaur rijal: 2/141, Siyaru a'alamin nubalaa: 3/214, Aakaamul marjaan: 147, Nadhmu duraris simtwain: 217, 223, 2249, al-Iswaba 1/334, Majmauz zawaaid: 9/199, alBidaya wan nihaya: 6/231, 8/197, 200, Tarikhul khulafaa: 80, as Sawaiqul muhriqa: 194, Wasilatul ma'a al:197, Miftaahun najaa: 144, Yanaabi'ul mawaddah: 320, 323, 351, 352, Ash-Sharaful muabbad: 68, Kifayatut twalib: 294, 295, alMaqtal: 2/95, at-Tadhkira: 279, 280, Tarikhu ibnu Asaakir:4/341 , al-Khaswaisul kubra: 2/126, 127, Muhaadharaatul Abraar: 2/160, , Tarikhul umam wal muluk: 4/ 357, alKamil fit tarikh: 3/301, Tah-dhibut tah-dhib: 2/353, alBad-u wat tarikh: 6/10, Akhbaarud duwal: 109, Nurul qabasil mukhtasar minal muqtabas: 263, Taajul arus: 3/196, Ihqaqul haq:11/570 - 589.*

21. Imam Husein (a.s.) alipouwawa kulipatikana jiwe lililokuwa limeandikwa juu yake:

لابد أن ترد القيامة فاطمة * وقميصها بدم الحسين ملطخ

ويل لمن شفعاؤه خصماؤه * والصور في يوم القيامة ينفخ

Ni lazima Fatima aje Qiyama Na huku nguo yake imelowa
Kwa damu ya (Imam) Husein Ole wake ambaye waombezi
Wake ndio makhasimu wake Qiyama itapopigwa tarumbeta

*at-Tadhkira:284, Nadhmu duraris simtwain:219, Yanaabi'ul mawaddah: 331, Ihqaqul haq:11/569.*

22. Kuta za ya nyumba ya utawa (kanisa) zilipatikana zikiwa zimeandikwa juu yake:

أترجو أمة قتلوا حسيناً شفاعة جده يوم الحساب

Je umma uliomuuwa Husein vipi unatarajia
Kupata uombezi wa Babu yake siku ya Qiyama

Na walipomuuliza mtawa kuhusu maandiko hayo na kuwa ni nani aliye yaandika akasema: Yaliandikwa miaka mia tano kabla ya kutumwa kwa Mtume wenu (wa dini ya Uislamu).

*Tarikhul Islam war rijaal: 386, al-Akhbaarut twiwal: 109, Hayatul hayawan: 1/60, Nurul Abswaar: 122, Kifayatut twalib: 290, Ihqaqul haq: 11/567-568.*

23. Mtu katika watu wa Najran alipochimba shimo alipata ndani yake bamba la dhahabu lililo kuwa limeandikwa juu yake:

أترجو أمة قتلوا حسيناً شفاعة جده يوم الحساب

Je umma uliomuuwa Husein vipi unataraji

Kupata uombezi wa Babu yake siku ya Qiyama

*Miftaahun najaa: 144Ihqaqul haq: 11/566.*

24. Ukuta mmoja ulipasuka na kiganja cha mkono kikatokea kilichokuwa kimeandikwa ndani yake kwa damu:

أترجو أمة قتلوا حسيناً   شفاعة جده يوم الحساب

Je umma uliomuuwa Husein vipi unataraji
Kupata uombezi wa Babu yake siku ya Qiyama

*Tarikhul khamis: 2; 299, Ihqaqul haq: 11/567.*

25. Baada ya ya kumuuwa Imam Husein (a.s.) na kukikata kichwa chake walipoketi katika kituo chao cha kwanza ili kunywa pombe ya nabidhi (divai) kulidhihiri mkono kutoka kwenye ukuta ukiwa umekashika kalamu ya chuma na kuandika kwa damu mstari wa maneno haya:

أترجو أمة قتلوا حسيناً   شفاعة جده يوم الحساب

Je umma uliomuuwa Husein vipi unataraji
Kupata uombezi wa Babu yake siku ya Qiyama

*Almu'ujarnul kabir: 147, Dhakhairul uqba: 144, Maqtalul Husein: 2/93, Mahaadhirul abraar: 2/160, Kifayatut twalib: 291, Tarikh Dimishq: 4/342, Tarikhul islam: 3/13, Majmauz zawaaid: 9/199, Albidaaya wan Nihaaya: 8/200, as Sawaiqul muhriqa: 116, al-Khaswaisul kubra: 2/l27, at-Tabaqaatul kubra: I/23,*

*Jam-ul fawaaid: 2/217, Wasilatul Ma'aal: 197, al-araisul waadhiha: 190, Is-a'fur raghibin: 217, Yanaabi'ul mawaddah:230,35, Jaaliyatul kadir:198, Ihqaqul haq:11/561-565.*

26. Walipata jiwe lilikulowa na maandiko yaliyokuwa yameandikwa miaka elfu moja kabla ya Mtume (s.a.w.a.) kuteuliwa kuwa Mtume: (na maandiko haya yalikuwa kwenye baadhi ya makanisa ya Roma miaka mia tatu - au mia sita- kabla kuteuliwa kwake (s.a.w.a.))

أترجو أمة قتلوا حسيناً   شفاعة جده يوم الحساب

Je umma uliomuuwa Husein vipi unataraji
Kupata uombezi wa Babu yake siku ya Qiyama

*Almu'ujarnul Kabir: 147, Kifayatut twalib: 290, Maqtalul Husein: 2/93, Albidaaya wan nihaaya: 8/200, Majmauz zawaaid: 9/l99, Tarikh Dimishq: 4/342, at-Tadhkira: 283, Nadhmu duraris simtwain: 291, Ma-athirul inaafa fi Ma'alimil khilaafa: 117, Yanaabi'ul mawaddah: 331, Mukhtasaru tadhkiratul qurtubi: 194, Ihqaqul haq: 11/557-560.*

27. Mtume (s.a.w.a.) aliipaka wanja macho ya mtu kwa damu ya Imam Husein (a.s.) ndotoni, akapofuka, kwa sababu ya kuwa alikuwa amehudhuria mauaji ya Imam Husein (a.s.):

*Nurul Abswaar: 123, as Sawaiqul muhriqa: 117, 194, Is-a'fur raghibin: 192, at-Tadhkira: 291, Maqtalul Husein: 2/104, Rashafatus swaadi: 291, Yanaabi'ul mawaddah:*

*330, Ihqaqul haq: 11/552-555.*

28. Abu Rajaa alisema: Msimtukane Ali, wala watu wa nyumba hii, kwani mtu katika Bani alHajim (kwani jirani wa Balhajim)[1] alikuja kutoka al-Kufa na kusema: "Je hamjamuona huyu fasiki mwana wa fasiki!!! Hakika Mwenyezi Mungu amemuuwa!!! - Akimaanisha Husein ibnu Ali (a.s.) - Mwenyezi Mungu (akamwadhibu) akayatia weupe macho yake na kuyapofusha.

*alManaqib cha Ahmad ibnu Hambal: makhtut (yaani nuskha iliyochapishwa kwa khati ya mkono), alMu'ujamul kabir: 145, Tarikh Dimishq: 4/430, Kifayatut twalib: 296, as Sawaiqul muhriqa: 194, Majmauz zawaaid: 9/197, Akhbaarud duwal: 109, alMukhtaar: 22, : Tah-dhibut tah-dhib: 2/353, Siyaru a'alamin nubalaa:3/211, Tarikhul islam: 2/348, Nadhmu duraris simtwain: 220, Miftaahun najaa: 151, Rashafatus Swaadi: 63, Yanaabi'ul mawaddah: 220,*

29. Kila aliyehusika katika kumuuwa Imam Husein (a.s.) alipata adhabu humu duniani, ima kwa kuuwawa au kupofuka au uso kuwa mweusi, au kupoteza utawala wake baada tu ya muda mfupi.

*at-Tadhkira: 290, Nurul Abswaar: 123, Is-a'fur raghibin: 192, Yanaabi'ul mawaddah: 322, Ihqaqul haq:11/ 513.*

30. Mtu mmoja aliyemfanyia Imam Husein (a.s.) kizuizi ili asiyafikiye maji, aliadhibiwa kwa ugonjwa wa kiu,

[1] - Kama ilivyo kwenye nuskha nyingine.

baada ya Imam Husein (a.s.) kumuombea laana kwa kusema: Ewe Allah, mpatishe kiu!! Ewe Allah, mpatishe kiu!! Basi alikuwa akilia kwa kupaza sauti kutokana na joto (la kuunguza) tumboni mwake na baridi mgongoni mwake hata mwishowe tumbo lake likapasuka pande mbili mfano wa kupasuka kwa ngamia.

*Maqtalul Husein: 2/91, Dhakhairul uqba: 144, as Sawaiqul muhriqa: 195, Mujaabid da'awa: 38, Ihqaqul haq: 11/514-515.*

31. Mtu mmoja alipomwambia Imam Husein (a.s.): "Jibashirie kuingia motoni" Imam Husein (a.s.) alimwombea laana na kusema: "Ee Mola wangu!! Mtumbukize motoni," ghafla farasi wake akasisimuka na kumuangusha kwenye kijito cha maji, mgu wake ukakwama na kuning'inia kwanye kikuku cha kumpandia farasi, na kichwa chake kuanguka ardhini, farasi akakimbia huku anamburuta, akawa anakipigisha kichwa chake kwenye kila jiwe na kila mti hadi kuaga dunia.

*Tarikhul umam wal muluk: 4/327, alMu'ujamul kabir: 146, Maqtalul Husein: 2/94, Dhakhairul uqba: 144, alkaamil fit tarikh: 3/289, Kifayatut twalib: 287, Wasilatul Ma'aal: 197, Yanaabi'ul mawaddah: 342, Ihqaqul haq: 11/ 516-519.*

32. Walipomzuia maji Imam Husein (a.s.) mtu mmoja alimwambia: "Yaangalie (hayo maji) kana kwamba ni mbingu iliyombali.Hutayaonja hata tone moja, hata ufe kwa kiu," Imam Husein (a.s.) akamwambia: "Ewe Allah!! Muuwe kwa kiu," basi akawa hata

pamoja na kunywa maji kwa wingi lakini kiu hakimwishi, hadi akafa kwa kiu.

*as Sawaiqul muhriqa:195, Ihqaqul haq:11/520.*

33. Kufa watu kwa kiu waliomzuia maji Imam Husein (a.s.).
    Mtu mmoja akawa kipofu na mikono yake miwili pamoja na miguu yake ikakatika na kuanguka, baada ya kumuona Bibi Fatima (a.s.) kwenye ndoto na kumuombea laana, kwa kuwa alitaka kuupora mshipi (wa kiunoni) wa Imam Husein (a.s.).
    Kukatika kwa mkono wa mtu aliyekipora kilemba cha Imam Husein toka kwenye kiwiko na kubaki kwake akiwa fakiri mwenye hali mbaya sana hadi alipofariki.
    Mtu mmoja alipatwa na wazimu na ulimi wake kupoteza nguvu za kuzungumza aliposema: "Mimi ndiye muuwaji wa Imam Husein."

*alBidaaya wan nihaaya: 8/174, Yanaabi'ul mawaddah: 348, Maqtalul Husein: 2/34, 94, 103, Tarikhu Dimishq: 4/340, alkaamil fit tarikh: 3/283, alMu'ujamul kabir: 146, Dhakhairul uqba: 144, Kifayatut twalib: 287, Wasilatul Ma'aal: 196, Ihqaqul haq: 11/522-525, 528-530.*

34. Aliyempora Imam Husein (a.s.) akapatwa na ugonjwa usiokwisha, na miguu yake kupooza, na aliye kichukua kilemba chake akapatwa na ukoma, na aliyeichukua deraya yake akapatwa na upungufu wa akili, na katika wakati huo vumbi kali na jeusi likapanda na kutandaa hadi mbinguni, lenye upepo mwekundu ndani yake, hakuna kilichoweza

kuonekana ndani yake, hata watu hao wakadhani kuwa adhabu imewashukia.

*Maqtalul Husein: 2/37, Ihqaqul haq: 11/526.*

35. Kichwa chake Imam Husein (a.s.) kilipoletwa kwa Yazid (laanahullah) na kuwekwa mbele yake, kulitokea ganja la mkono kwenye ukuta na kuandika kwenye kipaji chake:

شفاعة جده يوم الحساب   أترجو أمة قتلوا حسيناً

Je umma uliomuuwa Husein vipi unataraji
Kupata uombezi wa Babu yake siku ya Qiyama

*Ghurarul khaswaisil wadhiha: 276, Ihqaqul haq: 11/456.*

36. Kichwa cha Ibnu Ziyad kilipoletwa pamoja na vichwa vya wafuasi wake na kutupwa mbele ya alMukhtar, ghafla nyoka mmoja alitokezea na kupita kati ya vichwa vyote hadi mwishowe kuingia kwenye kinywa cha kichwa cha Ibnu Ziyad na kutoka kupitia kwenye pua lake, kisha akaingia kwenye pua na kutoka kupitia kwenye kinywa, kikawa kinaingia na kutoka kwenye kichwa chake, hata watu wakasema: "Ubeidullah na wafuasi wake hawakufaulu, na wamepata hasara ya duniani na akhera."Kisha waliangua kilio na kupaza sauti na kumuomboleza Imam Husein (a.s.) na wananawe na maswahaba wake.

*Swahihut tirmidhi: 13/97, Maqtalul Husein: 2/84, Usudul ghaaba: 2/22, alMu'ujamul Kabir: 145,*

*Dhakhairul uqba: 128, Siyaru a'alamin nubalaa: 3/359, Mukhtasaru tadhkiratil qurtubi: 192, Jaamiul usul: l0/25, as Sawaiqul muhriqa: 196, Nadhmu duraris simtwain: 220, Umdatul qaari: l6/241, Yanaabi'ul mawaddah: 231, Is-a'fur raghibin: 185, Nurul abswaar: 126, Ihqaqul haq: 11/542-545.*

37. Harmala alibadilika na kuwa mwenye sura mbaya sana yenye kuchukiza na nyeusi mno, na ulikuwa haupiti usiku ila tu alikuwa akichukuliwa na kupelekwa kwenye moto uliowashwa na kutupwa ndani yake.

    *at-Tadhkira:* 291, *Yanaabi'ul mawaddah:* 330, *Is-a'fur raghibin:* 192, *Nurul abswaar:* 123, *Ihqaqul haq:11/*.531-532.

38. Mtu mmoja aliposema: "Hakuna yeyote aliyehusika katika mauaji ya Husein ila tu alikumbwa na balaa kabla ya kufa kwake," mzee mmoja alisema: "Mimi ni miongoni mwa walioshuhudia mauaji yake, na wala sijakumbwa na jambo lenye kunichukiza hadi sasa."
    Mara taa ikazima, akasimama kuirekebisha, ghafla moto ukamshika, akatoka mbio akiuelekea mto wa Furati na kujitumbukiza ndani yake, lakini aliungua na kuwa kama mkaa.

    *Maqtalul Husein:* 62, *Tah-dhibut tah-dhibu:*2/353, alMukhtaar: 22, *Tarikhu Dimishq: 4/*340, *Kifayatut twalib:* 279, *at-Tadhkira:* 292, *Wasilatul Ma'aal:* 197, *Nadhmu duraris simtwain:* 220, *Siyaru a'alamin nubalaa:* 3/211, *as Sawaiqul muhriqa:* 193, *Yanaabi'ul mawaddah:* 322, *Miftaahun najaa:*

*almakhtut (yaani nuskha iliyochapishwa kwa khati ya mkono), Is-a'fur raghibin:* 191, *Ihqaqul haq:11/*536-539.

39. Imam Husein (a.s.) alipouwawa mti uliokuwa umemea kwa muujiza wa Mtume (s.a.w.a.) ulikauka baada ya shina lake kububujika kwa damu mbichi, na matawi yake kufa baada ya kuchuruzisha damu kama supu ya nyama.

    *Rabiul abraar: 44, at-Tuhfal aliyya wal aadaabul ilmiyya: 16, Maqtalul Husein 2/98, Ihqaqul haq: 11/494-497.*

40. Manjano iliyochukuliwa kutoka kwa majeshi wa Imam Husein (a.s.) ilibadilika na kuwa jivu.

*alMu'ujamul kabir: 147, Siyaru a'alamin nubalaa: 3/21I, Tarikhul islam: 2/ 348, Tah-dhibut tah-dhibu: 2/353, Maqtalul Husein: 2/90, Dhakhairul uqba: 144, Majmauz zawaaid: 9/197, as Sawaiqul muhriqa: 192, Nadhmu duraris simtwain: 220, al-Khaswaisu: 2/126, Yanaabi'ul mawaddah:321, Ihqaqul haq:11/503-505.*

41. Waligawana nyama ya ngamia wa kike waliyekuwa wamemchukua kutoka kwenye kambi la jeshi lake, mara sufuria waliyokuwa wakipikia ikawaka moto. Waliweka baadhi ya mali aliyoiacha Imam Husein (a.s.) kwenye bakuli, ikabilika na kuwa moto. Nyama ya ngamia waliyoiiba kutoka kutoka kwa askari jeshi wa Imam Husein (a.s.) ilibadilika na kuwa chungu kama machungu tango.

*Nadhmu duraris simtwain*: *220, alMahaasin wal masaawi: 62, alMu'ujamul kabir:* 147, *Majmauz zawaaid:* 9/96, *Tarikh Dimishq: /*340, *Tarikhul Islam:* 2/348, *as Sawaiqul muhriqa:* 3/2I1, *Tah-dhibut tah-dhibu:* 2/353, *al-Khaswaisul kubra:* 2/126, *Tarikhul khulafaa:* 80, *Maqtalul Husein:* 2/90, *at-Tadhkira:* 277, *Nurul abswaar:* 123, *Ihqaqul haq: 11/506-510.*

42. Imam Husein (a.s.) alipouwawa na kichwa chake kuletwa kwa Ibnu Ziyad, alisema: "Ni nani kati yenu ndiye aliyemuuwa." Mtu mmoja aliposimama na kusema: "Mimi ndiye nilimuuwa," ghafla uso wake ulibadilika na ukawa mweusi sana.

*Dhakhairul uqba:* 149, *Ihqaqul haq: 11/540.*

43. Nuru iliangaza usiku wa manane kutoka mahali kilipokuwa kichwa cha Imam Husein (a.s.) hadi mbinguni, kitu kilicho sababisha mtawa wa kikristo kusilimu.

*at-Tadhkira:273, Maqtalul Husein:2/102, as Sawaiqul muhriqa:119,Rashafatus swadi:163, Yanaabi'ul mawaddah:320, Ihqaqul haq:11/498-502.*

44. Imam Husein (a.s.) alipouwawa, kesho yake kulipokucha, kila chakula walichokuwa wamekipika walipata kuwa kimebadilika na kuwa damu, na vile vile, kila chombo chao kilichokuwa na maji kilikuwa kimebadilika kuwa damu.

*Nadhmu duraris simtwain: 220, Ihqaqul haq: 11/502.*

45. Mwanamke yeyote aliyejipaka marashi yaliyokuwa yameporwa kutoka kwa kambi la jeshi la Imam Husein (a.s.) alipatwa na ukoma.

*al-Aqdul fariid: 2/220, Uyunul akhbar: 1/212, Ihqaqul haq:11/511.*

Haya ni machache tu katika yaliyonukuliwa kutoka kwenye vitabu vya Ahlus sunna, na ama katika vitabu vya kishia, kumetajwa alama nyingi mno zilizo dhihiri baada ya shahada ya Imam Husein (a.s.), tunataja baadhi yazo kama ifwatavyo:

46. Imam Husein (a.s.) alipouwawa bundi alijiwekea kiapo kuwa hatowahi tena kuishi kwenye nyumba nzuri, bali atakuwa akiishi kwenye nyumba zilizoharibika, na mchana wake atakuwa daima kwenye saumu na mwenye huzuni hadi usiku uanapoingia, nao usiku unapoingia atakuwa daima katika hali ya kumuomboleza Imam Husein (a.s.).Kabla ya kuuwawa Imam Husein (a.s.) alikuwa akiishi kwenye majumba na mijengo na makasri, na watu walipokuwa wakila chakula alikuwa akipuruka na kutua mbele yao, wanamtupia chakula na kinywaji, kisha anarudi wakazi yake.

47. Imam Husein (a.s.) alipouwawa njiwa wenye sauti za kutisha walianza kuwaombea laana wauwaji wa Imam Husein (a.s.).

48. Imam Husein (a.s.) alipouwawa mbingu ilinyesha damu na majivu.

49. Imam Husein (a.s.) alipouwawa mbingu ilinyesha

mchanga mwekundu.

50. Imam Husein (a.s.) alipouwawa, watu wa baitul maqdis, kila walipoliliinua jiwe au udongo au mwamba walipata chini yake damu yenye kuchemka, na kuta zilikuwa nyekundu kama pande la damu, na watu walinyeshewa na mvua ya damu mbichi.

51. Imam Husein (a.s.) alipouwawa malaika elfu nne walishuka, wakabaki kando ya kaburi yake wakiwa wenye mavumbi na nywele zisizo chanwa, wenye kulia hadi siku ya Qiyama – atakapo dhihiri alQaim (a.j.) – na kiongozi wao ni malaika aitwaye Mansur.

52. Imam Husein (a.s.) alipouwawa wekundu ulipanda kutoka upande wa mashariki na wekundu mwingine kutoka upande wa magharibi, ukakaribia kukutana katikati mbinguni.

53. Imam Husein (a.s.) alipouwawa watu walikaa siku arobaini, jua likichomoza likiwa jekundu na kuzama likiwa jekundu, hii ikiwa ndiyo alama ya kulia kwake.

54. Imam Husein (a.s.) alipouwawa mbingu ilinyesha damu, hata mitungi na magudulia yakajaa kwa damu, ngamia walipoenda kwenye bonde ili kunywa maji, wakapata kuwa ni damu.

55. Mbingu haikumlilia mtu yeyote isipokuwa Yahya ibnu Zakariya (a.s.), na Husein ibnu Ali (a.s.) na kilio

cha mbingu kilikuwa ni kwamba, ilipokuwa ikielekezewa nguo kulikuwa kunamwagika kwenye nguo ile damu kutoka mbinguni na kuacha athari mfano wa athari ya kiroboto kwenye nguo ile.

56. Imam Husein (a.s.) alipouwawa, mbingu saba na ardhi saba zilimlilia pamoja na vyote vilivyomo ndani yazo na vilivyomo baina yazo na vyote vilivyomo peponi na motoni na vyote vionekanavyo na vyote visivyo onekana.

57. Imam Husein (a.s.) alipouwawa, vitu vyote vilimlilia , hata wanyama wa nchi kavu na samaki wa baharini na ndege wa angani.Jua pia lilimlilia pamoja na mwezi na nyota na mbingu na ardhi na waumini wote kati ya majini na watu, pamoja na Malaika wote wa mbinguni na wa ardhini, na Malaika Ridhwan na Malaika wanaoibeba Arshi ya Mwenyezi Mungu.

58. Imam Husein (a.s.) alipouwawa, wanyama wakali walizinyoosha shingo zao na kuzielekeza kwenye kaburi lake Imam Husein (a.s.) wakimlilia na kumuomboleza usiku wote hadi asubuhi.

59. Imam Husein (a.s.) alipouwawa, mbingu ilimlilia kwa damu, kwa muda wa asubuhi arobaini, na ardhi ikamlilia kwa kudhihirisha weusi na jua kwa wekundi, nayo milima ikapasuka na kuporomoka, na mabahari kulipuka, na Malaika walioko kando ya kaburi yake ni wenye kulia kiasi cha kumfanya kila Malaika aliye hewani na mbinguni kulia kutokana na kilio chao.

60. Amirul Muumin (a.s.) alipokuwa akiisoma aya hii:

(فَمَا بَكَتۡ عَلَيۡهِمُ ٱلسَّمَآءُ وَٱلۡأَرۡضُ وَمَا كَانُواْ مُنظَرِينَ)

(Na mbingu na ardhi hazikuwalilia, wala hawakuwa na ni wenye kucheleweshwa)[1] Imam Husein (a.s.) alimtokezea, Amirul Muumin (a.s.) akasema: Ama huyu, kwa hakika atauwawa, na mbingu na ardhi kumlilia.

61. Bibi Fatima (a.s.) anamlilia kwikwi Imam Husein (a.s.).

62. Imam Husein (a.s.) alipouwawa, Majini walimuomboleza kwa kusema mashairi haya:

إن الرماح الواردا صدورها     نحو الحسين تقاتل التنــزيلا
ويهللون بأن قتل وإنــمــا     قتلوا بك التكبير والتهليــلا
فكأنما قتلوا أباك محمــدا     صلى عليه الله أو جبــريلا

Mikuki imevielekeza vifua vyake
Aliko Huseini ili kupigana na Qurani
Wanatamka Tahlili kuwa umeuwawa

---

[1]- Suratud dukhan, aya ya 29.

Bali wameuwa Takbiri naTahlili
Kwa kukuuwa wewe kana kwamba
Wamemuuwa Babu yako Muhammad
Amani ya Allah imshukie au Jibrili
***

**خير العمومة جعفر الطيــار     يا بن الشهيد ويا شهيداً عمه**
**عجباً لمصقولٍ أصابك حده     في الوجه منك وقد علاك غبا**

Mbora wa wajomba ni Ja’afar Twayyar
Ee mwanae Shahid na Shahidi amuye
Ajabu kuwa ncha za upanga zilikuswibu
Kwenye uso na huku vumbi limekufinika

***

أيا عين جودي ولا تجمـدي     وجودي على الهالك السيـــد
فبالطف أمسى صريعاً فقد     رزئنا الغداة بأمـــرٍ بدي

Ewe jicho kirimu wala usikauke
Mkirimu chozi Seyyidi aleuwawa
Jioni imemfika ashauwawa Karbala
Tumekuchwa kwa msiba uliotutokea

***

**نساء الجن يبكين من الحزن شجيات وأسعدن بنوح للنساء الهاشميات**
**ويندبن حسيناً عظمت تلك الرزيات     ويلطمن خدوداً كالدنانير نقيات**

ويلبسن ثياب السود بعد القصبيات

Wanawake majini wanalia kwa huzuni wakiomboleza
Wamepata saada ya kuomboleza na wanawake wa kihashimiya
Wanamuomboleza Husein wakisema ni adhimu kweli hiyo misiba
Na wanayapiga mashavu yaliyosafi kama dinari
Na kuvaa nguo nyeusi baada ya kuvaa za Hariri.

*alManaqib cha Ibnu Shahri ashub: juzuu ya 4 kuanzia ukurasa 754 na kuendelea, Kaamiluz Ziyaara: 75 na kuendelea, Aamaalus swaduq: majlisi ya 27, IlaIush Sharaayi'i: 1/2 17, Aamaalul mufid, Bihaarul anwaar: 45/201-241, na katika vitabu vingine vingi.*